

# UNABII WA HABARI ZA BIBLIA

*Mwana Filadelfia  
wa Karne ya 21 ni nani?*

**Kamari na Dhambi:**

*Je, ni dhambi kwa Mkristo kucheza kamari?  
Ni akina nani ambao hucheza kamari zaidi?*


**Iraq katika Unabii:**

*Iraq imekuwa ikitajwa sana katika vyombo vya  
habari siku za karibuni.  
Je, Biblia inafundisha ni kipi kitakachotokea huko?*

# HABARI ZA UNABII WA BIBLIA



8



13




24



25



28



33

## KATIKA TOLEO HILI:

- 3 MwanaFiladelfia wa Karne ya 21 ni nani?** Je, Yesu alifundisha kwamba kungekuwepo na tofauti kubwa baina ya Wakristo wakati wa enzi za nyakati za mwisho? Baadhi ya viashiria vya MwanaFiladelfia ni vipi?
- 8 Kamari na Dhambi:** Je, ni dhambi kwa Mkristo kucheza kamari? Ni akina nani ambao huchoza kamari zaidi?
- 13 Kozi ya Jifunze Biblia Somo la 4** Hili ndilo somo la nne la kozi hii, ili kuwasaidia watu wajisomee Biblia na kuelewa vema zaidi
- 24 Siku Iliyo Kipenzi Kwangu** Ni kwanini Sabato ndiyo siku iliyo kipenzi kwa John Hickey?
- 25 Upatanisho na Mfungo:** Ni kwanini huwa tunafunga kwenye Sikukuu ya Upatanisho? Je, kuna faida zozote za kiafya zinazotokana na kufunga?
- 28 Iraq katika Unabii:** Iraq imekuwa ikitajwa sana katika vyombo vya habari siku za karibuni. Je, Biblia inafundisha ni kipi kitakachotokea huko?
- 33 Encyclopedia ya Kikatholiki juu ya Krisimasi:** Wakatholiki huisherehekea sikukuu ya Krisimasi, lakini wasomi wao wanafahamu juu ya baadhi ya kweli zinazoihusu.

**Jarida la Nyuma: Tovuti na Radio** Hili linaonyesha ni wapi watu wanaweza kuupata ujumbe kutoka Kanisa la Continuing Church of God.

**Kuhusu Jarida la Mbele:** Baadhi ya mabaki ya mji wa Filadelfia. Filadelfia ulikuwa ni mji wa kale uliokuwepo kwenye njia kuu ya kusambazia barua ya Kirumi na ulikuwa ni mmojawapo miongoni mwa makanisa saba yaliyoandikiwa ujumbe maalum katika Kitabu cha Ufunuo. Pamoja na kwamba kanisa la Continuing Church of God lilijengwa juu ya msingi wa mitume na manabii, Yesu Kristo akiwa ndiye jive kuu la kwenye msingi huo (Waefeso 2:20), linawakilisha masalia muhimu ya zama za WanaFiladelfia katika kipindi hiki cha kushamiri kwa Wanalaodikia. Photo na Joyce Thiel.

Unabii wa Habari za Biblia huchapishwa na Kanisa la Continuing Church of God, 1248 E. Grand Avenue, Suite A, Arroyo Grande, CA, 93420. <http://www.ccog.org>  
©2014 Continuing Church of God. Limechapishwa katika U.S.A. Haki zote zimehifadhiwa.

Kunakiri makala yote ama sehemu yake pasipo ruhusa ya kimaandishi toka kwa mmiliki hairuhusiwi. Tunaheshimu haki zako hivyo hatutoi, kuuza ama kukodisha orodha ya mawasiliano yetu. Endapo haungependa kuendelea kupokea gazeti hili, wasiliana na office yetu iliyo Arroyo Grande. Maandiko yamenukuriwa toka New King James Version (©Thomas Nelson, Inc., Publishers, used by permission) Isipokuwa pale tu tumeelekeza vinginevyo.

Unabii wa Habari za Biblia-HUWEZESHA KWA MICHANGO YENU

Bible News Prophecy has no subscription or newsstand price. This magazine is provided free of charge by the Continuing Church of God. It is made possible by the voluntary, freely given tithes and offerings of the membership of the Church and others who have elected to support the work of the Church. Contributions are gratefully welcomed and are tax-deductible in the U.S. Those who wish to voluntarily aid and support this worldwide Work of God are gladly welcomed as co-workers in this major effort to preach and publish the gospel to all nations. Contributions should be sent to: Continuing Church of God, 1248 E. Grand Avenue, Suite A, Arroyo Grande, CA, 93420.

Mhariri Mkuu: Bob Thiel

Mpigachapa/Mhariri Msaidizi: Joyce Thiel

Masahihisho na: John Hickey

Maandalizi & Uchapaji: Burdine Printing

Picha: Picha zote zimetokana na familia ya Thiel ama na vyanzo vya mitandao ya kijamii kama vile Wikipedia (ikiwa chanzo hakikutajwa, itakuwa ni kwa sababu inaaminika kwamba chanzo husika kililichia picha iwe kwa matumizi ya umma pasipo masharti yeyote).

## MWANA FILADELFIA NI NINI? MWANA FILADELFIA WA KARNE YA 21 NI NANI?

Kwa nini hili ni la muhimu kulijua? Je, Biblia inafundisha nini juu ya hili? Ni kwa namna gani historia ya kanisa yaweza kusaidia katika kulielewa hili?

Kitabu cha Ufunuo ni kitabu cha kiunabii. Kinaanza kwa kuandika: “Ufunuo wa Yesu Kristo, ambao Mungu alimpa ili awaonyeshe watumishi wake – mambo ambayo hayana budi kuweco upesi” (Ufunuo 1:1).

Katika sura ya 2 & 3, kitabu cha Ufunuo kinaonyesha mfuatano, katika maelezo ya hatua kwa hatua, juu ya makanisa saba, kilamoja likiwa na nguvu na udhaifu tofauti na jingine (ikiwemo na mwelekeo utakaonekana katika kipindi chote cha kanisa). Pamoja na mitazamo ya wanaopindisha maana na wengineo, Kitabu cha Ufunuo kwa hakika ni kitabu cha kiunabii (Ufunuo 1:3). Kwa kuwa taarifa kadhaa zilizotolewa kwa makanisa saba (mfano: Ufunuo 1:19; 3:3; 3:10) kiujumla zisingekuwa zilikusudiwa zikamilike katika makanisa hayo zilikokuwa zimeelekezwa wakati wa mwisho wa karne ya 1, maandiko yenyewe yanathibitisha kwamba nyingi baina ya taarifa kwa makanisa hayo zilikuwa ni za kiunabii, na baadhi ya nabii hizo zikiwa zililenga kwa wale watakoishi katika karne ya 21.

Biblia inaonyesha wazi kwamba Yesu anatembea katikati ya makanisa haya saba (Ufunuo 1:9-13), ikionyesha kwamba kwa namna fulani makanisa haya yanawakilisha kanisa lake katika kipindi chote cha kanisa. Ukweli kwamba ni makanisa saba ndiyo yamepelekewa ujumbe na namba saba huwakilisha ukamilifu, pamoja na ukweli kwamba makanisa hayo yametajwa katika mfuatano uleule wa jinsi yangepokea mawasiliano katika enzi za Warumi, inapatana na mtazamo kwamba makanisa haya yalikuwa yawakilishe kanisa la kweli katika nyakati zote kwa mfuatano uleule kupitia vipindi vyote.

Nyaraka kwa Makanisa ya Ufunuo 2 & 3 zinatakiwa zieleweke katika mtazamo wa kiunabii, na zinazungumzia kuhusu Kanisa lililoko Filadelfia pamoja na mengine pia.

### Yesu aliliambia nini Kanisa la Filadelfia?

Jionee kile ambacho Yesu aliliambia Kanisa lililokuwa Filadelfia:

7“Kwa malaika wa kanisa lililoko Filadelfia andika: Haya ndiyo maneno Yake Yeye aliye mtakatifu na wa kweli, Yeye aliye na ufunguo wa Daudi. Anachokifungua hakuna awezaye kukifunga, wala anachokifunga hakuna awezaye kukifungua. 8Najua matendo yako. Tazama, nimeweka mbele yako

mlango uliofunguliwa, wala hakuna awezaye kufungua. Ninajua kwamba una nguvu kidogo lakini umelishika neno Langu wala hukulikana Jina langu. 9Nitawafanya wale wa sinagogi la Shetani, wale ambao husema kuwa ni Wayahudi lakini sio, bali ni waongo, waje wapige magoti miguuni pako, nao watajua ya kwamba nimekupenda. 10Kwa kuwa umelishika neno la saburi Yangu nitakulinda hata utoke katika saa ya kujaribiwa inayokuja ulimwenguni pote ili kuwajaribu wote wakao duniani. 11Ninakuja upesi. Shika sana ulicho nacho, ili mtu asije akaichukua taji yako. 12Yeye ashindaye nitamfanya kuwa nguzo katika hekalu la Mungu wangu, wala hatatoka humo kamwe. Nitaandika juu yake Jina la Mungu wangu na jina la mji wa Mungu wangu, yaani, Yerusalemu mpya, ambao unashuka kutoka mbinguni kwa Mungu wangu. Nami pia nitaandika juu yake Jina langu jipya. 13Yeye aliye na sikio na asikie yale ambayo Roho anayaambia makanisa” (Ufunuo 3:7-13).

Yesu hapa anasema kwamba yeye “Anao ufunguo wa Daudi”, na anazungumzia akiashiria milango. Kielelezo juu ya “ufunguo wa Daudi” pamoja na milango zimetumiwa kwa pamoja katika eneo jingine la Biblia:

20“Katika siku ile nitamwita mtumishi wangu, Eliakimu mwana wa Hilikia. 21Nitamvika joho lako nami nitamfunga mshipi wako kiunoni mwake na kumkabidhi mamlaka yako. Yeye atakuwa baba kwa wale wanaoishi Yerusalemu na kwa nyumba ya Yuda. 22Nitaweka mabegani mwake ufunguo wa nyumba ya Daudi, kile afunguacho hakuna awezaye kufunga na kile afungacho hakuna awezaye kufungua. 23Nitamgongomea kama kigingi kilicho mahali palipo imara, naye atakuwa kiti cha enzi cha heshima kwa ajili ya nyumba ya baba yake (Isaya 22:20-23).

Hili, miongoni mwa mambo mengine, linaashiria kwamba “ufunguo wa Daudi” unahusika na utawala na pia na kiti cha enzi. Hili lingehusianaje na kipindi cha Kanisa cha Filadelfia katika karne ya 21?

### Lini Enzi za Filadelfia Zilianza

Kuzipitia nyaraka mbalimbali zinazohusu enzi za kanisa za “Sardi” (Ufunuo 3:1-6) zinaonyesha kwamba hakukuwepo na uongozi thabiti kwenye kanisa hilo (soma pia, True History of the True Church na A.N. Dugger na C.O. Dodd). Katika kitabu cha Autobiography of Herbert W. Armstrong (nakili zote zimetokana na chapa ya 1973), marehemu Herbert W. Armstrong aliandika:

Wachungaji walikuwa wakiajiliwa, na kuwa chini ya mamlaka ya waumini. Hii ndiyo aina ya uongozi ambayo leo ndiyo huitwa kuwa ni demokrasia: serkali ambayo madaraka yake hutoka chini kwenda juu. Wale wanaoongozwa huwaamrisha walio viongozi wao. Somo lililonitatanisha kupita yote katika Biblia lilikuwa hili swala la uongozi wa

kanisa. Sikuwa nimefikia kulielewa vema fundisho la BIBLIA juu ya swala hili hadi baada ya Chuo cha Ambassador College kilipokuwa kimeanzishwa (kurasa 411-412).

Elewa kwamba pale kanisa la Church of God Seventh Day (CG7) lilipogawanyika kutokana na kutofautiana juu ya mfumo wa uongozi mwaka 1933, Herbert Armstrong hakuambatana na kundi lililokuwa limepata kura nyingi zaidi, lakini, aliendelea kushirikiana japo kwa mbali, na kundi lililokuwa limepata kura chache (Toka: Mystery of the Ages, kur. 558, 561). Vilevile aliandika:

Niliendelea kuabudu na kushirikiana na ndugu waliokuwa kule West Coast waliokuwa wa kipindi cha enzi za Sardi hadi mwaka 1942, pale ambapo kazi iliyokuwa ikipanuka kwa kazi ya enzi za Filadelfia ilipokuwa inahitaji muda wangu wote. Enzi hii mpya kimsingi ilianza katika mwezi Octoba, 1933 (Toka: Worldwide News, Juni 24, 1985).

Herbert Armstrong alijitenga na kanisa la CG7 kimsingi kutokana na tofauti ya kiimani pamoja na ukweli kwamba kwake yeye ilionekana kama kanisa la CG7 halikuonekana limeweka mkazo kama lengo lake la kwanza, kuipeleka Injili ya Ufalme kwa ulimwengu kama ushuhuda. Kitabu cha maisha yake (autobiography) kinanukuru barua kutoka kwa mmoja wa viongozi wakuu wa kanisa la CG7 aliyoiandika akielezea kwamba kanisa la CG7 halikuwa tayari kufundisha juu ya kwamba Waingereza pamoja na Wamarekani ni Waisraeli waliotokana na Efraimu na Manase, ijapokuwa kiongozi huyo alikiri kuamini kwamba kile Herbert Armstrong alikuwa amekiandika juu ya fundisho hili kilikuwa ni ukweli na sahihi.

Ukweli ni kwamba marehemu rais na kiongozi wa kanisa la CG7, bwana A.N. Dugger, alikuwa na matatizo katika uelewa wake wa mafundisho ya kiimani. Kulingana na kiongozi mwingine wa awali wa kanisa la CG7 Rais, Robert Coulter, A.N. Dugger pia alikuwa na matatizo mengine makubwa ya kimwenendo wake katika nyakati hizo, ambayo yamkini Herbert W. Armstrong alikuwa anayafahamu. Yafuatayo ni yale ambayo Herbert Armstrong aliandika kumhusu Bwana A.N. Dugger:

Alilazimika kukiri, kwa maneno yaliyo wazi kabisa, kwamba mafundisho yao kuhusu imani hii yalikuwa ni ya uongo na yenye makosa. Lakini, alieleza, aliogopa kwamba ikiwa wangejaribu kuyasahihisha mafundisho hayo yenye makosa na kukiri kwa waumini juu ya ukweli, wengi ya waumini wao, hususani walio wa umri mkubwa ambao hulipa zaka zaidi, wasingeliweza kuyapokea. Aliogopa wangepoteza imani yao kwa kanisa endapo wangepabaini kwamba kwa miaka yote hiyo kanisa limekuwa likifundisha makosa katika kipengele chochote cha kiimani. Alisema alihofia wengi wangepacha kuchangia pesa zao katika mambo ya kanisa, na pia ingeliweza kuligawa kanisa. Na hivyo yeye alionelea Kanisa lilikuwa halina cha kufanya bali kuendelea kufundisha na kushika fundisho hilo la kiimani ambalo alikiri lilikuwa la kimakosa na la uongo.

Kwa ujumla, hii iliuwa matumaini yangu kwa kiasi kikubwa. Huyu kiongozi wa kanisa, ikiwa si kanisa lenyewe, alikuwa akiwategemea waumini kuwa wao ndio CHANZO cha

mafundisho ya imani, badala ya kumtegemea Mungu! (Toka: Autobiography, ukurasa. 315-316).

Hivyo ilikuwa ni kwa sababu ya maswala ya kimafundisho na kimwenendo ndiyo maana Herbert W. Armstrong alijitenga na kanisa la CG7 na kuanzisha kundi aliloliita Radio Church of God ili liifanye kazi ya Kifiladelfia. Chakushangaza, sababu za maswala yaleyale, miongo kadhaa baadaye, zilisababisha kuanzishwa kwa kanisa la Continuing Church of God, ambalo linahitaji kuendeleza na kuikamilisha kazi ya Mungu (soma Mathayo 24:14).

Mara baada ya kuuelewa muundo sahihi wa kiuongozi wa Mungu, Herbert Armstrong aliandika:

Kanisa linaundwa chini ya serkali ya kimungu, itokayo juu kwenda chini kimuundo (Toka: Mystery of the Ages, uk. 246).

Tangia mwaka 1931...kundi hili dogo la masalia kutoka kanisa la awali la kweli la Kanisa la Mungu lilianza kuchukua uhai mpya kwa kuanzisha enzi mpya za kipindi cha Filadelfia... Enzi hizi za Kanisa zilikuwa zizae matunda... (Toka: Mystery of the Ages, kur. 289-290).

Kisha, pia aliandika:

Baada ya miaka 3 1/2 ya kujisomea kwa makini na kuwa katika mafunzo, Kristo alinibariki ili nihubiri Injili hii ileile ya Ufalme wa Mungu kwa ulimwengu wote kama ushuhuda kwa mataifa yote (Mathayo 24:14). Ubarikio huu ulifanyika kwenye sikukuu ama karibu na sikukuu ya Pentekoste, mwaka 1931 (Toka: Autobiography, uk. 428).

Herbert Armstrong alikuwa amehubiri hata kabla ya hapo, lakini “baada ya muda huu moyo wangu wote ukazama katika jukumu hili” na ndipo akaweza kufanya kampeni yake pana ya kwanza (Autobiography, kur. 426, 430). Mnamo 1933, alikataa kupokea mshahara wowote kutoka kundi la kanisa la Oregon Conference la CG7, na ilipofika October 9, 1933 alianza kuihubiri Injili kupitia radio, jambo aliloamini kuwa ni mlango uliofunguliwa na Mungu na ndio ulikuwa “mwanzo wa kazi hii ya sasa” (Toka: Autobiography, kur. 506, 507, 525, 529, 530).

Alihisi “ijapokuwa hatukuelewa kwa wakati huo, kwamba enzi mpya za Kanisa zilikuwa zimewadia” (Toka: Autobiography, uk. 526).

Baadaye aliandika:

Yesu Kristo aliianzisha enzi ya Filadelfia ya Kanisa la Mungu kupitia kwangu... Agosti 1933 (Toka: What Is a Liberal? The Worldwide News, Feb. 19, 1979).

Herbert Armstrong alibaini kwamba kwa kuwa Mungu alimwahidi Daudi: “16Nyumba yako na ufalme wako utadumu milele mbele zangu, kiti chako cha enzi kitafanywa imara milele” (2 Samueli 7:16); na kwamba: “Daudi kamwe hatakosa mtu wa kukalia kiti cha enzi cha nyumba ya Israeli” (Yeremia 33:17); alitambua kuwa hili limetimizwa kwa sehemu tu katika enzi zote za historia kupitia kile kilichokuja kuitwa ni Ufalme wa Milki ya Uingereza.

Herbert Armstrong akaonelea kwamba taarifa hizi za kuitambua Uingereza na Marekani kama uzao wa Efraimu na Manase, ilikuwa ni sehemu ya “ufunguo wa Daudi”. Kufikia mwaka 1937, kutokana na maandiko yake juu ya Sikukuu Takatifu za kibiblia pamoja na kuitambua Uingereza na Marekani katika unabii, CG7 walimkana Herbert Armstrong—hivyo yaonekana kwamba kati ya mwaka 1933 na 1937, enzi za Kanisa za kipindi cha Filadelfia zilitenganiswa rasmi kutoka kanisa la CG7 (ijapokuwa Herbert Armstrong bado nyakati zingine alikuwa akihubiri kwa mojawapo ya kikundi chao hadi 1942).

## Mlango Uliowazi

Ijapokuwa baadhi ya walio wa imani za Protestant hudhani kwamba “mlango ulio wazi” wa Ufunuo 3:8 unahusika na lango la kuingia kwenye Yerusalemu Mpya (soma Nelson’s Study Bible, uk. 2,170), Herbert Armstrong alitambua kwamba ilihusiana na fursa ya kuihubiri Injili kwa wanadamu. “Mungu ameweka mbele yake [Kanisa la enzi za Filadelfia] mlango uliowazi”.

Imeandikwa katika 2 Wakorintho 2:12 na pia katika Matendo 14:27 jinsi ambavyo Kristo alivyofungua mlango kwa Mtume Paulo kumwezesha aende kwa mataifa mengine na kuihubiri Injili (Toka: Mystery of the Ages, uk. 290). Paulo alitumia msemu wa aina hiyo pia pale alipoandika:

“3Pia tuombeeni na sisi ili Mungu atufungulie mlango wa kunena, ili tupate kuitangaza siri ya Kristo” (Wakolosai 4:3).

Chakuvutia, mara baada ya Yesu kutangaza kwa Wanafiladelfia: “Nayajua matendo yako”, Anaeleza: “Tazama, nimeweka mbele yako mlango uliofunguliwa” (Ufunuo 3:8). Hivyo, Yesu anahusisha Kazi ya Mungu (matendo) ya Kanisa la Wanafiladelfia kwa “mlango ulio wazi”.

Vilevile mlango ulikuwa ufunguliwe kwa Wanafiladelfia ili kuitimiza Mathayo 24:14: “14 Tena Injili hii ya Ufalme itahubiriwa ulimwenguni pote, kuwa ushuhuda kwa mataifa yote. Ndipo ule mwisho utakapokuja”. (Ona: Mystery of the Ages, Kur. 290-291).

## Tabia za Wanafiladelfia ni Zipi?

Kitabu cha Strong’s Exhaustive Concordance kinaonyesha kwamba neno Filadelfia lina maana ya “Upendo wa kindugu” au “Upendano miongoni mwa ndugu”.

Pale Yesu alipotumia msemu “phileo” kwa Simon Petro (imetafsiriwa kama “upendo”), Ni kitu gani ambacho Petro alitarajiwa atende ili adhihirishe aina hii ya upendo?

Petro alitarajiwa awajibike kwa kufanya kazi:

17Kwa mara ya tatu Yesu akamwuliza Petro, “Simoni mwana wa Yohana, unanipenda?” Petro akahuzunika sana kwa kuwa Yesu alimwuliza mara ya tatu, ‘Unanipenda?’ Akamjibu, “Bwana, Wewe unajua yote, unajua ya kuwa ninakupenda.” Yesu akamwambia, “Lisha kondoo Zangu (Yohana 21:17).

Sifa ya Wanafiladelfia ni kwamba wanawapenda ndugu wa kiroho na wako tayari kujitoa muhanga kuwahudumia. Wakati baadhi

wanaweza kudai kwamba hili linahusu kuwahudumia wale tu waliomo katika Kanisa, hilo halitapatana na Mathayo 28:18-19 wala na maneno ya Yesu katika Yohana 10:16:

“16Ninao kondoo wengine ambao si wa zizi hili, inanipasa kuwaleta, nao wataisikia sauti yangu, hivyo patakuwa na kundi moja na mchungaji mmoja”.

Wanafiladelfia wanawapenda wengine, si kwamba wanapendana wao wenyewe pekee.

Sawa na Herbert Armstrong alivyoandika:

... enzi ya Filadelfia ...Enzi hii ya Kanisa ilikuwa izee matunda (Toka: Mystery of the Ages, uk. 290).

Sawa na Yesu alivyofundisha:

“35Kwa maana mtu yeyote anayetaka kuiokoa nafsi ataipoteza, lakini yeye ayapotezaye maisha yake kwa ajili yangu na kwa ajili ya Injili ataiokoa” (Marko 8:35).

Wanafiladelfia watatoa kilakitu ili kuihubiri Injili.

Wanafiladelfia wana: “... nguvu kidogo lakini umelishika neno Langu wala hukulikana Jina langu”(Ufunuo 3:8). Wao siyo sehemu ya Kanisa kubwa na lenye nguvu (siyo kanisa kubwa kwa mtazamo wa kidunia). Lakini wamelishika na kulitunza neno la Mungu bila kulibadiri. Wao hawajayakana madaraka ya Kristo (ambavyo ndivyo “jina”) linafafanuliwa katika kitabu cha Strong’s Exhaustive Concordance.

Wanafiladelfia wenye upendo wanaamini na kufuata kwamba: “Kristo ndiye kichwa cha kanisa” (Waefeso 5:23), na wanakubali juu ya madaraka yaliyo katika Kanisa:

“11Yeye ndiye aliyeweka wengine kuwa mitume, wengine kuwa manabii, wengine kuwa wainjilisti, wengine kuwa wachungaji na wengine kuwa walimu, 12kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu kwa ajili ya kazi za huduma, ili kwamba mwili wa Kristo upate kujengwa. 13mpaka sote tutakapoufikia umoja katika imani na katika kumjua sana Mwana wa Mungu na kuwa watu wazima kwa kufikia kipimo cha ukamilifu wa Kristo. 14Ili tusiwe tena watoto wachanga, tukitupwatupwa huku na huku na kuchukuliwa na kila upepo wa mafundisho kwa hila za watu, kwa ujanja, kwa kufuata njia zao za udanganyifu. 15Badala yake, tukiambiana kweli kwa upendo, katika mambo yote tutakua, hata tumfikie Yeye aliye kichwa, yaani, Kristo. 16Kutoka Kwake, mwili wote huunganishwa na kushikamanishwa pamoja kwa msaada wa kila kiungo, hukua na kujijenga wenyewe katika upendo, wakati kila kiungo kinafanya kazi yake” (Waefeso 4:11-16).

Sawa na Herbert Armstrong alivyoandika:

Serkali ya ufalme wa Mungu kiujumla ni serkali ambayo madaraka yake ni ya kutoka juu kuja chini. Haiwezi kuwa ni ‘serkali itokanayo na maelekezo ya wale wanaoongozwa’... Ufunuo 3:12 inaonyesha kwamba wale walio wa ‘Enzi ya Filadelfia’ watafanyika kuwa nguzo katika makao makuu ya

Kanisa ... Kile ninachowaonyesha hapa ni kwamba Injili ya Kristo ya Ufalme kwa ukweli inahusisha ufahamu huu wote uliofunuliwa hapa –hata ulimwengu wote utatawaliwa na sisi, ambao, pamoja na Mungu Baba na Kristo, tutafanyika ufalme wa Mungu” (Toka: Mystery of the Ages, kur. 49, 347, 362).

Wanafiladelfia pia walipewa onyo: “Shika sana kile ulichonacho, mtu asije akaitwaa taji yako” (Ufunuo 3:11). Herbert Armstrong aliandika kwamba alirejesha kwa Kanisa la Mungu kiasi cha kweli 18 hivi ambazo zilikuwa zimepotea katika enzi zilizotangulia (Toka: Mystery of the Ages, uk. 251). Wanafiladelfia ni wale wanaoshikilia kweli hizo (pamoja pia na kweli zingine zote zilizomo katika Biblia)-ikiwemo mfumo wa uongozi-na wataweza kupewa taji na kutawala!

Yesu alifundisha kwamba Wanafiladelfia walikuwa: “10 umelishika neno la saburi Yangu” (Ufunuo 3:10). Wanaushikilia ukweli kwa dharti, wakati wakiwa wameweka kipaumbele katika kuihubiri Injili, hilo ndilo linawatofautisha kanisa la Wanafiladelfia na makanisa mengine.

### Vipi Kuhusu Wanalaodikia?

Barua kwa Wanalaodikia ndiyo waraka wa mwisho miongoni mwa makanisa saba yaliyotajwa katika kitabu cha Ufunuo:

“14Kwa malaika wa kanisa lililoko Laodikia andika: Haya ndiyo maneno Yake Yeye aliye Amen, shahidi mwaminifu na wa kweli, mtawala wa uumbaji wote wa Mungu. 15Nayajua matendo yako, ya kwamba wewe si baridi wala si moto. Afadhali ungelikuwa baridi au moto. 16 Hivyo kwa kuwa u uvuguvugu, kwamba wewe si baridi wala si moto, nitakutapika utoke kinywani Mwangu. 17Kwa maana unasema, ‘Mimi ni tajiri, nimefanikiwa, wala sihitaji kitu cho chote.’ Hujui ya kwamba wewe ni mnyonge, wa kuhurumiwa, masikini, kipofu, tena uliye uchi. 18Kwa hiyo nakushauri ununue kutoka Kwangu dhahabu iliyosafishwa kwa moto ili upate kuwa tajiri na mavazi meupe ili uyavae, upate kuficha aibu ya uchi wako na mafuta ya kupaka macho yako ili upate kuona. 19Wale niwapendao, ninawakemea na kuwadibisha. Hivyo uwe na bidii ukatubu. 20Tazama, nasimama mlangoni nabisha. Kama mtu ye yote akisikia sauti Yangu na kufungua mlango, nitaingia ndani na kula pamoja naye,naye pamoja nami. 21Yeye ashindaye nitampa haki ya kuketi pamoja Nami kwenye kiti Changu cha enzi, kama vile Mimi nilivyoshinda nikaketi pamoja na Baba Yangu kwenye kiti Chake cha enzi. 22Yeya aliye na sikio na asikie yale ambayo Roho anayaambia makanisa” (Ufunuo 3:14-22).

Tofauti na nyaraka kwa yale makanisa mengine sita, waraka huu umeelekezwa kwa wengi. Hili yaonekana kama inatueleza kwamba kutakuwepo makundi mengi ya Wanalaodikia tofauti na enzi zilizotangulia za Kanisa la Mungu.

Je, hili hatulioni kwa sasa katika karne ya 21? Wengi wamejiuliza katika hali ya kutosadiki ni kwa nini kuwepo na makundi mengi ya Kanisa la Mungu, lakini ni makundi mengi ndiyo kwa dhahiri yalitabiriwa yangekuwepo katika kipindi ambacho enzi za Laodikia

zingeshamiri.

Ikiwa ni ya mwisho, enzi hiyo ndiyo itakayotapakaa katika nyakati za mwisho.

Neno “Laodikia” linaweza kufafanuliwa “watu wanaongoza”, “maamuzi ya watu”, au “watu ndio waamua”. Laodikia inatabia ya kuukataa uongozi uliomwaminifu unaokubalika kwa Wanafiladelfia na inatabia ya kuwa vuguvugu katika ukweli wa neno la Mungu. Laodikia inajijali zaidi (badara ya kuweka kipaumbele katika kuikamilisha kazi ya Mathayo 24:14), hivyo inauacha ukweli-na ndiyo sababu ime “kemewa na kuadibishwa” (Ufunuo 3:18).

Kutoka katika mtazamo wa nje (ni Mungu pekee ndiye auangaliaye moyo kiukweli) yaonekana wengi wa walio nje ya kanisa la Continuing Church of God hawaonekani kuwa na haja ya kweli ya “kuishindania kwa bidii imani ambayo hapo mwanzo ilikabidhiwa kwa watakatifu” (Yuda 3), wakati kuipeleka Injili ndiyo kipaumbele, wakati huohuo pia inahitajika kuishi kwa upendo wa Kifiladelfia, na kuelewa vema unabii. Wengine wanaodai kuyafanya haya, inasikitisha, wanategemea zaidi desturi za wanadamu kuliko neno la Mungu katika kipengele hiki cha mwisho (pamoja na vingine). Kuzielewa nabii nyingi kimakosa kutawasababishia matatizo Wanalaodikia na watawajibika kupitia Dhiki Kuu iwapo wataishi hadi muda huo.

### Ni kwanini kuna Masalia ya Wanafiladelfia katika Karne ya 21?

Kwa vile Laodikia ndiyo hali iliyoshamiri wakati wa mwisho wa zama, basi Filadelfia haiwezi kuwa ndiyo hali iliyoshamiri enzi hizo. Pamoja na hayo, masalia ya Wanafiladelfia sharti yawepo katika enzi hiyo.

Jionee kile kielezwacho katika kitabu cha Waebrania:

1 Upendo wa kindugu na udumu (Waebrania 13:1). 1 Uanafiladelfia na udumu (Waebrania 13:1, kama ilivyo katika tafsiri za neno kwa neno).

Sehemu ya Uanafiladelfia ilikuwa iendeleo luwepo (Idumu) hadi katika karne ya 21.

Vilevile tunatambua kwamba Wanafiladelfia watakuwepo katika karne ya 21kwa kuwa Yesu alilambia kanisa la enzi hizo:

10Kwa kuwa umelishika neno la saburi Yangu nitakulinda hata utoke katika saa ya kujaribiwa inayokuja ulimwenguni pote ili kuwajaribu wote wakao duniani. 11Ninakuja upesi. Shika sana ulicho nacho, ili mtu asije akaichukua taji yako (Ufunuo 3:10-11).

Wanafiladelfia ndio wao pekee ambao wameahidiwa kupewa ulinzi dhidi ya saa ya majaribu ijulikanayo kama Dhiki Kuu pamoja na Siku ya Bwana!

Punde kabla tu ya kuanza kwa Dhiki Kuu (ona: Mathayo 24:15-21), mabaki ya Wanafiladelfia: “12...pewa mabawa mawili ya tai mkubwa, kusudi aweze kuruka mpaka mahali palipotayarishwa

kwa ajili yake huko nyikani, ambako atatunzwa kwa wakati na nyakati na nusu wakati ambako yule joka hawezi” (Ufunuo 12:14). Kwa kufuata kile kilichotokea kwa wana wa Israeli walipokuwa wakija kutoka Misri (Kutoka 19:3-4), ni dhahiri kwamba haya si mabawa ya ndege halisi, bali ni Mungu atawaongoza watu wake watoke kwenye dhiki kupitia mpango atakaouandaa (ona: Kutoka 13:21-22; Danieli 12:1).

Kuhusu kazi ya kifiladelfia, Herbert Armstrong aliandika:

Lakini Kristo alitamka kwa Kanisa lake la enzi ya Filadelfia, kwamba kwa kuwa tunazo nguvu kidogo, angeli IFUNGUA HIYO MILANGO KWA AJILI YETU (Ufunuo 3:8) (Barua, Nov. 19, 1976).

Kazi yetu kupitia mikono ya Kristo BADO INGALI HAIJAMALIZIKA, na hatairuhusu kazi hii isimame hadi pale itakapokuwa imemalizika! Na hilo litakuwa lini? ...hakuna tarehe maalum iwezayo, kwa ujumla kutamkwa. Lakini pale Danieli aandikapo katika aya ya 7, “mambo haya yote yatakapotimizwa”, anaashiria kuhusu swala hili la sura ya 12 lililotajwa hapo mwanzoni—pale Malaika Mkuu Mikaeli atakaposimama (ona aya ya 1, ambalo pia limetajwa katika Ufunuo 12:7) na Shetani atatupwa chini—na DHIKI KUU (Aya ya 1 pamoja na Mathayo 24:21-22, Marko 13:19-20, Luka 21:22) kuanzia mwanzo itachukua miaka 3 1/2 ...Tulikuwa hatujawahi kuvielewa vipindi hivi vya siku 1260, 1290, na 1335. Lakini yaonekana kudhihirika, sasa! Baraka imeahidiwa kwetu—KANISA LA MUNGU—tutakaongojea na kuvumilia hadi zile siku 1335—takribani siku 1335 kabla ya kuja kwa Kristo. Lakini kwa kuwa hakuna awezaye kujua siku wala saa ya kuja kwake, yaonekana hatutaweza kufahamu hasahasa ni lini siku hizi 1335 zitaanza. Lakini yaonekana huo ndio muda ambapo KAZI YETU ITAKWISHA. Huo utakuwa ndio wakati SERKALI MOJA YA ULAYA itatokea –kufufuliwa kwa “Milki Takatifu ya Rumi” ya kale. Hapo ndipo tutakuwa tumeshituliwa na kujiweka tayari, kupelekwa kwenye eneo la usalama ambako tutahifadhiwa mbali na Dhiki Kuu. Siku arobaini na tano baadaye “majeshi ya mnyama” yatazunguka Yerusalemu. Siku therathini baadaye, Dhiki Kuu itaanza rasmi kwa shambulio la kinyukilia katika jiji la London pamoja na nchi ya Uingereza kwa ujumla—na yawezekana kwenye muda huohuo ama punde baadaye kidogo, miji ya Marekani pamoja na ya Kanada nayo pia itashambuliwa. DHIKI KUU, ndipo hapo tutakapoelewa wazi, kwamba huo ndio wakati wa “Taabu ya Yakobo”, iliyotajwa katika Yeremia 30:7. (Kutoka makala ya: Armstrong HW. The Time We Are In, Now. Pastor General’s Report-Vol 1, No. 15, November 20, 1979, uk. 1).

Wanafiladelfia wanahitaji kuendelea kuhubiri ulimwengu hadi mwisho uje, kwani wataendelea kuwepo hadi mwisho ufike. Wanafiladelfia wanapaswa waongoze hatua ya mwisho ya kazi.

## Jinsi ya Kutambua yupi ni Masalia (ama Siye)

Kwa kujaribu kutii maonyo ya Yuda: “Muishindanie kwa bidii imani iliyokabidhiwa kwa watakatifu mara moja” (Yuda 3), mabaki ya kanisa la Wanafiladelfia watakuwa wameshikilia kwa

bidii ukweli uliorejeshwa wakati wa enzi zao. Mabaki ya kanisa la Wanafiladelfia wataelewa na kuifundisha hiyo imani ya awali, na watajibidisha kupita katika kila mlango utakaofunguliwa ili waweze kuihubiri Injili ya Ufalme kwa ushuhuda. Vile vile watahubiri onyo la Ezekieli kwa wazao wa kimwili wa Israeli.

Watahika mfumo wa kibiblia wa uongozi katika Kanisa-mfumo uleule wa serkali utakaotumika wakati wa Ufalme wa Mungu. Kumbuka, hata hivyo: si kwamba mtu fulani tu (ama kanisa fulani) kujiiita “Filadelfia” haihalalishi kwamba wawe kweli ni Wanafiladelfia. Baadhi ambao wanadai kuwa ni Wanafiladelfia siyo.

Kanisa la Continuing Church of God halidai kwamba waumini wake wote ni Wanafiladelfia, bali tunaamini kwamba sisi tu mabaki ya kipekee ya Wanafiladelfia. Je, mtu yeyote ataweza kupata “kundi la kanisa” lililotimilifu ambalo limeshika ukweli kama unavyofundishwa na Biblia pamoja na Herbert Armstrong, ambalo halijaongezea mafundisho “yasiyo ya kibiblia”, lisiloegemea kwenye desturi kama kitu kilicho juu ya Biblia, ama haliwapotoshi waumini wake kwa kuwaondoa kwenye agizo la kutoa kipaumbele kwenye jukumu la kuihubiri Injili lililoagizwa na Yesu Kristo?

Halipo!

Mtu anaweza kutarajia kwamba Wanafiladelfia, ambao wao ndio wanafanya kazi yenye mafanikio, wakitekeleza Mathayo 24:14 pamoja na Mathayo 28:19-20, wakiwa wanashika kwa bidii ukweli, hatimaye wataongozwa na Mungu kuungana na kanisa la Continuing Church of God. Ni ukweli kwamba, kwa kuhudhuria ibada ama kulisaidia kanisa la Continuing Church of God peke yake haimfanyi mtu kuwa Mwanafiladelfia; waumini binafsi nao wanatakiwa watimize sehemu yao, na hawatakiwi waruhusu maisha yao yajawe na kuhangaikia maisha ya ulimwengu huu kiasi cha kuwafanya wapoe (Kilaodikia).

Kutokana na michanganyo pamoja na taarifa potofu zilizojitokeza katika miaka kadhaa iliyopita, tunafarijika kwamba wapo Wanafiladelfia nje ya kanisa la Continuing Church of God. Hata hivyo, hii siyo kisingizio kwa Wakristo waaminifu kuamua kubaki “wamejitenga”. Herbert Armstrong aliandika kwamba “kusudi la kwanza la kuwepo kanisa” ni kuhubiri:

Injili ya Ufalme wa Mungu ujao kwa ulimwengu... Mkristo ‘ajitengaye’, aliye ‘peke yake’ ambaye anataka apande na kuingia kwenye ufalme kwa njia tofauti badala ya njia ya Kristo na njia yake ya kupitia katika Kanisa Lake-atakuwa hapokei mafunzo yaliyo katika aina ya mafunzo ya Kristo, ya kutawala na kuongoza pamoja na Kristo katika ufalme wake!... mtu ajiambiaye, ‘Nitautafuta wokovu mimi peke yangu, pasipo kujiunga na Kanisa, amedanganyika kwa kiwango kikubwa (toka: Mystery of the Ages, uk. 270).

## Kwanini Hili ni Muhimu Kulijua?

Wengine husema kwamba elimu juu ya zama/enzi za Kanisa haina umuhimu, na wanaamini kwamba haiteti tofauti yoyote katika jinsi Wakristo watakavyoishi ama kutenda. Je, huu ni mwelekeo sahihi? Siyo bahati nasibu tu kwamba wengi ambao

wanapuuzia juu ya enzi za Kanisa ndio ambao pia wameachana na kweli muhimu zilizorejeshwa na Herbert Armstrong—na wakati mwingine hawafikirii tena kwamba ni jukumu lao kubwa kutoa kipaumbele katika kuihubiri Injili kamili kama ushuhuda. Hii inasaidia kufafanua mtazamo wao huo-lakini je, wako sawa?

Safari saba (katika Ufunuo 2 & 3) Yesu alionya:

13 Yeye aliye na sikio, na asike kile ambacho Roho anayaambia makanisa (mfano: Ufunuo 3:13).

Ni kwanini Yesu alisema hivyo kwa kurudiarudia ikiwa taarifa hizi hazikuwa na umuhimu wowote? Yesu aliwaahidi Wanafiladelfia zaidi ya kupewa ulinzi wa kimwili tu. Vilevile aliwaambia:

12Yeye ashindaye nitamfanya kuwa nguzo katika hekalu la Mungu wangu, wala hatatoka humo kamwe. Nitaandika juu yake Jina la Mungu wangu na jina la mji wa Mungu wangu, yaani, Yerusalemu mpya, ambao unashuka kutoka mbinguni kwa Mungu wangu. Nami pia nitaandika juu yake Jina langu jipya (Ufunuo 3:12).

Ni nani katika Kanisa la Mungu ambaye hapendi apokee ahadi hizi?

Wale ambao Mungu amewaita wanaweza kuamua endapo wakubali kufundisha ukweli uliorejeshwa kwa Kanisa la Wanafiladelfia ama la. Hilo ni juu yao-lakini gharama zake za kimwili na za kiroho za kutokuukubali na kutoufundisha Ukweli zaonekana kuwa ni kubwa. Sisi tulio wa kanisa la Continuing Church of God: “19...tunalo pia neno la hakika zaidi la unabii, ambalo mtafanya vema mkiliangalia kwa bidii” (2 Peter 1:19; Amos 3:7).

Wanafiladelfia hushikilia kwa bidii mafundisho ya kweli ya kiimani, hawaikani mamlaka ya Kristo, wanalishika neno lake, wanaupenda kwa dhati ukweli, hutumia milango ambayo Kristo anaifungua na kuilinda hadi mwisho. Wanafiladelfia hutii “kile ambacho Roho anayaambia makanisa”.

## UCHEZAJI KAMALI NA DHAMBI



Na Bob Thiel

Kamali ni biashara kubwa. Mamilioni, ikiwa siyo mabilioni ya watu, hucheza kamali.

Je kamali ni mchezo usio na madhara yoyote?

Je, kupiga kamali ni dhambi? Dhambi ni nini?

Je, ni dhambi siku zote kubahatisha?

### Biashara ya Kamali

Biashara ya kamali hujiiita yenyewe kuwa ni biashara ya michezo. Kimsingi, wamiliki wake hupenda wajulikane kwamba wamo katika aina ya biashara ya burudani. Pamoja na kwamba hilo kwa kiasi fulani ni kweli, watu wengi wapigao kamali si kwamba wanafanya michezo peke yake, bali wananuia kujishindia pesa na wakitarajia kutopoteza hela zao.

Na wakati mwingine upigaji kamali ni kucheza mchezo tu.

Maramoja, wakati mimi na mke wangu tulikuwa tukisubiri mlo wetu wa mchana kwenye mgahawa mmoja huko Uholanzi, tulijionea kile ambacho kilionekana kama ni aina ya video ya Kidachi ama aina ya mchezo wauitao “pinball”. Tulifikiri yaweza kuvutia ikiwa tutajaribu kuucheza kwa kuwa haikuonekana kama chochote ambacho tumewahi kukiona katika Marekani. Ilikuwa inagharimu kama senti 25, sawasawa na Dola ya Marekani (\$0.25) kwa kila mchezo.

Ionekanavyo, ni kama tulikuwa tukicheza vizuri na mtu aliyekuwa ameketi kando yetu akatufahamisha kwamba tulikuwa tukishinda na kujipatia pesa. Hili lilitushangaza kwani sisi hatukuwa tumetarajia kwamba huo ulikuwa ni mchezo wa kamali na wala hatukuwa tunauhakika unachezwa namna gani. Mwisho wake tulifikia kuwa washindi wa pesa amabazo ziilingana na gharama ya mlo wetu wa mchana wa bei nafuu kwenye mgahawa huo. Hivyo, ni kweli, kamali yaweza kuwa mchezo usio na madhara na ya kuburudisha.



Lakini kuicheza kila mara si salama.

## Dhambi ni Nini?

Dhambi ni nini? Biblia inafundisha:

4Kila mtu atendaye dhambi afanya uasi, kwa kuwa dhambi ni uasi wa sheria (1 Yohana 3:4).

Ni sheria zipi ambazo hazitakiwi kuvunjwa? Ni Amri Kumi.

Ambazo amri yake ya kumi inahusika na kutokutamani.

17“Usiitamani nyumba ya jirani yako. Usimtamani mke wa jirani yako, wala mtumishi wake wa kiume au wa kike, wala ng’ombe wake au punda wake wala cho chote kile alichu nacho jirani yako” (Kutoka 20:17).

Wengine watadai kwamba katika kamali hawatamani chochote kilicho cha jirani yao. Lakini Yesu aliipanua amri hiyo zaidi, kitu ambacho Mtume Paulo naye pia alikifanya. Jionee:

15Ndipo Yesu akawaambia, “Jihadharini! Jilindeni na aina zote za choyo. Kwa maana maisha ya mtu hayatokani na wingi wa mali alizo nazo” (Luka 12:15).

7Tuseme nini basi? Kwamba sheria ni dhambi? La, hash! Lakini, ni kwa sababu ya sheria nisingekuwa nimejua dhambi. Nisingekuwa nimejua kutamani ni nini kama sheria haikusema, “Usitamani” (Warumi 7:7).

Kutamani inaweza kuwa ni tatizo ambalo wengi hawalitambui:

Ni ya Mwisho — Lakini si Ndogo Kuliko: Na Richard H Wilkinson.

Hivi karibuni, Padre mmoja mashuhuri aliandika kwamba katika miaka yake yote ya kusikiliza waumini walioenda kwake kuungama dhambi, hakuwa amewahi kusikia dhambi ya kutamani ikiwa inaungamwa.

Inashangaza. Je, inaweza kuwa ni kwa sababu, kibinadamu, ni rahisi kutafakari juu ya Amri Kumi kwa kufuata mtiririko wake, tukidhani ya kwanza kutajwa ni bora na muhimu zaidi kuliko ya mwisho, na hivyo kutoichukulia Amri ya Kumi kwa umakini mkubwa sawa na zile tisa zilizoitangulia?

Ya mwisho miongoni mwa Amri Kumi za Mungu, “Usitamani” (Kut. 20:17), ni muhimu na kamalifu na inayotakiwa kutimizwa sawa na zile zingine zote.

Neno la Kiingereza “covet”, ambalo ndilo lilitafasiriwa kwa Kiswahili “Usitamani”, lilitafsiriwa kutokana na maneno saba mbalimbali ambayo yanaainisha aina mbalimbali za kutamani zinavyoweza kuwa. Ebu na tuziangalie maana za maneno haya.

1) Kile ambacho siyo cha kwako: Neno ambalo hutafasiriwa mara kwa mara kuwa “tamani” linamaana ya tama iliyo kinyume, kuhitaji kile ambacho siyo haki yetu. Hili ndilo neno la Kiebrania lililolumiwa katika Kutoka 20:17; aya hii inazungumzia juu ya mali ya jirani zetu.

2) Matumizim mengine ya neno hili yaliyo ya kustaajabisha ni katika Kutoka 34:24, ambapo Mungu anaiahidi Israeli: “24Nitawafukuza mataifa mbele yako na kupanua mipaka ya nchi yako, wala hakuna mtu ye yote atakayeitamani nchi yako wakati unapokwenda mara tatu kila mwaka kuonana na BWANA Mungu wako”. Mungu aliahidi kulinda mali za watu wake dhidi ya jirani zao iwapo Israeli wangemtii na kuzishika Sikukuu zake. Pale Israeli walipoghairi kuzishika Sikukuu za Mungu, Mungu naye hakuwalinda dhidi ya tatizo hili kuu miongoni mwa wanadamu la tamaa (Waamuzi 2:11-23).

3) Kujipatia kwa njia isiyo halali: Neno jingine ambalo, mara kwa mara hutafasiriwa “tamani” linaashiria juu ya kutaka kitu fulani wakati hauko tayari kukilipia. Siyo lazima iwe kwamba kile kinachotamaniwa siyo cha kwetu kihalali, bali ni kwamba tunakitaka isivyo halali. Ezekiel anazungumzia juu ya maafisa wa Israeli ambao walikuwa: “27Maafisa wake walioko ndani yake ni kama mbwa mwitu wararua mawindo yao, wanamwaga damu na kuua watu ili kupata faida ya udhalimu” (Ezek. 22:27). Msemu “faida ya udhalimu” umetafsiriwa kutoka kwenye neno hili la pili.

Kamali, katika miundo yake yote, inaashiria aina hii ya tamaa iletayo faida ya udhalimu, pale mtu atamanipo kupata pasipo kutoa jasho ama kutoa malipo halali.

4) Kuhitaji kwa lengo batili: Neno la tatu la Agano la Kale limaanishalo “kutamani” lina maana ya kuhitaji kitu fulani kwa malengo/kusudi batili ama baya. Ilikuwa ni katika dhana hii ambapo nabii Amosi aliandika: “18Ole wenu ninyi mnaoitamani siku ya BWANA” (Amo. 5:18). Hapa tunaonyeshwa tunaweza kutamani kitu kizuri kwa malengo mabaya.

5) Kuthamini zaidi vilivyo vya kimwili/kidunia: Katika Agano Jipya tunakuta maelekezo aina ingine ya kutamani: kutumainia zaidi na kuthamini mambo ya kimwili. Paulo aliandika: “33Sikutamani fedha wala dhahabu wala nguo ya mtu ye yote” (Matendo 20:33). Katika Mwanzo 25:29-34 tunakuta mtazamo huu ukiwa unaonyeshwa kupitia tamaa ya Esau ya kukitaka chakula cha Yakobo. Waebrania 12:16 inatuonya tusiwe watu wenye tama: “16Angalieni miongoni mwenu asiwepo mwasherati au mtu asiyemcha Mungu kama Esau, ambaye kwa ajili ya mlo mmoja aliuza haki ya uzaliwa wake wa kwanza”. Neno “asiyemcha” hapa linaashiria kutoweka mtazamo wetu zaidi kwenye vitu sahihi na muhimu, hususani mambo ya Mungu.

6) Kutaka zaidi na zaidi/kutokuridhika: Je, umewahi kusikia msemu: “Baadhi ya watu hawaridhiki?” Moja ya maneno yaliyotafsiriwa “tamani” katika Agano Jipya linatokana na mzizi umaanishao “katafuta zaidi”, “kutwaa zaidi”, “kusukumwa na uroho”. Siyo kosa kuweka bidii na jitihada katika kanuni za mafanikio, lakini neno la Mungu linasema wazi kwamba moyo wa kutokuridhika—wa siku zote kutamani zaidi na zaidi—ni aina ingine ya “kutamani”. Paulo alitumia neno kama hili pale alipoandika juu ya: “tamaa mabaya, mawazo mabaya na kutamani, ambayo ndiyo ibada

ya sanamu” (Kol. 3:5).

- 7) Shauku au hamu isiyozuilika: Neno jingine katika Agano Jipya linaashiria hamu kali. Hamu ama shauku siyo kitu kibaya (ona I Timotheo 3:1), bali ni pale tuwapo kwenye hamu ambayo hatuwezi kuidhibiti. Shauku kali kupita uwezo wetu wa kujilinda dhidi ya majaribu ni mbaya (Good News, May 1983).

Kutamani ni kosa na ni dhambi. Upigaji kamali mara nyingi hutokana na msukumo wa kutamani, na hata ikiwa sivyo, hatimaye hupelekea tuzame katika kutamani.

## Kukutana na Wacheza Kamali

Herbert Armstrong alielezea uzoefu wake pale alipokutana na wacheza kamali, akianza na tukio la mama wa mtu mwingine:

Yote ambayo mama huyu aliyokuwa akijali ni michezo ya karata. Alicheza karata na bingo kila usiku mara tano hadi sita kwa juma. Anatomia hata hela ambayo Len pamoja na mimi tulijipatia kwa kufanya kazi ndogondogo baada ya masaa ya shule. Kisha, Leonard alizidi kusema, pale mama huyu kichaa kilipopanda, huwa anatulaani na kututukana kwamba sisi tulikuwa tunamzibia njia, kwamba kama isingekuwa sisi basi angekuwa huru na angekuwa na maisha ya raha. Vijana hawa walifafanua kamali hizo za karata, ambazo mama yao alikuwa amezama. Alikuwa akilipia senti hamsini ama dola kwa kiti kilichowekwa mbele ya meza, na kisha alianza kucheza kamali ya karata hadi aishiwe ama alewe kwa ushindi wa kujipatia pesa, ambazo kesho yake tena angeenda nazo na kujikuta zote ameliwa usiku huo. Unajua hiyo ndiyo siri ya mchezo wa kamali, nitaishia hapa kwa kuwa hili limeshaelezewa.

Sielewi iwapo mnasoma makala iliyoandikwa na mmoja wa wamiliki wakubwa, Ninadhani jumba kubwa zaidi la mchezo wa kamali ni lile la Reno, ni kubwa zaidi katika kamali Marekani yote, au hata ulimwenguni mwote. Na kwa ujumla, upigaji kamali ni halali kisheria huko. Lakini pamoja na hayo, huyu mmiliki wa jumba hilo la kamali alisema, alikuwa akijibu swali, ‘je, huwa tunawaibia ama ni haki tu au ni mchezo usio na kasoro katika jumba letu la kamali?’ Hapana, alijibu, hatutakiwi kupunja. Ni mchezo ulio haki. Na huo ndio ukweli katika majumba haya ya kamali. Hawawajibiki kupunja. Hata kidogo. Mchezo wa kamali umetengenezwa kwa namna fulani. Yaani zile mashine zifanyazo kamali pamoja na mfumo wote kamili. Kwa mfumo wake imeandaliwa ili wenye jumba la kamali waweze kupata kiasi fulani pamoja na faida ili mradi tu wawe wamepata michezo ifikiayo maelfu kadhaa ama maelfu ya dola. Lakini hii ndiyo jinsi kama alivyofafanua. Hawahitaji kupunja wala kuweka kitu chochote kilichofichwa ama cha kiujanja kwa namna yoyote. Wanajikusanyia pesa na wanakuwa mamilionea kwa kuendesha majumba hayo ya kamali pasipo kuingiza ujanjaujanja. Na hii ndiyo sababu, ni swala la asili ya wanadamu.

Mtu anakuja kucheza kamali. Inamwingia kwenye damu hadi anakuwa mlevi wa kamali. Pale aanzapo kushinda japo kidogo, anakuwa anatamani ashinde zaidi na zaidi. Na hapo hawezi kukoma kucheza. Hawezi kuacha wakati anaona kuna fursa;

hawezi kuacha kwa kuwa tayari akili zake zote zimezama katika tamaa hiyo ya kushinda mapesa mengi. Anaishi kwa matarajio kuwa atafikia kushinda zaidi. Anajidanganya, ngoja nicheze tena japo kidogo na baada ya hapo nitaachana na mchezo. Lakini kabla hajafikia hatua hiyo ya kuanza kushinda pesa nyingi, pale ambapo angependa kuacha kucheza, ndipo huanza kupoteza. Ndipo anapofikiria kwamba, ni lazima acheze zaidi ili aweze kurejesha pesa alizopoteza. Lakini mara nyingi na kwa wengi, ndipo huendelea kupoteza zaidi na zaidi. Na wakati mwingine hufanikiwa kushinda japo kiasi kidogo, na hiyo humchochea azidi kucheza akiamini sasa anaelekea kushinda pesa nyingi. Hapo ndipo huanza tena kupoteza pesa, jambo linalomchochea aongeze kucheza ili arudi tena kwenye hali ya kushinda. Lakini hapo anakuwa tayari amebakiwa na pesa kidogo kuliko alizokuja nazo. Hilo nalo linamwongezea nia ya kuzidi kucheza ili arejeshe pesa alizopoteza. Anakuwa amefikia kiwango cha kutoachana na mchezo huo. Hivyo anazidi kuendelea na hali hii inajirudia—mara ashinde kidogo na baada ya hapo apoteze, na kunakuwa na michezo mingi ambapo yeye na wenye jumba la kamali wanapata 50% kwa 50%, yaani, mwanzoni yeye ndiye anashinda na kisha wao ndipo wanashinda. Lakini ukweli ni kwamba wakati anashinda japo kidogo huwa hawezi kuacha akitegemea kujipatia angalau pesa zidi. Lakini anakuwa hajashinda kiwango kikubwa na cha kutosha kumfanya aachane na mchezo. Na pale anapojiona amepoteza hawezi kuacha akijaribu kurejesha na kushinda pesa zaidi. Na hivyo sasa anafanya nini? Anazidi kucheza hadi aishiwe kabisa. Lakini sasa, jumba la kamali huwa haliishiwi. Jumba linazo pesa za kutosha, hawawajibiki kusitisha. Wao wanapesa zaidi ya wateja wao, na wateja wanajikuta wamezidi kucheza kamali hadi wanaishiwa na kuwa bila hela. Sasa, mmoja kati ya aidha mteja ama mwenye jumba la kamali lazima aishiwe kwa sababu wote hawawezi kuacha kucheza. Na siku zote ni mteja ndiye huishiwa na hivyo jumba sikuzote hupata faida.

Na sawa na mtu huyo alivyosema, wenye biashara ya kamali wanayo mabango ya kutangaza biashara yao kila eneo Marekani na majumba yao yanapatikana katika karibia kila senta kubwa. Na makala hii iliandikwa katika moja ya magazeti yetu makubwa. Nadhani ilikuwa miaka kadhaa iliyopita, kama nikumbukavyo. Sasa anaendelea kueleza, chukulia mcheza kamali anashinda kama dola 10,000 ama chochote kwenye mchezo katika jumba lake! Je, wenye biashara hujisikia vibaya kumpa kiasi hicho chote cha pesa? La hapana, wanajisikia furaha kabisa kumpa kiasi hicho. Na si hivyo tu, bali pia wanalitangaza tukio hilo kwenye vyombo vya habari, ili kila mtu ajue kiasi ambacho mtu huyo amejipatia kwani hili linawashawishi watu watamani na waanze kucheza kamali, nao wakitegemea kushinda. Lakini kiujumla, hao wengine wengi wao hawatashinda badala yake watapoteza. Sasa kimsingi, ni mara moja miongoni mwa nyingi ambapo mtu anashinda kiasi kikubwa na kuwa na akili za kuamua kuachana na kamali.

Kwa kusema ukweli, niliwahi kwenda Las Vegas kikazi wakati fulani, na nikajikuta katika jumba hilo kwenda kumuona mtu fulani, ambaye nilikuwa nimearifiwa kwamba alikuwa anataka kuchangia chuo cha Ambassador College. Na tulifikia

katika hoteli fulani, na tukiwa tunaenda kumuona mtu huyo tuliendesha gari na kufika huko jioni ama usiku, ambapo ilikuwa tuonane naye asubuhi yake. Asubuhi yake, yule mtu ambaye alikuwa wakala wetu akiandaa swala hili baina yetu na yule mtoaji, akaja kuniona na akaniambia, unajua kuna jambo ambalo pengine haulifahamu, mtoaji huyu ni mmoja wa wawekezaji katika kasino (majumba ya kamali) zetu hapa, na amesema kwamba walikuja watu wawili ama watatu toka Hollywood ambao walicheza kamali hapa usiku uliopita na walishinda na kuchukua kama dola zaidi ya laki moja. Na waliposhinda tu wakasitisha kucheza. Sasa hili limekuwa ni hasara, hili limeiathiri biashara ya kamali kwenye kasino hii, swala lililomwathiri mmiliki pamoja na uongozi kiasi wanasema hadi alipatwa na maumivu ya kichwa, kiasi kwamba anajisikia hataweza kuchangia chochote leo, na hivyo tukashindwa kuonana naye. Kiujumla sikuwa nimefahamu iwapo alikuwa katika biashara ya kamali kwa sababu mtu huyu alikuwa ni maarufu sana. Alikuwa ni mmoja ya watu wanaoheshimika sana hapa Marekani.

Sasa, ni nini hasa kilichotokea kwa hawa wacheza kamali walioshinda, je, waliachana na kamali mara baada ya kujipatia malaki hayo ya dola? Hiki ndicho kilichotokea. Walipotoka hapo walielekea kwenye jumba jingine la kamali, ambapo walipoteza sehemu kubwa ya pesa waliyokuwa wameshinda. Na kisha wakaelekea kwenye jumba jingine tena la kamali ambako walipoteza pesa yao yote iliyosalia. Hivyo sasa, jumba hili moja la kamali lilipoteza lakini yale mengine yalipata faida, na hiyo ndiyo biashara ya kamali ilivyo. Mnatakiwa mfahamu ndugu zangu kwamba huwezi kuishinda tamaa. Hakuna faida yoyote katika kujaribu. Watu wengi mno katika Marekani wanajaribu kujipatia mafanikio pasipo kufanya kazi. Wanajaribu kujipatia pesa pasipo kuitokea jasho.

Sasa, nimesikia juu ya watu wengi ambao huenda Reno au Las Vegas kucheza kamali. Na husafari kwenda huko angalau mara moja ama mbili kila mwaka. Na huwa wameaanda kiasi fulani cha pesa. Na husema kwao ni burudani na wanaifurahia. Huenda huko na kiwango fulani cha pesa. Wakijua watazipoteza. Lakini wao huona hiyo ndiyo njia yao ya kuzitumia hela zao ili wapate burudani. Na hivyo wanacheza kamali na hiyo huwachukua kati ya siku mbili hadi tatu au hadi nne, huwa wameenda na kiasi kikubwa cha pesa za kuchezea. Mara wanashinda na kutengeneza pesa, kisha tena wanapoteza, baadaye wanashinda tena kabla tena ya kupoteza sehemu kubwa. Lakini hawaachi, huendelea kucheza hadi wanapokuwa wamepoteza pesa zote walizokuwa wametenga na kuja nazo kucheza kamali. Na ndipo inapofikia hali hiyo, huacha na kurejea nyumbani. Kuna watu ambao huenda Las Vegas kila mwaka kwa ajili ya swala hili ambao huishia namna hii. Lakini ni burudani gani ambayo huipata kutoka kwenye hali hiyo ya mchezo huo; sijawahi kuiona.

Mnajua, baadhi ya watu hujipatia hata madawa ya kulevya humo. Huanza kwa kuvuta bangi na kisha huendelea kwa kuvuta unga. Huwa wanafikia hatua ambayo wanatamani sana na hivyo ni lazima wapate zaidi. Ukweli ni kwamba

haifai kiafya. Usijaribu kujidumbukiza kwenye sehemu ambako unajikuta unatamani aina ya vitu hivyo. Sasa mimi sijachanjiwa vitu hivyo. Sijui ni burudani gani wanayoipata kutokana na vitu hivyo, nimewaona wakiwa katika vibanda vya kamali, iliponibidi nipite katika maeneo hayo. Na niwaangaliapo katika hali ya muonekano wao, hawaonekani kuwa na nyuso za furaha. Nyuso zao haziakisi tabasamu, shangwe, furaha na wala hawaonekani kuwa wanaweza kuwatendea watu wengine jambo lolote jema wakiwa katika hali hiyo...

Swala uwezalo kusema tu ni kwamba walienda sehemu hiyo kutafuta burudani, lakini sasa wengi wao wanaishia kuwa na nyuso za muonekano wa woga. Na nimewaona baadhi ambao walikuwa na nyuso za woga mbaya kabla hawajashinda na nimesikia juu ya taarifa nyingi, katika Las Vegas kwa mfano, pamoja na sehemu nyingine kama hiyo, ambako watu huenda huko kucheza kamali, hujikuta wamepoteza pesa yote na kisha watu hao huunda mpango wa kuweka rehani kitu muhimu kinachotegemewa na familia walichonacho, wakitarijia watashinda pesa kubwa na kukirejesha kwa kununua kingine bora na cha kisasa zaidi. Ukweli ni kwamba huwa hawashindi, hupoteza kila walichonacho. Ikitokea wakashinda japo kidogo, hawashtuki na kuachana na kamali muda huo. Pengine wewe unadhani ungesitisha kucheza mara ukijipatia japo kidogo; ukweli ni kwamba usingeacha, wewe pia ni binadamu sawa na wao na wengine wote. Ni wachache sana ambao hupata ujasiri wa kusitisha mchezo mara washindapo. Na wakisitisha mchezo wakati wameongoza na kula pesa kidogo sehemu hiyo, hushawishika baadaye kwenda eneo jingine ambako hupoteza pesa zote. Na hivi ndivyo yule kijana alisema: ikiwa mama yake angefaulu kushinda na kujipatia pesa usiku wa leo, angezipoteza usiku wa kesho yake. Sasa hiyo ni asili ya mwanadamu. Fahamu aina hiyo ya kitu hailipi...

Ebu na turejee kwenye hadithi yetu, ambayo nimeianza ili tujue hasa ni nini kilitokea. Sasa Leonard aliongeza kusema kwamba: Huyu mama aliporejea nyumbani kutoka kwenye kamali, alikuwa amejaa kichaa tupu, alikuwa akitutukana na kutulaani, akisema tulikuwa tunamzibia njia na kama isingelikuwa sisi angekuwa mtu huru na mwenye furaha akifurahia maisha. Vijana hawa walifafanua mchezo wa kamali wa karata. Kwamba ulikuwa aina ya mchezo ambapo alishinda pesa kidogo ambazo kesho yake alipoteza pesa zaidi. Hivyo ndivyo kamali ilivyo. Sasa baba wa vijana hawa walimwelezea kuwa alikuwa ni mtu mwenye malengo sahihi lakini bahati mbaya alikuwa mdhaifu asiye na uwezo wa kufanya lolote juu ya tabia ya mama yao. Hali hii ndiyo imeshamiri siku hizi, ndiyo, sawa na Biblia ilivyosema kuwa hali hii itatapakaa.

Mambo mengi yamo ndani ya Biblia ambayo yanatufundisha mambo sahihi. Tatizo tu wengi wenu husema eti mnashindwa kuelewa Biblia. Na baadhi yenu mmeamini katika vichwa vyenu kwamba eti Biblia haieleweki. Sasa napenda kuwaeleza kwamba Biblia inaeleweka. Na ikiwa mnadhania kuwa haieleweki, basi ni kwa vile tu hamjaanza kuelewa. (Toka: Armstrong HW. Hebrew Series 13 - Juvenile

Delinquency. Radio broadcast, transcript at <http://www.hwallybrary.com/cgi-bin/get/hwacgi?action=getbroadcast&Infold=1333120240&SearchWhat=Keyword&SearchFor=gambling&page=0&return=search#.U2UHa1fStUM>).

Watu walio wengi hupoteza nidhamu pamoja na pesa pale wanapocheza kamali. Aina mbalimbali za kamali kama “Slot machines, paramutual horse racing”, n.k. zimeundwa ili zihakikishe bila makosa, wamiliki wanajipatia faida wakati wachezaji wanapoteza, japo asili ya moyo wa mwanadamu inazidi kuzama katika kudanganyika na kutamani..

## Vipi Kuhusi Kupiga Kura?

Katika Biblia, nyakati zingine kura zilipigwa ili kutafuta kujua Mungu anakusudi gani (Matendo 1:23-26). Hii ni hali ambayo yaonekana Mungu aliiruhusu itumike kabla ya kuja kwa Roho Takatifu kwenye siku ya Pentekoste katika Matendo 2. Pamoja na kuwepo kwa hali hii, haionekani kuwa ni mfumo ambao Wakristo walikuwa wakiutumia mara kwa mara. Mfumo wa kumwenda Mungu katika imani ndio ambao yaonekana umetuwajibisha tusitumainie sana aina hii ya kuutafuta mpango wa Mungu.

## Nani Wapotezao Zaidi katika Kamali? Nani Washindao Zaidi?

Ripoti ya mwaka 2014 ilionyesha ni yupi ambaye alipoteza zaidi katika mchezo wa kamali:

Biashara ya kamali duniani ni kubwa na Marekani ndiyo soko kubwa zaidi la biashara hii, ambako wacheza kamali walipoteza kiwango cha kutisha kifikiacho dolla \$119 bilioni katika mwaka 2013...

Baadhi ya wacheza kamali wanajiamini wana bahati ya aina yake na hivyo wameshinda—hili siyo kweli kwa wacheza kamali waliowengi. Wacheza kamali wasio wazoefu (pamoja na wawekezaji) wanaweza kujikuta wamekuwa wahanga wa hali iitwayo “Dunning-Kruger Effect”—tabia ya wacheza kamali wasiowazoefu kupendelea kudhani wanaweza kuwa bora na wenye bahati, na kushindwa kugundua ugumu wa mchezo huu wawapo katika ucheza kamali. Wanaweza pia hata kubuni mawazo yasiyo sahihi na dhana iwafanyayo waamini kwamba watafaulu na kushinda.

Hivyo hilo ndilo wanalokuwa nalo wacheza kamali wengi wasio na uzoefu, lakini kwa wale ambao ni wa aina ya kamali ya upigaji ramli, wao huwa na shida ya kucheza kutokana na kuwa walevi wa kamali. <http://theweek.com/article/index/255982/how-did-americans-manage-to-lose-119-billion-gambling-last-year>

Makala hii ilionyesha orodha ya hasara za watu waliopoteza zaidi fedha kulingana na taifa, waliopoteza zaidi walikuwa ni Australia. Hapa jionee orodha ya mataifa ambayo watu wao walipoteza zaidi katika kamali:

1. Australia
2. Singapore

3. Finland
4. New Zealand
5. United States
6. Italy
7. Ireland
8. Norway
9. Canada
10. Sweden
11. Britain

Waaustralia walipoteza zaidi ya dola za Marekani \$1000 kwa kila mchezaji katika mwaka 2013, ambapo Waingereza walipoteza kiasi cha dola za Marekani chini ya \$400 kwa kila mchezaji. Ilistaajabisha kuona kwamba mataifa ya Marekani na jamii za Waingereza walikuwa ni miongoni mwa mataifa sita kati ya kumi na moja ya juu zaidi duniani katika wacheza kamali wakubwa ambao walipoteza pesa nyingi.

Kwa kuwa Australia ilitajwa kuwa ndiyo inaongoza katika kamali, nilidhani yafuatayo ambayo yameandikwa katika toleo la Julai-Agosti 1983 la gazeti la zamani la Plain Truth pengine ingewavutia baadhi yenu:

Akitoa maoni juu ya hotuba ya kiongozi wa nchi kuhusu hali ya taifa, mwalimu mmoja wa Kiaustralia, ambaye pia ni mwandishi na mchambuzi, Bill Broderick, alinukuriwa katika gazeti la Time, Septemba 22, 1980, akisema juu ya Australia ya leo kwamba, “Kwao Mungu amekufa. Ni katika michezo tu, kamali na ngono ndiko walikoweka tumaini la wokovu. Hakuna kiwezacho kulitikisa na kuliamba taifa labda tu aina fulani ya janga kubwa litakalolikumba taifa zima”.

Katika Hosea 5:14 Mungu anasema: “14Kwa maana nitakuwa kama simba kwa Efraimu, kama simba....Nitawararua vipande vipande na kuondoka, nitawachukua mbali, HAKUNA WA KUWAOKOA”.

Kuweka tumaini lao katika kamali na siyo katika Mungu si jambo jipya kwa wengi katika Australia, ama wengine wa aina hiyo. Wakristo wanatakiwa kuwa na imani katika Mungu (soma kijitabu chetu: Faith for those God has Called and Chosen).

Jinsi ambavyo mashine za kamali zilivyoundwa kuhakikisha kila mchezo unaenda sawa kwa mmiliki (kamali aina ya “blackjack” yaweza kuwa tofauti, ijapokuwa majumba ya kamali huwa yanafikia hatua ya kuwakataza kushiriki wacheza kamali ya blackjack walio maarufu), kiujumla, casino ndio hushinda zaidi na kutengeneza pesa zaidi katika kamali.

Serkali nazo, kwa namna fulani, wameunda taasisi za bahati na sibu ambazo nazo zimeandaliwa ili wao siyo raia ndio washinde na kujipatia faida. Kushinda katika bahati na sibu ya taifa ni chini zaidi hata kuliko katika majumba ya kamali binafsi. Kwa kuwa mimi huona kwamba bahati nasibu ni namna ya kodi kwa maskini na hufanyakazi kama CHOMBO CHA KUDUMAZA watu wasiboreshe maisha yao, na wala sijashawishika kwamba serkali nyingi zinakuwa na hali nzuri ya kipesa kutokana na hili, zaidi ya hali ambayo wangukuwa nayo kama wasingendesha bahati nasibu. Bahati nasibu za taifa hustawi kutokana na tamaa, ulaghai na kuwaibia watu wao.

Je, ninasema kwamba kila aina ya kubahatisha ni dhambi? Hapana. Wakati mwingine ni kitu kidogo tu cha kujifurahisha. Lakini kwa kuwa inatabia ya kuwafanya watu watamani, kwa walio wengi ni bora kuikwepa mara kwa mara.

Yesu alifundisha wanafunzi wake kwamba walitakiwa waombe:

13 Usitutie majaribuni, bali utuokoe kutoka kwa yule mwovu (Mathayo 6:13).


Na sisi wenyewe pia hatutakiwi tujiingize katika majaribu. Sisi sote tunaubora na udhaifu. Lile liwezalo kumtia mtu fulani katika majaribu, laweza kuwa halina mvuto na matatizo ya aina hiyo kwa mwingine (Ona: Wagalatia 6:1).

Msijidanganye wenyewe (ona: 1 Yohana 1:8) iwapo mnalo tatizo la uchezaji kamali.

7Msidanganyike, Mungu hadhihakiwi. Kwa kuwa kile apandacho mtu ndicho atakachovuna. 8Apandaye kwa mwili, katika mwili wake, atavuna uharibifu, lakini yeye apandaye katika Roho, katika Roho atavuna uzima wa milele (Wagalatia 6:7-8).

Ikiwa upigaji kamali unaweza kukuathiri mapato na hali yako ya kimaisha, ukakufanya uzame na kuwa mlevi, au ukakuongoza katika kutamani, basi unapaswa kuukwepa.

# KOZI YA KUJIFUNZA BIBLIA



## Somo la 4: Jinsi ya Kujifunza Biblia

Bob Thiel, Mhariri Mkuu

Imechapishwa 2014 na Kanisa la Continuing Church of God

---

Utangulizi: Kozi hii kwa kiasi kikubwa inatokana na kozi kwa mawasiliano iliyoanzishwa mwaka 1954 iliyoanza chini ya usimamizi wa marehemu C. Paulo Meredith enzi za Radio Church of God. Maeneo kadhaa yameboreshwa ili yaendane na karne ya 21 (japo sehemu kubwa ya mafundisho ya awali imebaki kama ilivyo). Pia tumeongeza nukuru za Maandiko, taarifa na maswali ambavyo havikuwemo katika kozi ya awali.

---

Kwanini ni wachache sana HUIELEWA Biblia kiukweli?

Kwanini tunakumbana ma kuchanganyikiwa kukubwa—kutokubaliana juu ya nini Biblia inachosema? KWANINI mamia ya makundi ya makanisa na madhehebu mbalimbali yatofautianayo HAYAKUBALIANI juu ya kile kitabu chao kitakatifu KINACHOSEMA? NI KWANINI watu wengi tofauti, walio na uwezo wa kuvielewa vitabu vyovyote vingine wavisomavyo, husema: “Mimi huwa sielewi kabisa BIBLIA”?

Ebu chukua kitabu kinachojulikana cha somo la bayolojia. Ebu waonyeshe kitabu hicho maprofesa wa somo la bayolojia tofauti kumi, kutoka vyuo vikuu tofauti kumi. Waulize kile ambacho kitabu hicho kinaeleza. Wote kwa ujumla watakuja jibu lilelile. WANADAMU HUWA KWA KAWAIDA HAWAPINGANI KUHUSU VITABU VYAO VINAELEZA NINI—ISIPOKUWA TU PALE INAPOKUJA KATIKA KITABU KIMOJA miongoni mwa vitabu VYOTE—Biblia Takatifu! Je, umewahi kuliwazia hilo?

Lakini ebu ichukue Biblia Takatifu kwa wachungaji kumi ama maprofesa kumi tofauti wa vyuo tofauti vya theolojia, na waulize wakuelezee kitabu cha Mungu kinasemaje—na yamkini utapewa majibu kumi tofauti!

Je, haujawahi kujiuliza hili ni KWA NINI? Hapa, kwa dhahiri ndipo palipo na fumbo la karne! Kitabu ambacho ndicho mashuhuri

zaidi, cha kushangaza ndicho kisicholeweka zaidi miongoni mwa vitabu vyote! Mwaka baada ya mwaka, KITABU KINACHOUZIKA ZAIDI duniani—kitabu ambacho kinamilikiwa na watu wengi zaidi kuliko vingine. Kitabu ambacho kimeendelea kuwepo, pamoja na jitihada zote za kutaka kukiangamiza, katika karne mbalimbali – na ndicho kinauzika kuliko vyote vingine! KITABU PEKEEE AMBACHO NDICHO KILITABIRI, karne nyingi kabla, juu ya hali ya machafuko na vurugu za ulimwengu wa sasa-KITABU PEKEE AMBACHO NDICHO KIFAFANUACHO MAANA ya hali hii ya machafuko-inayofunguka mbele ya macho yetu ili tujionee KABLA YA MUDA, ULIMWENGU WA AMANI, WA KUPENDEZA, ambao unakuja KESHO! Kitabu pekee ambacho kilitabiri kabla ya kutukia, kuinuka na kuanguka kwa mataifa maalum na serkali-kinachonyesha HATIMA YA ULIMWENGU!

Hakuna kitabu ambacho kingekuwa kimeandikwa na wanadamu kingeweza kufunua mambo haya! Iwapo ungetaka kuifahamu elimu iliyo muhimu, iliyo ya kimsingi wa maisha yote-ambayo ni MSINGI wenyewe wa elimu yote iliyo sahihi –UNGEENDA WAPI?

## **Kusudi la Biblia**

Sisi tu KITU GANI? Je, tuliwekwa hapa duniani kwa KUSUDI maalum? Na kusudi hilo ni LIPI? KWANINI maisha ya wanadamu ni matupu, yasiyo ya kuridhisha, yasiyo na furaha? Ni kwa njia gani maisha ya wanadamu yatakuwa yenye FURAHA, yaliyojaa msisimko, MAKAMILIFU, yenye mafanikio, yanayojitosheleza? CHANZO cha vita hasa ni nini, na NJIA ya kufikia amani ya dunia ni ipi? NINI hutokea baada ya kifo-NJIA ya kufika kwenye maisha ya furaha, makamilifu, ya MILELE ni ipi? Hakuna kitabu kilichowahi kuandikwa, isipokuwa Biblia Takatifu, KINAFUNUA huu MSINGI wa maarifa yote.

Je, maswali haya ni ya muhimu? Pengine mtu anaweza kujiuliza, je kuna swala muhimu ZAIDI ya hili? Unaweza kuyapata majibu kwa maswali HAYA katika hiki kitabu tu ambacho kimevuviwa na kuwekwa wakfu!—lakini pamoja na hayo, HAKUNA ambaye ameyapata majibu ambayo yameandikwa kwa uwazi kabisa ndani ya KITABU hiki! Ijapokuwa wanadamu wamekipotoa sana, bado kimebadiri maisha ya watu wengi kuliko vitabu vingine vyote vikiwekwa pamoja! Lakini hata hivyo— bado ni KITABU AMBACHO HAKUNA AKIELEWAYE!

Kitabu kisicholeweka kuliko vyote katika historia! Ndicho ambacho maana yake imegeuzwa zaidi, kimefafanuliwa kimakosa zaidi, kimesemwa vibaya zaidi, watu wamedanganya na kuongopa zaidi-juu yake! TATIZO NI NINI?

## **Ni Kwanini Biblia Inaeleweka Kimakosa?**

Hapa tunakupa jibu—na liko wazi sana!

Jibu limejikita katika ukweli kwamba watu HAWAJAWA TAYARI KUTII kanuni za hili neno takatifu la Mungu—na hivyo ulimwengu huu UMEPOTEZA NJIA YAKE. Katika kufanya hivyo, si kwamba umepoteza AMANI peke yake, na FURAHA, na MAFANIKIO, lakini pia umepoteza elimu juu ya LENGU la Biblia—haufahamu Biblia hasa ni nini!

Ebu tafakari! Je, Mwumbaji, mwenye hekima na uwezo mkuu, mwenye busara na upendo wa kuweza kufikiri, kubuni, kuunda, na kutengeneza uumbaji—dunia hii, pamoja na uhai wote ndani yake-je, angewaacha viumbe wake muhimu na wa kipekee katika GIZA na KUTOFAHAMU juu ya KUSUDI lake—LENGU la viumbe hao kuwepo—na juu ya SHERIA zitakazowaletea AMANI, furaha, na SHANGWE na kila jambo jema? BIBLIA NI UFUNUO WA KIMUNGU WA ELIMU YA KIMSINGI IHITAJIKAYO ambayo mwanadamu hana njia nyingine ya kuipata tofauti na hiyo!

Ni wazi kwamba hakuna vyombo ama zana za kisayansi viwezavyo kukuhakikishia iwapo kuna uhai baada ya kifo—viwezavyo kukueleza LENGU la wewe kuwepo—wapi unakoenda—ama NJIA ya kufikia furaha, maisha yaliyokamili, ama jinsi ya kuipata AMANI ya ulimwengu. Wanasayansi wetu, viongozi wetu wa dunia pamoja na wanasiasa wetu wameshindwa KABISA kutupatia majibu haya, ama hata kutuongoza kufikia AMANI yenye furaha, na maisha ya MAFANIKIO ambayo sote tunayatamani!

Mungu Mwenyezi hakuwaficha wanadamu kweli zote hizi. Alizitoa kwa wanadamu. Aliweka HAZINA yake ya kweli muhimu ndani ya MAANDIKO. Alifunua NJIA YA KUFIKIA AMANI na yote ambayo moyo wa mwanadamu unayatamani!

Sasa, KWANINI ni wachache sana ambao ndio huiielewa Biblia? KWANINI makanisa na madhehebu mbalimbali ya Kikristo na yasiyo ya Kikristo yote hutofautiana na kupingana juu ya kile Biblia inachosema?

Tunalikuta jibu katika kitabu cha 2 Timotheo 3:16-17: “Kila Andiko”—siyo zile aya chache pekee ambazo wewe hupenda kuzitumia kulingana na uonavyo, bali—“16Kila andiko, limevuviwa na Mungu”. Maandiko YOTE kumbe yamevuviwa na Mungu—KILA Andiko limevuviwa kwa pumzi ya Mungu—“na linafaida katika”—KITU GANI? “... lafaa kwa mafundisho, kwa kuwaonya watu makosa yao, kuwaongoza na kuwafundisha katika haki; 17Ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila kazi njema”. Maandiko yote yametolewa kwa kuvuviwa na Mungu na YANAMANUFAA KATIKA MAFUNDISHO, KWA KUTUONYA, KWA KUTUSAHIHISHA, KWA KUTUONGOZA KATIKA HAKI, ili mtu wa Mungu awe amekamilika, awe katika uwezo wa kutenda kila jambo jema.

Hivyo faida ya Maandiko ni KUTUONYA na KUTUSAHIHISHA! Lakini ni wangapi wanapenda na wako tayari kuonywa na kurekebishwa na Maandiko! Ni watu wangapi ambao wewe unawafahamu ambao WAKO TAYARI kusahihishwa pale wawapo katika upotofu—KUONYWA kwa mambo batili wayafanyayo!

## **Wanadamu Hawapendi Kusahihishwa**

Watu HAWAPENDI KUONYWA na KUREKEBISHWA! Wanapenda KUSIFIWA—wanapenda kuambiwa UONGO—lakini kuonywa na kurekebishwa kwa hakika WANACHUKIA! Sasa waona ni kwa nini kwa walio wengi ni vigumu kuelewa Biblia, wala kukubaliana nayo juu ya kile inachosema? Biblia ni KIOO kikubwa cha kiroho cha Mungu. KINAONYESHA KILA MAPUNGUFU YALIYOMO KATIKA MAWAZO YETU, huonyesha kila doa katika tabia zetu. Hututoa picha kama TULIVYO KWELIKWELI—kama vile Mungu

anavyotuona, siyo kama tupendavyo KUJIDHANIA kuwa tuko hivyo, wala siyo kama tupendavyo wenzetu watuchukulie kuwa tuko hivyo!

“Maana neno la Mungu” (tunasoma katika Waebrania 4:12), “... li hai tena lina nguvu tena lina makali kuliko upanga uwao wote WENYE MAKALI KUWILI, tena LINACHOMA hata kuzigawanya nafsi na roho, viungo na mafuta yaliyo ndani yake, tena li jepesi kuyatambua mawazo na MAKUSUDI ya moyo”. Ndiyo, huufunua moyo na kuuweka wazi na kufanya FIKRA ZA NDANI YA MTU ZIJULIKANE!

Pale watoto wako wadogo wafanyapo mambo ya makosa— ambayo umewakataza wasiyafanye—je, huwa mara zote wanakili kwa wazi pasipo kuficha? Je, husema: “Baba siwezi kukuambia uongo. Ni kweli hilo nimelifanya?”—ama siku zote HUKANA kadri wawezavyo, wakijaribu kuficha na kutumia visingizio, kutaka KULIHALALISHA kosa, ama kulisukumia kwa wenzao ama kutafuta namna yoyote nyingine ile? Ndiyo, ni kwa sababu hiyo ndiyo asili ya mwanadamu. SISI sote ni watoto wadogo ambao tumekua kimwili tu; na hivyo, pale Baba yetu wa mbinguni aongeapo nasi, kupitia Maandiko yake matakafifu, na anatumemea, anatumemea na anatumemea, mara nyingi hatupendi KUKIRI makosa yetu, mapungufu yetu, njia zetu POTOFU.

Mara nyingi sana, watu WAMEWEKA MAANA TOFAUTI na iliyokusudiwa kwenye Maandiko yanayowakosoa—mara nyingi wameyaruka na KUYAPITA Maandiko mengi ambayo yanawakemea na kuwasahihisha, ama wameyapuza moja kwa moja, na wakajisomea kwa bidii kutafuta Maandiko MENGINE, ambayo yanaweza kuwasaidia kusoma na kuelezea maana ipingayo Maandiko yanayowakosoa, ILIWAHALALISHEMWELEKEO WAO! Na hivyo watu walianza, karne nyingi zilizopita, KUITAFSIRI Biblia! Neno la MUngu limegeuzwageuzwa, limepotoshwa na kupindishwa mno. Lakini hata kabla ya enzi hizi—Yesu alieleza kwamba Wafarisayo pamoja na wengine wasingeweza kuelewa kile ambacho Biblia ilisema katika siku zile—na ndipo wengi wao wakaanza kutafakari na kuyaelewa hayo kwa namna walivyooona wao (soma: Mathayo 15:3-9).

Kila aina ya maana isiyosahihi na ya uongo iliambatanishwa na maneno haya ya Yesu, badala ya kumeza maana ya kweli ya kawaida iliyokusudiwa—maana wazi, rahisi na iliyokuwa IMEKUSUDIWA juu yake! Leo tunayo mamia ya TAFSIRI za kibinadamu za Biblia. Lakini hausikii MAMIA YA TAFSIRI TOFAUTI ZA KITABU CHA BAYOLOJIA KATIKA MAMIA YA VYUO! KWANINI? SABABU VITABU VYA BAYOLOJIA HAVIWAONYI WALA KUWAKOSOA WASOMAJI!

Badala ya kuukiri ukweli, kuzitubu dhambi, na kuzifanya zisafishwe kikweli na damu ya Kristo, badala yake wanadamu hutafuta KUYASAFISHA MATENDO YAO WENYEWE kwa KUYAPINDISHA MANENO MATEULE NA MATAKATIFU YA MUNGU!

SWALA LILIOGUMU ZAIDI duniani kwa mtu wa kawaida kulifanya ni KUKIRI na KUUNGAMA pamoja na kutubu pale anapokuwa amekosea. Hilo LINAONEKANA KUWA GUMU kiasi gani! Jambo la nadra sana hapa duniani ni kumpata mtu ambaye yuko tayari kukiri siku zote kila anapokuwa amekosea, kutubu na kuwa tayari kuigeukia njia aliyokuwa ameiacha. Dunia hii IMEJAA

watu wanaodai WAMEFANYWA upya, kwamba sasa wako tayari kufanya haya. Lakini wayafanyayo kweli ni dhahabu adimu.

Chini ya uongozi wa Mungu, Paulo aliendelea kusema, katika 2 Timotheo 4:1-4, kwamba wakati umewadia ambao walio wengi hawatathamini kikwelikweli MAFUNDISHO YA UKWELI. Watu wamegeuza masikio yao kukataa kusikia UKWELI nao wamezigeukia NGANO pamoja na desturi za wanadamu! Ndiyo, ni ngano, hadithi zilizogeuzwa zionekane na kusimama kama ukweli wa Neno la Mungu! Wengine wanategemea, kinyume na alivyofundisha Yesu katika Mathayo 24:29-31, kwamba atarudi kabla ya kuanza kwa Dhiki Kuu ili aje ‘awanyakue’na kuwaondoa— lakini hilo silo litakalotokea.

Isaya alitabiri kwamba katika siku hizi za mwisho watu watadai: “Msitoe kwetu unabii wa mambo ya kweli; Tuambieni maneno laini, ‘tabirini yadanganyayo’” (Isaya 30:8-11).

## Bado Kuna Sababu Nyingine

Hii ndiyo sababu nyingine ni kwa nini Biblia haieleweki vema. Je, uliwahi kuketi chini na kutafakari kwamba UFAHAMU, TAARIFA unaweza kutolewa kwa fikra za mwanadamu, moja kwa moja, KUPITIA MILANGO MITANO YA UFAHAMU pekee? Njia za asili pekee ambazo mwanadamu anaweza kupokea UFAHAMU WOWOTE, ni pamoja na jicho, sikio, pua, mdomo, pamoja na hisia kwenye ngozi ya mwili wake—hii ndiyo milango mitano ya ufahamu wa mwanadamu. Lakini sasa Biblia hufunua vitu vya KIROHO—na VITU VYA KIROHO KWA KAWAIDA HAVIWEZI kuonekana, wala kusikiwa, kuonjwa kwa ulimi, wala kupapaswa, wala kunuswa kwa pua. Hivyo mtu wa asili hawezi kuelewa mambo ya kiroho ambayo yamefunuliwa kiroho.

Ebu jionee 1 Wakorintho 2:14: “14Mtu wa ASILI” (yaani, mtu aliyezaliwa kibinadamu, mwenye roho ambayo haijaongoka), “... hawezi kupokea mambo yatokayo kwa Roho wa Mungu, kwa kuwa ni upuzi kwake, naye hawezi kuyaelewa kwa sababu hayo yanaeleweka tu kwa jinsi ya rohoni!”—Yanafunuliwa na ROHO YA MUNGU; kwani inaelezwa katika aya ya 10: “10...haya Mungu AMETUFUNULIA kwa njia ya Roho wake”. Na tena unasoma, kwamba ni “ROHO ya Ukweli” ambayo “itawaongoza kuwaweka katika kweli yote” (Yohana 16:13). Kwa kuwa Biblia ni neno la Mungu (inasema wazi kwamba “NENO LAKO NDIYO KWELI”), hivyo linahitaji ROHO TAKATIFU KUUFUNGUA UFAHAMU wa akili na moyo wa mwanadamu kwa ajili ya ufunuo huu wa ajabu wa Mungu. Elewa: ROHO TAKATIFU ikiwa ndani yetu ndiyo UFUNGUO AMBAO PEKEE NDIO UWEZAO KUFUNGUA MILANGO YA KUYAELEWA MAANDIKO.

Hivyo, sawa na Maandiko haya yalivyosema, PALE TUPOKEAPO ROHO TAKATIFU—pale mioyo yetu ianzapo kuongozwa na ROHO, ndipo kwa kupitia hii hatua ya kimungu, ndipo elimu ya kiroho HUFUNULIWA, na moyo wenye uvuvio wa kiroho ndipo HUELEWA!

## TUBU na USADIKI

MASHARTI katika Biblia ya kuipokea Roho Takatifu ya Mungu kimsingi ni MAWILI-TUBU, na USADIKI. Lakini, KUTUBU inamaana

zaidi ya kusunoneka na kusikitika moyoni pekee. Inamaana ya KUJITOA KIKAMILIFU kwa MAKUSUDI ya MUNGU, sawa na KUSUDI hilo lilivyoenezwa katika Neno lake! Inamaanisha kuwa tayari kikamilifu kupokea, na kutekeleza kile ambacho Maandiko yanafundisha, bila ya kujali gharama, kujali mateso, wala kujitoa kunakohitajika, ama jitihada!

Yesu alisema, kama ilivyoandikwa katika Yohana 7:16, 17): “Mafundisho yangu siyo ya kwangu, bali ni YAKE YEYE ALIYENITUMA. Mtu yeyote AKIYAFANYA MAPENZI YAKE, atayajua mafundisho haya”. Ndiyo, hilo ndilo sharti: Ni lazima UJITOE KUYASHIKA MATAKWA YA MUNGU IKIWA UNATAKA UIJUE Biblia.

WENGI wako sawa na mtu ambaye aliwahi kusema: “Mimi nisingeweza kutenda lolote ambalo ninaamini ni kosa kwa ulimwengu!” Moyoni alikuwa amekusudia kweli, lakini BIBLIA inasema: “Iko njia ione kanayo kuwa njema machoni pa mtu, lakini mwisho wake ni njia ya mauti!” (Methali 14:12). Hivyo, kwa kuwa mauti ndiyo adhabu ya DHAMBI, basi zile njia zionekano kuwa NJEMA katika macho ya mtu wa asili ni LAZIMA ZIWE NDIZO NJIA ZA DHAMBI.

LENGO KAMILI LA MUNGU NI KUMWEPUSHA mwanadamu dhidi ya njia hii ya UONGO ambayo huonekana yenye mvuto mkubwa—njia hii ambayo yaonekana kama NJEMA—ambayo hata hivyo mwisho wake ni katika kukata tamaa, mateso, na kifo!

Tunasoma katika Zaburi 111:7-8, 10: “...Maagizo yake YOTE ni makamilifu. Yanasimama MILELE na MILELE na yametengenezwa katika kweli na haki. KUMCHA BWANA NDIO MWANZO WA HEKIMA: UELEWA MZURI WANAO WOTE WALE WAZISHIKAO AMRI ZAKE!”

Tunaweza kuona sasa ni kwa nini watu hawaelewi Biblia. Hawako tayari kujitoa kwa matakwa ya Mwenyezi—wamejaa woga wa kuwaogopa WANADAMU wenzao, badala ya woga wa Mungu. Wanatetemeka wanapowaza kile ambacho WATU wanasema—lakini ni heri sisi sote tungeanza kutetemeka tusikiapo NENO LA MUNGU ALIYE HAI.

UKWELI HUFUNULIWA. Hufunuliwa na ROHO TAKATIFU ya MUNGU—na hilo linahitaji tendo la Mungu KUJIINGIZA ndani yetu. Masharti na vigezo viwe vimetekelezwa—ndivyo TOBA na IMANI.

DAUDI alikuwa na ufahamu. Naye DAUDI alisema: “Neno lako ni taa katika miguu yangu na mwanga katika njia zangu” (Zaburi 119:105).

Kizazi cha leo ni sawa na kile cha siku za Yesu, ambacho alikiambia: “...na hii ndiyo laana, kwamba nuru imekuja ulimwenguni, na watu wakachagua giza badala ya nuru, kwa sababu matendo yao yalikuwa maovu” (Yohana 3:19).

Ndiyo, Biblia ni NURU— ni TAA kwa ajili ya miguu yetu—ni MWANGA katika njia zetu. Lakini sasa kwa hakika badala yake dunia iko katika giza nene.

Sasa basi, utaelewa Biblia kwa njia gani?

Hivi ndivyo waweza kuanza hii safari ya kusisimua, ya kubururudisha roho. Hivi ndivyo uwezavyo kuanza KUIELEWA Biblia vema.

Kwanza, JITOE kwa Mungu, na kwa mamlaka ya Neno Lake. Achana na njia zako—mawazo yako—na njia za jamii ya dunia hii—hii sehemu ya jamii ndiyo huwa ngumu zaidi kwa wengi (Mathayo 10:34-38). Jisomee kuutafuta UKWELI—ili kujionyesha unakubalika kwa Mungu. Muombe Mungu akuongoze—MUOMBE akufunulie maana za kweli. Kisha MWAMINI Mungu—LIAMINI NENO LAKE—Lipokee na ulikubali likiwa katika hali yake ya kawaida, ya asili, na rahisi, sawa na ambavyo ungelipokea uelewa na ukweli wa neno lolote la kitabu chochote kingine ukiaminicho. Kuwa mwangalifu kwa KUTHIBITISHA kila jambo. Chukua tahadhari—epuka kurukia uamuzi fulani, ama kuyachukulia mambo kijuujuu. Na zaidi ya yote—usijaribu kabisa kuifafanua Biblia. Usiruhusu fafanuzi zozote za wanadamu ama kanisa ama dhehbu fulani zijiingize kati ya ufahamu wako. BIBLIA KIUJUMLA HUJIFAFANUA YENYEWWE.

Mungu asingetufanya tuzibe masikio yetu na mioyo yetu ili ISISIKIE kile kinachohubiriwa—hata kama kinatofautiana na kile ambacho uliwahi kuhubiriwa. Pale Mtume Paulo alipofika Beroya, Waberoya walikuta alikuwa akiwahubiri swala TOFAUTI kabisa na waliyokuwa wamewahi kufundishwa na kuamini. Ilikuwa vigumu kujua iwapo Paulo alikuwa ni nabii wa uongo ama ni mtu kutoka kwa Mungu. Tunasoma juu yake katika Matendo 17:11: “11Hawa walikuwa waungwana zaidi kuliko wale wa Thesalonike, maana walilipokea neno kwa moyo mkunjufu” (yaani, BILA MAWAZO MABAYA) na wakayachunguza Maandiko kila siku ili waone ikiwa mambo haya ndivyo yalivyo”. JIFUNZE KWA KUJISOMEA BILA YA MOYO WA MASHAKAMASHAKA—bali wenye TAHADHARI—hadi UMETHIBITISHA kila jambo— Yatafiti MAANDIKO ili ujihakikishie iwapo MAMBO HAYO ndivyo yalivyo.

SOMO HILI LIMEANDALIWA MAALUMU LIKUONYESHE JINSI YA KUJISOMEA BIBLIA YAKO. Limebuniwa ili likupe mbinu na fafanuzi juu ya NAMNA YA KUYAELEWA MASOMO TUTAKAYOYATOA HAPO BAADAYE. Mbinu hizi za kujifunza Biblia ni kama VIFAA katika kazi yako. Utakuwa ukizitumia mara kwa mara. Kwa ajili hiyo somo hili limechapishwa ili kukupa fursa ya MAREJEO ya jinsi ya kujifunza. Fanya marejeo mara kwa mara kwenye somo hili!

Utumie muda ulioutenga kwa ajili ya somo hili ili kuelewa vema maelekezo yake. Itakuwa vema iwapo utanunua Itifaki ya Biblia. Jizoeze namna ya kutumia kifaa hiki cha muhimu, na hakikisha unafanya mapitio kwenye Masomo matatu yaliyopita. Wakati upitiapo hayo Masomo ya awali, yatumie kwenye masomo hayo mawazo yoyote mapya uliyojifunza hapa. Kwa mfano, pengine utapenda kuweka alama kwenye vifungu fulani maalum vya Biblia yako. Kisha, pale somo la kawaida la mara kwa mara litakapotoka, utajikuta umejiandaa vema zaidi kuliko pale mwanzo, kwa ajili ya kozi hii ya kupendeza!

Sasa endelea na kujifunza njia sahihi ya Kujifunza Biblia. Lakini kumbuka, MWELEKEO sahihi—ROHO SAHIHI—KUJISHUSHA kikamilifu kwa kuyatii Maandiko, UWE TAYARI /UKUBALI



## Mahitaji Muhimu kwa Kujifunza Biblia

Mungu aliiandika Biblia. Aliwa-vuvia watu walioiandika (2 Timotheo 3:16). Ni ujumbe wa Mungu kwa mwanadamu!

Maana Ilifichwa Hadi SASA!

Bruce Barton, mwandishi ambaye ni marehemu, ameiita Biblia kuwa ni Kitabu Ambacho Hakuna Akielewaye—na amekuwa sahihi hasa kwa watu walio wa ulimwengu! Huku kushindwa kueleweka ndiyo sababu kuu ya uwepo wa madhehebu na makanisa mengi siku hizi—hayawezi kukubaliana juu ya nini Biblia inafundisha. Iko sababu kwa hili.

Mungu alisema: “28 Amri juu ya amri, amri juu ya amri, kanuni juu ya kanuni, kanuni juu ya kanuni, hapa kidogo, kule kidogo.” 11... KWA MIDOMO MIGENI NA KWA LUGHA NGENI, Mungu ATASEMA na watu hawa” (Isaya 28:10-11).

Mungu ameiandika Biblia kwa kuyasambaza maneno ya somo moja kidogokidogo kila kitabu—maneno ambayo LAZIMA YAWEKWE PAMOJA ili maana iliyokusudiwa iwe bayana. Baadaye, pale uanzapo kuelewa MPANGO wa Mungu, ndipo utakapoelewa ni KWANINI aliiandika Biblia kwa mtindo huo. Hata Kristo, wakati wa siku zake, alihubiri kwa MAFUMBO ILI KUFICHA MAANA iliyokusudiwa (ona Marko 4:11-12 na pia Mathayo 13:11-13).

## SASA Imefunuliwa!

Lakini ilikuwa uwepo muda baadaye ambapo ujumbe wa kweli wa Biblia ungeeleweka kwa wale walio tayari kusahihishwa? Ndiyo! Lini?

Mungu alimwambia Danieli: “kifunge kitabu hadi wakati wa mwisho: (pale) wengi wangekimbua mbio huko na huko [katika kuchambua kurasa za kitabu hiki], na MAARIFA YATAONGEZEKA” (Danieli 12:4). Mlipuko wa elimu wakati wa karne ya 20 na ya 21, uliochangiwa na kuvumbuliwa kwa tovuti (internet) unachangia kutimizwa kwa sehemu ya unabii huu.

KATIKA WAKATI WA MWISHO MAARIFA YA KIBIBLIA YANGEONGEZEKA! Moffatt inatafsiri “wakati wa mwisho” kama “JANGA la hatua ya mwisho”. Ulimwengu wote kwa sasa unakaribia kipindi cha machafuko—kwa sasa tumefikia kipindi cha JANGA la ULIMWENGU la MWISHONI mwa zama! Mungu alisema kwamba katika nyakati za janga hili—SASA—“Mwovu yeyote hataelewa, bali WENYEHEKIMA NDIO WATAKAOLEWA” (Danieli 12:10).

## Kuwa na Mtazamo Sahihi Ili Uelewe

### 1. Unatakiwa Elimu UITUMIE

Ebu na tuliweke jambo moja sawa! Endapo hautaielewa pointi hii, hauna uhakika kwamba utaweza kuelewa kozi hii pamoja

na jitihada zote za KIBINADAMU za kuifanya iwe rahisi kwako. Mungu ameapa kwamba hakuna mwovu yeyote atakayeweza kuelewa Neno lake katika nyakati hizi za majanga, bali kwamba walio werevu ndio watakaolewa (Danieli 12:10).

Kwa kuwa Biblia inafunua kwamba: “Dhambi ni uasi wa sheria” (I Yohana 3:4), wale wanaoenenda kana kwamba sheria yake ilishapita, kulingana na msemo wa Kibiblia, ndio wanaoitwa “waovu”.

Sasa basi, “wenye hekima”, ambao ndio watakaolewa, ni akina nani? Mungu anasema: “10Kumcha BWANA ndiyo chanzo cha HEKIMA, wote wanaozifuata amri zake WANA UELEWA SAHIHI.” (Zaburi 111:10). Hili linahusikaje na kuweza kuelewa kwako kozi hii?

Masomo haya yatafunua kwako mambo mengi ambayo Mungu anakuamuru uyafanye. Iwapo unamwogopa (unamcha) kwa kiasi cha kuweza kuanza kujenga katika maisha yako tabia ya utii kwake (KUZISHIKA Amri zake), amesema, kama tulivyojionea hivi punde, kwamba UTAANZA KUWA MWENYE HEKIMA! KADRI UTII WAKO KWA MUNGU UNAVYOZIDI KUWA MKUBWA, NDIVYO BUSARA ZAKO ZITAKAVYOZIDI KUONGEZEKA – ndivyo matatizo ya kutokuelewa masomo yanayotolewa kwako yatakavyozidi kupungua.

Endapo, kwa upande mwingine, wakati wowote ujao, utaasi juu ya maswala yoyote ambayo Yeye anayataka uyafanye, hekima yako itaondolewa.

Hakuna awezaye kuelewa kwa juhudi zake mwenyewe. Moyo wa kimwili hauwezi kuyaona maswala ya kiroho: “...14Mtu ambaye hana Roho wa Mungu hawezi kupokea mambo yatokayo kwa Roho wa Mungu, kwa kuwa ni upuzi kwake, naye hawezi kuyaelewa kwa sababu hayo YANAELEWEKA TU KWA JINSI YA ROHONI” (1 Wakorintho 2:14). Kristo alisema: “13Roho wa kweli atawaongoza [WATIIFU] awatie katika kweli yote” (Yohana 16:13).

Kweli hizi zinafunuliwa kupitia kwa uvuvio wa Roho Takatifu—na Mungu huwapa ROHO yake kwa wale WANAOMTII na kuzishika amri zake (Matendo 5:32). Uchaguzi uko katika mikono yako. Pamoja na hayo, siyo kumwamini Yesu pekee na kuzishika amri za Mungu ambayo ndiyo Mungu anayotegemea peke yake kutoka kwako.

Yesu pia alifundisha kwamba ni baadhi tu ya wafuasi wake wa kweli ndio watakaokuwa wakifanya kazi ya Kifiladelfia katika nyakati za mwisho, na ndio watakaoweza kuelewa maswala kadhaa ya unabii wa nyakati za mwisho—kwa kuwa watakuwa ‘wameushikilia kwa bidii’ ukweli wa neno la Mungu na kuyatenda mapenzi yake (Ufunuo 3:7-13). Wasio-Wanafiladelfia hawatakuwa wakiishi maisha yao katika uelewa sahihi juu ya maswala mbalimbali (soma: Ufunuo 2:21-29; 3:1-6; 3:14-22).

### 2. Unatakiwa USALI

Yesu aliagiza watu wake wasali kuomba wahesabiwe kuwa wanastahili:

“36Kesheni daima na mwombe ili mweze kuokoka na yale yote yatakayotokea na kusimama mbele ya Mwana wa Adamu” (Luka 21:36).

Mbali na kukesha (kukaa macho –chonjo) na kusali kuomba hilo, kuna nini kingine?

Mwombe Mungu akuongeze Roho yake zaidi – Roho ya UKWELI (Waefeso 5:17-18). Kristo alipokea uwezo wake kutoka kwa Mungu. Alikuwa akisali kwa masaa kumwomba Mungu – wakati mwingine usiku mzima. Hakika tunatakiwa tutumie japo saa moja ama zaidi kila siku tukiwa katika maombi – sisi tu wadhaifu zaidi na tusio na hekima zaidi kuliko alivyokuwa Kristo. TUNAHITAJI MSAADA KWA KIWANGO KIKUBWA! UWAPO KATIKA MAOMBI MWOMBE MUNGU AUFUNGUE UELEWA WAKO WA UKWELI WAKE!

### 3. Unatakiwa UJISOMEE

Hii Kozi ya Jifunze Biblia imeandaliwa ikitegemewa kwamba angalau dakika thelathini kila siku zikitolewa kwa kozi hii zitamwezesha mwanafunzi kulimaliza kila somo angalau ndani ya siku thelathini. Tunaamini kwamba kila mmoja ataweza kutoa muda huo kwa siku kwa somo lililo muhimu kama hili. Upo wakati unakuja, wala hauko mbali, pale wengi wa wanaolisoma somo hili watakapo hukumiwa kupitia Neno la Mungu—Biblia. Ni muhimu tuwe na uelewa wa kile lifundishalo!

Baba anaagiza: “15JIFUNZE UJIONYESHE KWA MUNGU KUWA UMEKUBALIWA na Yeye, mtenda kazi asiye na sababu ya kuona aibu, ukilitumia kwa usahihi neno la kweli” (2 Timotheo 2:15). Tunatakiwa tujandae kwa ajili ya majukumu makubwa katika huduma ya Mungu!

### 4. Unatakiwa Uweke BIDII

Utafahamu, kadri unavyozidi kujifunza masomo haya, kwamba Mungu anatekeleza kusudi maalum hapa duniani. Kila mmoja wetu sharti atumie kila dakika, saa, siku na miaka ya uhai wetu ambayo Mungu ametupatia, tukijiandaa kuendana na kusudi lake hili.

Hatuna umilele wa kulifanya hili, bali Mungu ametupatia wasaa wa kutosha! Sisi, leo, hatuna uhai wa miaka mingi—HATA HIVYO TUNAYO MIAKA YAKUTOSHA JAPO MICHACHE ya kutuwezesha kujiandaa itakiwavyo—na nyakati za awamu ya mwisho ya kipindi hiki, mazingira yatakuwa magumu kutufanya tupate taabu sana kujifunza. Tunaishi katika nyakati za “Majanga ya Hitimisho”. Muda huu, wakati kungali angalau na utulivu kiasi – KABLA DHORUBA HAIJAZIDI – ndio muda wa kujifunza na kujiandaa kwa ajili ya baadaye (ona: Sefania 2:1-3)!

Kwa vile wengi wenu sharti mfanekazi ili kujipatia kipato jambo lichukualo muda wenu mwingi, mnapaswa kuutumia muda wenu unaosalia kwa faida kubwa zaidi. Zaidi ya yote, MSIRUHUSU KUSUMBUKIA MAISHA HAYA KUKAZIBA MUDA MNAOTAKIWA KUJIFUNZA NA KUSALI (Mathayo 13:22).

Mungu analiweka neno lake wazi kwa muda mfupi kwa sasa – punde kabla ya hitimisho—anauweka wazi ujumbe ambao Biblia

IMEULETA. Ebu na tuutumie kwa uangalifu muda huu mfupi! Weka bidii katika kujifunza Biblia! Nenda mbali! Chimba ndani! Mungu anasema: “10Lo lote mkono wako upatalo kufanya, fanya kwa nguvu zako zote, kwa kuwa huko kaburini, unakokwenda, hakuna kufanya kazi wala mipango wala maarifa wala hekima” (Mhubiri 9:10). YALE UYAFANYAYO SASA YAWEZA KUWA KIGEZO KWA MAISHA YAKO YA MILELE (Danieli 12:3)!

## Kile Utakachojifunza

Katika masomo ya KOZI YA KUJIFUNZA BIBLIA Mungu atafanya yafuatayo:

1. Atakufunulia matukio ya kutisha ambayo hivi karibuni yako mbele – na atakuelekeza jinsi uwezavyo kuepuka kuchinjana kwa kutisha ambako mataifa hivi karibuni yatajishababishia yenyewe kutokana na uovu wao.

2. Athibitisha kuwa yuko na atakuonyesha MPANGO wake wote kwa ujumla.

3. Atakupatia yale anayohitaji uyatekeleze IKIWA UNATAKA UWE SEHEMU YA KUUTIMIZA MPANGO WAKE WA MILELE.

## Kozi Iliandikwa Kukusaidia Kukumbuka na Kufanya mapitio

### 1. RAHISI KUKUMBUKA

MPANGILIO SAHIHI wa masomo utaukuta katika kozi nzima. Ukianzia na ufafanuzi wa hali ya ulimwengu kama ilivyo kwa sasa, umuhimu wa Mungu kujiingiza ndilo swala litakalofuatia katika kujifunza. Litakalofuatia haya, ni Ufunuo mtukufu wa ulimwewngu ambao Kristo ataufanya.

Kisha tutaenda nyuma hadi mwanzo kabisa ambapo tutajifunza jinsi Mungu anavyojifunua mwenyewe. Mungu ni nani—ni kitu gani? Ni wachache sana siku hizi wajuao. Ni kusudi gani ambalo ameliiazimia kulitimiza? Vipengele vya masomo vitaendelezwa, katika mpangilio, hadi maeneo yote ya Biblia yakamilike.

Biblia inaeleweka vema pale maswala yake yote yanapokuwa yameeleweka. LAKINI kusudi lake la ujumla haliwezi kueleweka hadi maeneo yote yanayoendana, ambayo yametawanyika hapa na pale, yawe YAMEWEKWA PAMOJA. Kozi hii imekusudiwa ikusaidie kutekeleza swala hilo! Hiki ndicho kiifanyayo kozi hii iwe tofauti na zingine zote. Utakapo maliza kujifunza KOZI YA KUJIFUNZA BIBLIA, Biblia kwako haitakuwa tena, “Kitabu ambacho Hakuna Akielewaye”, bali utatambua kwamba kumbe hata mtoto mdogo anaweza kabisa kuzielewa kanuni zake!

Kueleweka vema kwa Biblia, pale inapofundishwa kwa MTINDO HUU MPYA, kutakuwezesha KUKUMBUKA KATIKA NAFSI YAKO KANUNI KUU AMBAZO MUNGU ANAZIKUSUDIA WATU WAZIELEWE KUTOKANA NAYO!

### 2. VYEPESI KUFANYA MAPITIO

Maneno muhimu ama misemo maalum iliyosambaa kote katika masomo haya imechapishwa katika namna mbili kuu: HERUFI

KUBWA, kama hii, ama Herufi za Italiki, kama hizi. Haya yanasaidia ama kuonyesha KICHWA CHA SOMO cha maneno yafuatayo ama hutumika kutoa MSISITIZO KWA POINTI MUHIMU. Kwa kutumia vichwa hivi vya habari ama maeneo yaliyowekewa msisitizo, unaweza kufanya mapitio kwa urahisi na haraka ili kukumbushia ufahamu wako. Kufanya mapitio inakuwa rahisi kwa namna hii.

Weka machapisho yote pamoja. Weka katika JARIDA, kama KITABU, nawe utatamani kuyapitia mara kwa mara!

## Matumizi ya Muda na Vifaa

### 1. TENGA MUDA

Unatakiwa utenge muda maalum kwa ajili ya kujifunza Biblia yako pamoja na kuabudu. Amua mwenyewe ni muda upi kwa siku ndio unaokufaa. Moyo wako hata hivyo waweza kuwa katika hali ya umakini zaidi nyakati za asubuhi.

### 2. GAWANYA MUDA

Pale alipokuwa angali kijana, marehemu Hebert Armstrong alikuwa ameugawanya muda wake wa kujifunza Biblia katika makundi matatu, akitumia theluthi moja ya muda huo katika maombi kwa Mungu, akitumia theluthi nyingine ya muda ho kwa kujisomea na kujifunza Biblia, na kutumia theluthi iliyobaki kwa kutafakari yale aliyojifunza siku hiyo. Kwa kufuata utaratibu huu, Mungu alizifunua kweli za Biblia kwake. Nyakati zingine alijifunza Biblia akiwa kapiga magoti.

Japo hilo siyo lazima (ama kuwezekana) kwa kila mmoja, inaonyesha jinsi alivyokuwa amepania na kuweka mkazo katika kujifunza Biblia na sote tunatakiwa tuwe hivyo.

### 3. HAPANA MASOMO YA WENGINE

Mosomo ya kidini ya kutoka madhehebu mengine yanapaswa yasisomwe hadi pale utakapokuwa umezama katika kuujua ukweli kupitia kozi hii na kuwa umeipata picha ya kusudi la Biblia ikiwa imejaa ndani ya moyo wako. Hili linahitaji muda. Kozi yetu ya Biblia inalenga kukukamilisha na inaongoza toka andiko moja hadi jingine na kuifanya Biblia ijieleze na kijifafanua yenyewe kadri ujisomeavyo. HAKUNA MASOMO YA WENGINE YANAYOZIDI HAPO! Badala yake yatakuchanganya tu kwa kuichanganya kozi hii na masomo ya madhehebu mengine, hasa wakati unapokuwa ndiyo unanza. Haifai kabisa kwa wanafunzi ambao bado ni wachanga katika Neno la Mungu.

### 4. KUCHAGUA BIBLIA

Tunapendekeza, tumia nakala ya Biblia yako ya Kiswahili na iwapo unafahamu Kiingereza, pia linganisha maandiko na nakala ya kiingereza ya "New King James Version".

Itifaki za Biblia (Concordances) zipatikanazo mwishoni mwa kurasa za baadhi ya Biblia hazina maelezo kamilifu vya kutosha, hivyo usizipe uzito mkubwa katika kuchagua kwako Biblia ya kutumia kwenye kozi hii.

### 5. USOMAJI

Kwanza fanya mapitio ya vichwa vya habari kuu utakazojifunza ambazo zimeandikwa kwa HERUFI KUBWA katika Kozi yako ya Biblia utakayo jifunza. Hii itakupa uelewa juu ya eneo la kiujumla la utakayojifunza na kukuwezesha tangia mwanzo kuwa na picha kamili. Kisha endelea kujifunza kila eneo linalofuata.

Ukishamaliza kujifunza masomo yaliyotolewa, mara nyingi inasaidia kuelewa maana ya aya za Biblia ama sura ZIHUSIKAZO na maeneo uliyojifunza. Usitumie muda wako mwingi wakati huu – wa kuyapitia haya. KWANINI hili linasaidia?

KWASABABU waandishi wengi zaidi ya udhaniavyo wamechezea kurasa nzima za Biblia kwa kuandika kinyume na wametumia hilo kujaribu kuthibitisha tofauti na kile kurasa awali ilikusudiwa kuonyesha.

Ni muhimu sana ulielewe hili. Taratibu utajifunza na kutambua kwamba UMEHADAIKA VIBAYA katika MAMBO MENGI. IRUHUSU BIBLIA IWE KIONGOZI WAKO, siyo wanadamu! VILEVILE, wakati mwingine majarida yaliyopo yaweza kuwa na maana karibu sana na aya inayoongelewa katika kozi ya Biblia kiasi kwamba itakuongezea UELEWA ZAIDI juu ya somo.

### 6. UTIAJI ALAMA

Enzi za Chuo cha Ambassador College, wote wanafunzi na wakufunzi waliweka alama kwenye aya muhimu za Biblia zao. Wengi hata baada ya miaka mingi kupita, wameligundua hili kuwa la MSAADA SANA katika kujikumbushia na kujisomea Biblia.

Wazo la utiaji alama ni KUFANYA MANENO FULANI MUHIMU AYA ZIWEZE KUKUMBUKWA KIURAHISI zaidi ya maeneo ya maneno mengine. Maneno ama sura hizi muhimu, huwezesha kuweza kupaona kwa urahisi na kukufanya ukumbuke upesi wazo na ujumbe unaohusika.

JIFUNZE maneno muhimu ama maelezo yaliyoandikwa kwa herufi kubwa katika Kozi ya Biblia kwa ajili ya kukusaidia kufanya mapitio. Hili litakupatia uelewa wa JINSI YA UTIAJI ALAMA katika Biblia yako. Utajifunza kanuni ya maneno yapi yanastahili kuwekewa msisitizo. Inaweza kukuchukua muda kabla haujawa hodari wa mbinu hii, lakini inafaa kujaribu.

NJIA RAHISI ni kutumia penseli ya kawaida na kuchora mistari juu na/ama chini pembeni mwa maeneo unayohitaji kuyafikia tena baadaye kwa urahisi.

NJIA ITUMIKAYO NA WENGI ni KUPIGA MSTARI KWA KALAMU YA RANGI KWENYE MAENEO MUHIMU.

Utakuja kutambua hapo baadaye kwamba, Biblia yako iliyotiwa alama itakuwa na msaada mkubwa kwako. Unatakiwa UIHIFADHI BIBLIA hii. Iwapo jarida lake litachakaa na kuchanika, waweza kuwekewa jingine kwenye stationery nyingi. Gharama haitakuwa kubwa mno ukizingatia umuhimu wake kwako. Iwapo hata kurasa za Biblia zitaachia, stationery nyingi zinaweza kuzibandika tena kwa gundi.

### 7. TAFAKARI

LENGO LAKO katika kujifunza Kozi hii ya Biblia ni lipi? Ni kujifunza na kukumbuka kweli Mungu azitoazo kwako ambazo zitakusaidia katika kuishi kwako. Lakini la zaidi ya yote, unatakiwa uoanishe kweli hizi zitolewazo na Mungu na uzoefu wako wa maisha ya kila siku katika njia ambayo itakuwezesha KUJIFUNZA KANUNI za njia sahihi ya kuishi.

Iwapo utajifunza kanuni hizi utatambua njia sahihi ya jinsi utakiwavyo kuenenda katika kila mazingira. Hautajisikia kuhitaji kujiulizauliza kila wakati kila jambo ambalo Mungu ameeleza “fanya hili” ama “usifanye hili”. Lakini ni JINSI GANI waweza kujifunza kuzitumia kanuni hizi?

DAUDI, kipenzi cha Mungu, alitupatia JIBU! Alisema: “Heri mtu yule ambaye haendi katika shauri la watu waovu ...2Lakini huifurahia SHERIA YA BWANA, NAYO HUITAFAKARI MCHANA NA USIKU” (Zaburi 1:1-2).

DAUDI alitafakari matukio yaliyotokea siku hiyo. Pia alikumbuka juu ya amri za Mungu – “sheria” Yake. Na wakati wa muda wake aliokuwa huru – wakati wa kila siku, na hasa wakati wa jioni ambapo ndipo alikuwa na mapumziko zaidi – aliyakumbuka yote, na KUYATAFAKARI–akafikia MAAMUZI MAPANA juu ya nini hasa Mungu alikusudia. Maamuzi hayo aliyafanyia kazi! Kwa sababu hii, alifaulu kutembea “siyo katika baraza la wasio na Mungu” kwa kiwango kwamba alifikia kuwa mmoja wa wale waliosimama juu sana katika neema njema ya Mungu. TUNATAKIWA NASI TUFANYE SAWA NA YEYE! Tutawezaje kuenenda kwa njia kama hii?

Watu walio wengi hawawezi kumimina ufahamu katika mioyo yao na kwa wakati huohuo kuweza kutafakari na kuchuja mambo hayo vema. Kama DAUDI, wataweza kuona inasaidia ikiwa WATATUMIA JIONI AMA MAPEMA ASUBUHI KWA KUYATAFAKARI mambo ya Mungu. Pia, ufahamu huteleza haraka na kupotea mara baada ya masaa ishirini na nne baada ya kuwa umejifunza. Baada ya kipindi hicho, kiwango cha kusahau huanza kupungua. Endapo tutaipoteza elimu tuliyojifunza kwa kusahau, hakuna faida yoyote ya kuitafuta. Utakuwa na uhakika gani kwamba utaiweka bila kuisahau elimu uliyojifunza siku hiyo, ili ufikie muda utakaoitafakari na kuelewa vema? Hii ndiyo njia ya namna ya kulifanya hilo!

Ikiwa utasikia ama kujifunza elimu ya kidini siku hiyo, inashauriwa kwamba uifanyie mapitio kwa kuitafakari haraka kadri uwezavyo mara baada ya kuisikia ama kuisoma. ITAFAKARI KATIKA MAWAZO YAKO kama ulivyoisoma ama kuisikia. Tabia hizi zitakusaidia kwa kiwango kikubwa uweze kukumbuka yale ambayo unayahitaji usiyasahau. (Iwapo unaweza kuandika notisi, hilo litakuwa lenye faida kuu endapo utalifanyia mapitio). FANYIA MAZOEZI MBINU HIZI HADI ZIWE TABIA YAKO!

Wakati wa jioni wa kila siku, ama alfajiri ya asubui inayofuata, waweza kuyatafakari maswala ya mambo hayo uliyojifunza karibuni kadri uwezavyo, na kufikia maamuzi ama kanuni. TOA MAJIBU wewe mwenyewe kwa maswali kama, “NINI?” “WAPI?” “LINI?” “NANI?” “VIPI?” na “KWANINI?” haya kiujumla yatakuwezesha kuwa umepitia swala lote ulilojifunza ama kusikia.

HAPOHAPO AMUA NI VIPI KANUNI HIZO ULIZOJIFUNZA KARIBUNI ZITAKUONGOZA KATIKA MATATIZO YAKO YA KILASIKU UNAYOJUA KUWA YATAJITOEZA. Zitumie kanuni hizo mara Kwa mara! Taratibu zitafanyika kawaida kwako kukufanya uishi kwa kuzitenda! MUNGU ANAKUTAKA UJIFUNZE KWA KINA KILASIKU!

## 8. FANYA MAPITIO

Mapitio ni njia ya kurudia tena kile ulichokisoma na itakusaidia sana katika kuiweka kwenye kumbukumbu zako elimu uliyojifunza ili usiisahau—baada ya wiki mbili ama tatu, PITIA YALE ULIYOSOMA. Wakati wa mapitio hayo, unachotakiwa kufanya ni kusoma tu “VIPENGELE VIKUU VYA SOMO”, wakati ukilisoma somo ama hata unapolitafakari hapo baadaye. YAHUSISHE MASOMO YOTE YA WIKI MBILI AMA TATU KATIKA FIKRA ZAKO. Yasome masomo kwa mfuatano wake ili kuelewa vema kinachofundishwa kwa MTIRIRIKO sahihi.

Yawezekana utashangazwa kwa uelewa mpya na bora zaidi utakaoupata kwa kutumia mbinu hii. Itasaidia kwa kiwango kikubwa katika kukuweka kwenye hali ya kujitegemea katika kupata uelewa sahihi wakati ujifunzapo na uisomapo Biblia.

## 9. VITABU VINGINE VITASAIDIA

Waweza kujifunza KOZI YA KUJIFUNZA BIBLIA pasipo msaada wa vitabu vingine vyovyote isipokuwa Biblia pekee, lakini VIPO VINGINE AMBAVYO VINASAIIDIA KUONGEZA KUIFANYA BIBLIA IWE HALISI kwako.

Uelewa mkubwa juu ya mila, jamii na maisha ya kielimu, historia ya watu, pamoja na ufahamu wa jiografia ya nchi, ni msaada mkubwa katika kukupa picha na ufahamu wa matukio yaliyoelezewa katika Biblia. Kutokana na uzoefu wetu, tunajua ni vitabu vipi vitakusaidia zaidi. Baadhi ya vitabu hivi NI MUHIMU ZAIDI kuwa navyo kuliko vingine. (Hata hivyo hatuna mahusiano yoyote na wachapishaji wa vitabu tulivyovipendekeza hapa). Vitabu muhimu zaidi ya vingine ndivyo vimetangulia kutajwa kwanza hapa.

Itifaki ni muhimu zaidi. Kwanini? Sababu ikiwa unajua maneno fulani yaliyomo katika Biblia lakini haujui yamo katika kitabu gani, sura gani ama aya ipi, itakuonyesha ni WAPI YALIPO katika Biblia.

Inasaidia pia katika njia nyingine—na hii NI YA MUHIMU SANA! INASAIIDIA KUKUFUNGULIA MAANA YA MASWALA YA BIBLIA. Inazifunguaje maana za Biblia? Ni katika njia mbili:

(a) Kumbuka kwamba mwanzoni kabisa mwa somo hili katika kipengele: “Jinsi ya Kujifunza Biblia”, tulieleza kwamba Mungu aliandika Biblia akiweka mapengo miongoni mwa maswala yanayofanana ili kuificha maana (Isaya 28:10-11). Maswala yafananayo kwa ujumla huwa na somo moja na mara nyingi yana maneno mengi yanayofanana ambayo yametumika katika maeneo hayo. Kwa kutumia ITIFAKI, ambayo inaorodhesha maneno makuu ya Biblia kwa kuyapanga kialfabeti na kueleza ni wapi ndani ya Biblia ambako yametumiwa, hivyo unaweza kuyakusanya pamoja MASWALA YAFANANAYO na kwa njia hiyo UKAYAZIBA MAPENGO haya, na kuipata MAANA KAMILI NA YA KWELI ya kile ambacho Biblia imekusudia kusema katika kila

swala!

(b) Sasa itambue njia ya pili. Mungu pia ametumia namna nyingine katika kuficha maana ya Maandiko hadi kipindi cha LEO! – nayo ni “Wakati wa Mwisho” (Danieli 12:4). Ametumia ISHARA ama ALAMA! Alama ni kitu kinachosimama badala ya kitu kingine, kinachowakilisha swala, jambo, kitu ama hata taarifa nyingine. Mungu mara nyingi hutumia alama ambazo hazionyeshi moja kwa moja kile zinachokiwakilisha. Anazungumza nasi (kupitia Biblia) kwa “lughha nyingine na kwa ndimi zisizoeleweka [ishara, alama na mafumbo] pamoja na ULIMI MWINGINE” (Isaya 28:10-11) – ulimi utumiao ALAMA zisizojulikana. Ni Yeye pekee ndiye awezaye kukuambia alama hizo zinamaana gani, kwa kuwa ni yeye pekee ndiye ajuaye zinawakilisha nini.

Katika maeneo mengine ya Biblia, Hutumia neno lililile la kialama na KUTOA MAANA YAKE WAZIWAZI hapohapo. Tunajifunza nini? IWAPO HAUELEWI MAANA YA NENO LA KIALAMA, LITAFITI KWENYE ITIFAKI!

Hapa kuna MFANO wazi na rahisi wa nini cha kufanya: “Joka kuu jekundu” la Ufunuo 12:3 ni kitu gani? Kwa kuifungua Itifaki na kulitafuta neno “Joka”, tunakuta neno hilo limetokea katika Sura hii tena kwenye aya ya 9. Tukienda kwenye Biblia, tunasoma katika aya ya 9: “9Lile joka kuu....aitwaye Ibilisi au Shetani”. Tayari siri ya kimafumbo, lugha ya kialama sasa imefafanuliwa! “Joka” la aya ya 3 kumbe ndiye Shetani! (Mara nyingi hata hivyo, neno la alama lisilojulikana huwa haliko karibu na jibu lake kama hivi).

Ziko aina MBILI za ITIFAKI: Itifaki Kubwa na Kamilifu (Mfano Itifaki ya Kiingereza iitwayo “Strong’s Exhaustive Concordance”), ambazo aina hii zinafaa zaidi kwa utafiti; na nyingine ni ndogo, lakini ni Itifaki zenye maneno kamili ambazo ni nyepesi kubeba na rahisi kulipata neno unalolitafuta.

Tahadhari: Siyo kwa kuwa tunapendekeza vitabu fulani, kwamba tunakubaliana na yote wanayosema. Tunachosema ni kwamba umuhimu wa kazi yao unazidi makosa yaliyomo ndani yake. Kiujumla tunawaona kuwa wako sahihi. Ite Itifaki ndogo ya Kiingereza “Cruden’s Complete Concordance” hupendwa na baadhi ya wengi.

KAMUSI YA BIBLIA (DICTIONARY) pia nayo ni muhimu. Kamusi ya Biblia ya Kiingereza, “Peloubet’s Bible Dictionary” hutumiwa sana na wengine. Kamusi ni kitabu kinachofafanua juu ya watu, maeneo, pamoja na vitu vilivyotajwa katika Biblia. Inazo pia chati na majedwali mbalimbali pia na ramani zinazohusu maeneo ya Kibiblia.

Nakala mbalimbali na tafsiri za BIBLIA nazo husaidia. Kwa wasomi wa Kiingereza nakala ya Biblia ya New King James Version (NKJV) ni mashuhuri sana. Enzi za chuo cha Ambassador College walipendelea sana nakala ya Biblia ya MOFFATT version. Namna walivyochagua maneno kwa maswala magumu wakati mwingine ilisaidia kufanya kinachoongelewa kieleweke zaidi kuliko nakala ya King James Version. Nakala za Biblia ziiwazo ENGLISH and AMERICAN REVISED versions nazo pia ni nzuri katika eneo hili, hata na nakala ya NEW INTERNATIONAL VERSION inafaa katika baadhi ya maeneo.

ATLAS ya BIBLIA ni kitabu kilicho na ramani za Biblia. Zinasaidia sana.

## 10. MENGINEYO

Urefu wa Kozi: Miezi kadhaa yaweza kuhitajika. Jiandae vema kwa hilo. Kadri watu wa Mungu watakavyozidi kuwa na njaa na kiu ya neno la Mungu, Kozi hiii nayo itaendelea.

## Mawazo Mawili ya Mwisho

Yapo mambo mawili unayopaswa kuyaweka katika fikra zako.

1. Kumbuka, ijapokuwa makosa kadhaa yasiyo makubwa ya kiuandishi yamejitokeza mara kadhaa, bado BIBLIA HAIKOSEI.

2. BIBLIA INAMAANA SAHIHI. INAMAANISHA KILE IKISEMACHO. Ichukulie kama Neno la Mungu! Inazungumzia maeneo, matukio, pamoja na watu—ukweli halisi—na INAFUNUA elimu ambayo unaihitaji kuijua, ambayo usingeweza kuipata kwa njia nyingine.

## MAMBO UPASWAYO KUJUA

### THAMANI YA KOZI HII YA BIBLIA KWAKO!

Salamu!! – Wanafunzi wenzangu katika Neno la Mungu:

Mtashangazwa kuujua uelewa halisi wa Biblia (Biblia I.Q.) wa Wakristo walio wengi! Hapa tunakujulisha mfano wa kile kilichokuwa kikiendelea katika baadhi ya makanisa, kama ILIVYOELEZWA NA MWANAHABARI ALIYESHITUSHWA:

“Miezi kadhaa iliyopita, mchungaji wa kiprotestanti alitoa jaribio la Biblia kwa waumini wa dhehebu lake. Maswali yenyewe yalikuwa mepesi rahisi sana. Yeyote mwenye uelewa wa kawaida wa Biblia angeweza kuyajibu yote kwa urahisi tu.

“Matokeo ya jaribio yalimfadhaisha mchungaji huyo!

“Ni asilimia 5% pekee ya waumini wake ndio waliopata angalau alama za kueleweka katika jaribio hilo. Asilimia 15% walishindwa kutoa hata jibu moja sahihi. Asilimia 60% hawakuweza kuvitaja vitabu vine vya Injili. Asilimia 75% hawakuweza kupatambua Kalvari kuwa ndipo mahali aliposulubiwa Yesu Kristo.

“Pengine baadhi ya madhehebu yangeweza kufaulu vema zaidi kuliko hao. Lakini siyo mengi. WALIO WENGI MIONGONI MWA Wamarekani leo ni MBUMBUMBU wa BIBLIA! Wanaonekana kuwa hawajakisoma kitabu ambacho wanakiri kukichukulia kuwa ni ‘Neno la Mungu’. Kwanini? . . . Kundi kubwa la watu wengi LIMEITEGEA BIBLIA mgongo kwa sababu, pale wajaribupo kuisoma, wanajikuta HAWAWEZI KUIELEWA . . . Kwa msomaji wa siku hizi, ina ladha ngeni na isiyo na mantiki. Inakuwa inamuacha akiwa na mtazamo kwamba Biblia ni kitabu cha historia ya maswala ya kale ambacho hakina chochote kiendanacho na maisha ya sasa”. (Louis Cassels; Tyler, Texas; Courier-Times, April 16, 1961).

Nukuu hii siyo iliyo pekee na isiyotarajiwa kwingineko! Nukuu za aina hii hufurika kila mara kwenye ofisi zetu za kukusanyia habari, na kujazana katika mafaili yetu. Hali imezidi kuwa hata mbaya zaidi katika karne ya 21. Watu wengi ambao wanalikiri jina la Yesu Kristo HATA HAWAELEWI NI KIPI ALICHOKISEMA! Kwanini?

## Elewa– na USTAAJABU!

SIKILIZA maneno ya Yesu KRISTO! ANATOA JIBU!!

“14Kwao unatimia ule unabii wa Isaya aliposema: “‘Hakika mtasikiliza lakini hamtaelewa, na pia mtatazama lakini hamtaona. 15Kwa maana mioyo ya watu hawa imekuwa mizito, hawasikii kwa masikio yao, na WAMEFUMBA MACHO YAO. Wasije wakaona kwa macho yao, wakasikia kwa masikio yao, wakaelewa kwa mioyo yao, WAKAGEUKA, nami nikawaponya” (Mathayo 13:14-15).

WALIO WENGI WAMETIWA UPOFU JUU YA INJILI YA NJIA YA KWELI YA KUWAWEZESHA KUOKOLEWA! BALI KWENU NINYI – ndiyo, ninyi mnaoisoma hii kozi– KRISTO ANASEMA:

16“...HERI MACHO YENU, KWA SABABU YANAONA na heri masikio yenu kwa sababu yanasikia. 17Amin, nawaambia, manabii wengi na wenye haki walitamani kuona yale mnayoyaona, nao hawakuyaona na kusikia yale mnayosikia lakini hawakuyasikia” (Mathayo 13:16)

KUMEKUWEPO NA UPOFU ULIWAFUNIKA MATAIFA YOTE (Isaya 25:7)! MUNGU KWASASA AMEANZA KUJIONDOA huu UPOFU, LAKINI NI KWA WACHACHE TU WALIOTEULIWA!

Litafakari hili kwa muda! WENGI wa hawa wanaojiita kuwa ni “WAKRISTO” HATA HAWAJAANZA KUOKOLEWA kwa wakati huu kwa kuwa hawaoni wala hawayapokei maneno ya Biblia! Yesu Kristo ndivyo alivyosema!

JE UNAWENZA KUTAMBUA BARAKA ZA KUSTAAJABISHA ambazo Mungu AMEKUPATIA WEWE?

AMEZIWEKA MAHALA WEWE UWEZAPO KUZIFIKIA– katika hali ambayo unaweza kuelewa– elimu iliyo muhimu mno. Unaweza kuipata elimu hii muhimu iliyo ya lazima kwa WOKOVU. Na imefanywa iwe rahisi sana kwako!

Kwani umetambua kwamba kuifuata mbinu iliyofunuliwa na Mungu ya Kozi hii; ya kuambatanisha tena pamoja na kwa usahihi ujumbe na maana iliyokusudiwa ya Biblia yake – KUIREJESHA tena maana yake halisi na muundo wake, NENO JUU YA NENO, KANUNI JUU YA KANUNI, hapa kidogo na huku kidogo (Isaya 28:13), siku zote kuliacha neno la Mungu lijifafanue lenyewe, Roho Takatifu ya Mungu ikituongoza – IMEIFANYA BIBLIA YAKO iwe iliyohai, yakusisimua kwa kiwango kikubwa, iendayo na wakati, KITABU KIONGOZACHO UWEZACHO KUKITUMAINIA AMBACHO WAWAZA KUWEKA MATEGEMEO YAKO YOTE kwakuwa ghafla kila jambo limewekwa WAZI kabisa na kufanywa RAHISI. Umestaajibishwa kukuta kwamba mfumo wetu wa maelekezo hauwezi kufananishwa hata kidogo na kozi zozote zingine!

Umestaajabu kukuta kwamba Biblia yako inashughulika na

maswala ya historia ya kale kwa kiwango kidogo sana kuliko inavyoshughulika na maswala yetu ya leo, ya karne iendayo kasi ya ‘zama za mawasiliano’ ya karne ya ishirini na moja! Kwamba INAKUONGOZA KUELEKEA KATIKA UFAHAMU wa HATUA UTAKIWAZO KUCHUKUA KATIKA NYAKATI HIZI ZA HATARI! Umeanza kukuta kwamba umefanywa uanze kuelewa Biblia yako katika hali ambayo hukuweza hapo kabla!

Tunayo furaka kuu kusema kwamba HAKUNA hata MWANAFUNZI WETU MMOJA aliyeki katika KOZI YA KUJIFUNZA BIBLIA KISHA AKABAKIA MBUMBUMBU wa BIBLIA kwa MUDA MREFU. Wengi hata miongoni mwa Wachungaji hukuta – kwa mara ya kwanza–UKWELI wa Biblia unaanza kueleweka kwao!

## Maneno ya Mchungaji Fulani

HAPA TUNAKULETEA kile ambacho MCHUNGAJI FULANI alikiandika kwa RADIO CHURCH OF GOD (Mwanzilishi wa kozi hii) – BAADA YA MASOMO MANNE TU!

“Napenda kutoa shukrani zangu na kuwafahamisha jinsi ninavyoburudika kuisoma Kozi ya Biblia kwa Mawasiliano (Bible Correspondence Course). Ninatarajia kufanya jaribio langu la kwanza ndni ya siku chache hivi. Ninajiona kama mwanafunzi wa darasa la kwanza ambaye ndipo kamaliza kujifunza kwamba ‘LMNOP’ siyo neno bali ni herufi tano tofauti za alfabeti.

“NIMEKUWA MHUBIRI KATIKA DHEHEBU MOJAWAPO KUBWA Kwa takribani miaka miwili sasa. Katika muda huu wote nilifikiri nilikuwa ninamfanyia Mungu kazi. NIMESHANGAZWA NA NIMEHUZUNISHWA KUONA NI KWELI NYINGI KIASI GANI ZA MUNGU KWANGU ZILIKUWA SAWA NA ‘LMNOP’ nilipozisoma kupitia mtazamo wa kidhehebu. NAMUOMBA MUNGU AWAONEE HURUMA WALE NAFSI MASIKINI WOTE NILIOWAPOTOSHA KWA KUWAHUBIRI KIMAKOSA”.

BIBLIA KULINGANA NA INAVYOHUBIRIWA NA MAKANISA YA KIULIMWENGU, INAKUWA KAMA ISIYO NA MAANA YOYOTE BALI NI NYARAKA KADHAA TU ZA KIALFABETI!!

Ikiwa hata wachungaji waliosoma toleo la awali la KOZI ya Biblia HII wameshtushwa na elimu inayotoa, ebu tafakari kile inachoweza kukufanyia wewe. ITAMAANISHA UZIMA WAKO WA MILELE! UAMUZI NI WAKO!!

## MUNGU HUUANGALIA MOYO!

Mungu amekupatia FURSA ADIMU na ya THAMANI! Anakutarajia uthamini. FANYA kujisomea Biblia – MANENO YA BIBLIA YAKO – iwe ni sehemu halisi ya MAISHA YAKO, iwe ni sehemu yako. Iwe ni sehemu YAKO sawa na mkono wako wa kuume, ama sawa na moyo wako upigao daima.

Ikiwa tayari unafanya hivyo, basi tayari unajua ni Baraka kuu kiasi gani umejipatia. Liwazo, hekima, na busara, pamoja na utulivu mkuu wa moyo, uko katika njia sahihi kuendea uzima wa milele. Kwa sasa tayari UNAFHAMU NI KWA JINSI GANI KOZI YA KUJIFUNZA BIBLIA INATHAMANI KWAKO!

Ikiwa wewe ni yule ambaye bado hajaenda mbali sana katika zoezi hili, FAIDA KUU NA YA KUSTAAJABNISHA INAKUNGOJEA. Wewe pia utajifunza kwamba muda ulioutumia katika kujifunza Biblia yako, kupitia msaada na maelekezo ya Kozi hii ya Biblia, utakuwa ni wa kuburudisha mno, uliojaa uelewa na wenye faida kuliko wote uliowahi. Muda utakuwa ukipaa tu! Nawe utatambua kwamba hatimaye umefika katika njia sahihi ya kukufikisha kwenye wokovu wenye furaha!

SIKU HIZI tunaishi katika NYAKATI ZA MWISHO ZA ZAMA HIZI – nyakati za kuelekea kwenye MAANGAMIZI ya USTAARABU wa mwanadamu! Unatakiwa utambue ni katika kipindi kipi unachoishi – ndiyo, WEWE–uko katika TISHIO la KUANGAMIA!

Kusema kweli tunaishi katika nyakati ambazo Paulo alizitungumzia pale aliposema: "...Lakini yakupasa ufahamu jambo hili, kwamba siku za mwisho kutakuwa na nyakati za hatari" (2 Timotheo 3:1).

Wakati huo ndio SASA!

Kwa kweli unashuhudia wakati huo wa hitimisho ambao nabii nyingi ziliuzungumzia– wakati ule wa watu wasioamini Mungu, wasio wacha Mungu, wakaidi, waishio katika tishio la maangamizi ya nyuklia – ule wakati ulio wa zama za mwisho wa kizazi hiki, na kukaribia kwa ule Ulimwengu wa Kesho (Ujao) ulio wenye utukufu mkuu!

UNAHITAJI KWA KIASI KIKUBWA KUJUA NI VIPI unaweza KUJIEPUSHA na dhahama ya wakati huu itishiayo ulimwengu mzima – kujua ni jinsi gani utakavyoishi hadi kuingia katika ulimwengu wakupendeza wa Ufalme ujao!

**HII NDIYO SABABU UNAIHITAJI KOZI HII KWA KIWANGO KIKUBWA!**

HAKUNA MAHALA PENGINE uwezapo kuipata taarifa hii ikiwa rahisi, wazi, yenye maelekezo ya hatua kwa hatua unayohitaji mno ikusaidie uweze kupenya salama! Hakuna pengine ambako ELIMU YA THAMANI iwezayo kuokoa maisha yaweza kupatikana!

NI HAPA PEKEE katika HII KOZI ya Biblia ndipo utakakopata, taarifa wazi, zisizopindapinda ambazo ni za lazima uwe nazo! Ni za muhimu katika maisha yako!

Mungu kasema iko njia moja pekee–mbinu moja peke yake ya kujiponya! Naye anakupatia njia hiyo wewe bure—iwapo unaihitaji!

**KWA NAMNA YOYOTE ILE HAKIKISHA UNAENDELEA NA KOZI HII!**

Kufikia sasa, masomo 4 yalichapishwa katika gazeti hili. Katika toleo lijalo la Gazeti la Habari za Unabii wa Biblia, badala ya somo, UTAPOKEA JARIBIO JEPESI linalohusika na masomo ambayo umejifunza katika matoleo manne yaliyotangulia.

**MAJARIBIO ni RAHISI!**

JARIBIO litakuwa ni RAHISI tu, la maswali – yakukuwezesha kufanya mapito ya kukusaidia kuelewa na kuiweka pamoja elimu uliyoipokea na kuiweka katika matumizi. Kwetu sisi utakapolifanya jaribio hili itatuonyesha nia yako ya dhati ya kuhitaji kuendelea

kuipokea elimu hii ya thamani ya Biblia.

WANAFUNZI WENGI WA KOZI KWA MAWASILIANO HUPATA 100% KATIKA JARIBIO LAO! ZAMANI KARIBU 9 MIONGONI MWA WANAFUNZI 10 WALIPATA 'A' KATIKA MIAKA YA 90!! HII NI IDADI KUBWA SANA YA WATU! Uzoefu wetu unaonyesha kwamba ni wachache tu ndio hufeli!! KIWANGO CHA KUFELI CHA ALAMA 69 NI CHA CHINI SANA KULIKO ALAMA AMBAZO WENGI HUPATA. Hii inakuonyesha wazi kwamba haitakuwa vigumu kwako wewe kufaulu jaribio hili utakalolipokea.

**MUHIMU!**

Yaweke kwenye JARIDA haya MAELEZO Muhimu ya Jinsi ya kujifunza yatanguliayo SOMO LA 4. YAFANYIE MAPITIO mara kwa mara. Yana hazina ya maelekezo unayotakiwa kukumbuka.

# SIKU ILIYO KIPENZI KWANGU



**Yohana Hickey Akizungumza kwenye Sikukuu ya Vibanda**

## Na Yohana Hickey

Sikuzote kwa namna fulani nimekuwa nikifahamu kwamba Siku ya Saba ni Sabato. Sielewi ni jinsi gani lakini ninafikiri pengine nililisoma hilo katika habari ya uumbaji ama katika Amri Kumi. Sawa na wengine wengi, pale nilipoenda kanisani nilienda kwenye siku ya Jumapili hivyo nikachukulia kwa kujiambia mwenyewe kwamba kalenda pamoja na dhehebu la Waandiventista wa Sabato (S.D.A.) walikuwa wamepotoka. Jumatatu inatakiwa ndiyo iwe siku ya kwanza ya juma na Jumapili ndiyo ya saba. Ninamaanisha, kila mmoja huenda kanisani siku ya Jumapili, ama sivyo???

Nilikuja kulipata jibu kwa swali hili pale nilipoangalia kipindi cha kwenye TV ambacho nilidhania kilikuwa cha kisayansi, lakini kumbe makala hiyo ilikuwa ni ya kikanisa, ikitolewa na Church of God, tena iliyokuwa na mambo zaidi na niliyodhania. Iliyabidiri maisha yangu. Niliwapigia na kukiagiza kijitabu walichokitoa kuhusu makala hiyo na pale kilipowasili nilizama katika kukisoma – Ninamaanisha, sikukiweka chini kwani kilikuwa cha kusisimua mno.

Unajua, jambo la kwanza kabisa ambalo Mungu alilifanya mara baada tu ya kutuumba ilikuwa ni kuiumba Sabato kwa ajili yetu, kwa kupumzika na kwa kuitakasa siku hiyo ya saba. Hii ilikuwa ni mapema hata kabla ya gharika, mapema hata kabla ya Ibrahimu na Musa, mapema hata kabla sheria haijatolewa Mlimani Sinai. Haikuwa sehemu ya amri na maelekezo yaliyotolewa ili kuiweka Israeli ienende kwa utaratibu. Na haijawahi kubadirika.

Amri hii ya nne inaanza kwa kutamka: “Ikumbuke siku ya Sabato, uitakase”. Kumbuka. Kwa kuanza na neno hilo Mungu kwa hakika alijua kwamba tungelisahau. Kisha anafuatia hilo kwa kufafanua namna tunavyotakiwa kuikumbuka. Kusema kweli, ilichukuliwa kwa umuhimu mkubwa katika wakati huo na Mungu kiasi kwamba alisema kila mtu ambaye ataihalifu atatakiwa auawe, na kwamba tunatakiwa tuishike katika vizazi vyetu vyote kama agano la milele.

Sabato ni ishara kutoka kwa Mungu kwa watu wake inayotuwezesha kujua kwamba yeye ndiye BWANA atutakasaye. Vilevile ni ishara kutoka kwetu kumwonyesha Mungu aweze kuwajua watu wake walio waaminifu, walio Waisraeli ama walio

wa Mataifa. Tatizo ni kwamba makuhani wa Kiebrania waliingiza taratibu na masharti mengi yakuiongoza Sabato na jinsi ya kuishika, kuhusu kile watu wawezacho ama wasichoweza kufanya siku ya Sabato, kiasi kwamba wakaifanya iwe ni mzigo kwa watu, ambao kinyume chake walitakiwa wafurahie kwa kuwa katika pumziko lililoletwa na siku hiyo.

Kulingana na mawazo ya hawa Rabbi, tendo la kuchuma masuke ya ngano na kuyasugua kwenye mikono ili nafaka zitoke iliyoelezwa katika Luka Sura ya 6 Aya ya 1, ilikuwa kuivunja Sabato katika njia 2, kwani kuchuma masuke ilikuwa ni kuvuna na kuyasugua ilikuwa ni kupula. Mtazamo wa Yesu katika Marko 2:27 ambako alisema: “Sabato ilifanyika kwa ajili ya mwanadamu, si mwanadamu kwa ajili ya Sabato”, ilikuwa ni njia ya kuinusuru Sabato kutoka kwenye mizigo hiyo ya mila na desturi ilikokuwa imefikishwa, ambako ilikuwa imefanywa kuwa yenyewe ndiyo hatima badala ya kuwa ni ya kutupeleka kwenye hatima.

Isaya anatupatia mfano wa namna tunavyopaswa kutenda katika siku ya Sabato kwenye Sura ya 58, aya ya 13 & 14 ambako anatuambia kwamba, tunatakiwa kuichukulia kuwa ni furaha na ni utukufu. Kwamba kwenye siku hii hatupaswi kuitafuta anasa yetu ama mambo yetu wenyewe. Kwamba tunatakiwa tujifurahishe katika BWANA kwenye siku hiyo naye atatubariki kwa kiasi kikubwa.

Tunaelewa kwamba tunahitaji kukutana pamoja mara kwa mara ili tuweze kutiana moyo na kubadirishana mawazo na wengine walio watu wa Mungu. Kwamba pasipo huku kutiana mioyo, kudumu katika imani yetu yaweza kuwa vigumu sana.

Yesu alituachia mfano kwa kuungana na wengine walio watu wa Mungu ili kumwabudu Mungu kila siku ya Sabato, sawa na walivyofanya pia Mitume 12 baada ya hapo. Paulo kwa mfano alienda kwenye sinagogi kila siku ya Sabato pale alipoweza. Kwanza ili kukutana na Wayahudi huko, na kisha, baada ya kuwa wamemkataa, alienda kukutana na watu wa Mataifa, nao pia kwenye siku ya Sabato, kwani wao ndio waliokuwa na mioyo iliyo na usikivu kwa ujumbe wake. Ijapokuwa Paulo aliyarahisisha baadhi ya mambo kwa waongofu wa Mataifa, Biblia haionyeshi popote kuwa aliachana na kumwabudu Mungu siku hiyo na kufundisha juu ya Sabato.

Tunafahamu kwamba tunatakiwa kujitahidi kuachana na dhambi. Tunaelewa kwamba dhambi ni uasi wa sheria. Amri ya nne inaamuru tuitunze Sabato idumu kubaki takatifu na hii ndiyo sababu kwanini tunaishika na kuitii leo.

Juma la uumbaji pamoja na majuma ya siku sabasaba tuliyonayo leo ni kielelezo cha utukufu utakaokuja. Pale tuichukuliapo siku kuwa ni sawa na miaka elfu moja kama Petro alivyoainisha, baada ya miaka elfu sitaya utawala wa mwanadamu juu ya dunia hii, tunatarajia utawala wa miaka elfu moja ya Ufalme wa Mungu.

Katika jamii yetu hii ya maisha ya kasi, wazo la kutumia siku nzima ya masaa 24 kama muda mtakatifu yaweza kuonekana isiyostahili, ama isiyowezekana. Watu waliowengi hudhani kwamba iwapo wataenda kanisani tayari watakuwa wametimiza jukumu lao na hivyo wanaweza kuendelea na maisha yao. Kusema kweli, kama mchungaji wa awali wa dhehebu la kawaida, nilikuwa



na mazoea ya kuwahubiri kwa nguvu na kwa mda mrefu watu ambao walikuja kanisani kwa kugesha boti zao – mwendo mfupi kuelekea ufukweni. Ninaamini hili limepotea kwa watu wengi wa ulimwengu huu. Wanaishi maisha ya kasi wakijali kazi zao na hata pale wanapokuwa hawafanyi kazi bado wanakimbizana na maisha. Kusitisha maswala yao kwa masaa 24, mara moja kwa juma ni baraka kubwa.

Baada ya kuwa nimemaliza kukisoma kile kijitabu nilichotumiwa na kanisa la Church of God, nilimpigia mchungaji wa lile kanisa la Kiutamusho ambako ndiko nilikuwa nikienda kusakli nyakati hizo, na nikamwuliza ni kwanini tulikuwa tukiabudu katika siku ya Jumapili. Hakujibu kuwa ni kwa kuwa Sabato ilibadirishwa baada ya usurubisho, hakueleza kwamba Paulo aliibadiri, hakueleza kuwa ni kwa kuwa tulikuwa tukikumbukia ufufuo. Ni lipi alilosema? Nilistaajabishwa na jibu lake. Alijibu “Sijui!” Fikiri kufanya swala kila juma wakati haujui ni kwanini unalifanya katika siku na wakati unaolifanya! Hulusani pale unapokuwa unafahamu kile kinachofundishwa katika Biblia sawa kama yeye alivyokuwa anajua.

Tofauti na mchungaji wangu wa awali, na wachungaji wengine wengi katika ulimwengu leo, tunamwabudu Mungu katika siku yake ya Sabato – na tunafahamu wazi ni kwanini tunafanya hivyo.

Niliita makala hii “Siku Iliyo Kipenzi Kwangu” sababu hivyo ndivyo Sabato ilivyo. Ni wakati wa mapumziko, ni wakati wa kuwa na Mungu, ni wakati wa kukutana na watu niwapendao ili tuabudu pamoja, ni muda wa maombi na wa kujumuika pamoja. Mungu kaumba Siku iliyo kubwa na muhimu kiasi gani!

## MFUNGO NA SIKUKUU YA UPATANISHO



*Watu Wakifunga huko New Zealand*

Kwenye Siku ya Upatanisho, Biblia inasema “mzitese nafsi zenu” (Walawi 23:32). Ni kwanini wale wawezao katika kanisa la Continuing Church of God hufunga kwenye siku hiyo?

Katika Isaya 58:5 Biblia inafundisha kwamba siku ya kufunga ni siku ya kuitesa nafsi yako. Zaidi ya hapo, jionee swala jingine kutoka kwa Isaya:

12Bwawa, BWANA Mwenye Nguvu, aliwaita siku ile ili kulia na kuomboleza, kung’oa nywele zenu na kuvaa nguo ya gunia. 13Lakini tazama, kuna furaha na karamu zilizojaa ulevi na ulafi, kuchinja ng’ombe na kuchinja kondoo, kula nyama na kunywa mvinyo! wakisema, “Sisi na tule na kunywa, kwa kuwa kesho tunakufa!” 14BWANA Mwenye Nguvu amelifunua hili nikiwa ninasikia, Bwana, BWANA Mwenye Nguvu asema: “Mpaka siku ya kufa kwenu dhambi hii haitafanyiwa upatanisho” (Isaya 22:12-14).

Elewa kwamba kushindwa kuepuka chakula wakati umeagizwa hivyo imechukuliwa sawa na kutokuwa na upatanisho. Na pamoja na kwamba neno lililotafasiriwa sawa na upatanisho katika Isaya 22:14 siyo lile neno la Kiebrania lililo katika Walawi 23, ni maneno yaliyo sawa katika maana na matumizi.

Siku ya Upatanisho iliitwa “Mfungo” katika Matendo 27:9.

Jionee kile ambacho marehemu Herbert Armstrong aliandika:

Siku ya Upatanisho, au Mfungo

Kisha, ebu na tusome katika Walawi 23:26, 27, 31-32: “26BWANA akamwambia ... 27“Siku ya kumi ya mwezi huu wa saba ni Siku ya Upatanisho. Mtafanya kusanyiko takatifu, mfunge.... 31Hamtafanya kazi kamwe. Hili litakuwa agizo la kudumu kwa vizazi vijavyo po pote mnapoishi. 32Ni sabato ya mapumziko kwenu ninyi, ni lazima mfunge. Tangu jioni ya siku ya tisa ya mwezi hadi jioni inayofuata, mtaishika sabato yenu”.

Siri ya ajabu! Kupatana na Mungu! Mwaadamu hatimaye afanyika mmoja na Muumba wake! ...

Na tunaikuta hii sikukuu ya mwaka imetajwa katika Agano Jipya. Katika Matendo 27:9, pale Paulo alipokuwa katika safari yake ya hatari kwenda Roma, imeandikwa kwamba: “ 9Muda mwingi ulikuwa umepotea na kusafiri baharini kulikuwa hatari kwa sababu wakati huu ulikuwa baada ya siku za kufunga...” Liangalie neno hili “KUFUNGA” pembeni mwa Biblia yako. Utakuta maelezo yasemayo ‘Kufunga” ni Sikukuu ya Upatanisho ya siku ya 10 ya mwezi wa saba wa kalenda ya Mungu. Sasa basi siku hiyo isingeliweza kuwa imepita katika mwaka huo isipokuwa tu ikiwa walikuwa bado wanaishika. Vinginevyo Roho Takatifu ya Mungu isingeliyaongoza maneno hayo kuandikwa! Hakika hili linaashiria kwa kiasi kikubwa kwamba sikukuu hiyo bado ilikuwa ikiabudiwa na kushikwa na ilitambuliwa hivyo na Roho Takatifu ya Mungu. (Armstrong HW. Pagan Holidays or God’s Holy Days Which?).

Wale walio wa kanisa la Continuing Church of God walio waaminifu na wanaoweza kufunga hufunga kwenye Siku ya Upatanisho. Hii ni kwamba, hujiepusha na chakula chote pamoja na maji katika muda wote wa masaa 24 ya siku hiyo.

Je, kuna faida zozote za kufanya hivyo?

Kwanza jionee kile Biblia inachofundisha:

“5Je, hii ndiyo aina ya mfungo niliouchagua, siku moja tu kwa ajili ya mtu kujinyenyekeza? Je, ni kwa kuinamisha kichwa chini kama unyasi na kwa kujilaza juu ya nguo ya gunia na majivu? Je, huo ndio mnaouita mfungo, siku iliyokubalika kwa BWANA? 6“Je, hii si ndiyo aina ya mfungo niliyoichagua: kufungua minyororo ya udhalimu na kufungua kamba za nira, kuwaweka huru walioonewa na kuvunja kila nira? 7Je, sio kushirikiana chakula chako na wenye njaa na kuwapatia maskini wasiokuwa na makao hifadhi, unapomwona aliye uchi, umvike wala si kumkimbia mtu wa nyama na damu yako mwenyewe? 8Ndipo nuru yako itajitokeza kama mapambazuko na uponyaji wako utatokea upesi, ndipo haki yako itakapokutangulia mbele yako, na utukufu wa BWANA utakuwa mlinzi nyuma yako. 9Ndipo utaita, naye BWANA atajibu, utalia kuomba msaada, naye atasema: Mimi hapa. “Kama ukiiiondoa nira ya udhalimu, kutokunyoosha kidole na kuzungumza maovu, 10nanyi kama mkimkunjulia mtu mwenye njaa nafsi zenu na kutosheleza mahitaji ya walioonewa, ndipo nuru yenu itakapong’aa gizani, nao usiku wenu utakuwa kama adhuhuri. 11BWANA atakuongoza siku zote, atayatosheleza mahitaji yako katika nchi kame naye ataitia nguvu mifupa yako. Utakuwa kama bustani iliyonyweshwa vizuri, kama chemchemi ambayo maji yake hayakauki kamwe. 12Watu wako watajenga tena magofu ya zamani na kuinua misingi ya kale, utaitwa Mwenye Kutengeneza Kuta Zilizobomoka, Mwenye Kufanya upya Barabara zenye Makazi” (Isaya 58:5-12).

Hivyo, Biblia inafundisha kuna faida za kimwili na za kiroho pamoja na majukumu yaambatanayo na kufunga.

Hapa tunakuletea maelezo kutoka kwa Herbert W. Armstrong kuhusu kufunga:

KUFUNGA NA KUSALI: Hakuna . . . KIFANANACHO na kufunga

pamoja na kusali katika kumkaribia Mungu, kurejesha mawasiliano naye, kujazwa na Roho Takatifu yake. Kwa lengo hili ni vema kufunga jumla — hakuna kunywa juisi ya matunda ya aina yoyote. Katika enzi za Biblia walifunga nyakati zingine hata kuacha kutumia maji, lakini wakati mwingine maji yalitumika. Binafsi nadhani matokeo yatapatikana hata pale mtu anafunga kwa kunywa maji, lakini si kitu kingine.

Kwa makusudi zaidi ya kiroho kufunga kuanzia siku moja hadi siku tatu kwa ujumla inatoshia. Unaweza kupata maumivu ya kichwa, au kusikia hali ya kichwa kizito katika siku chache za awali. Si hali ya kupendeza. Kwa kutumia lugha ya ki-Biblia, Ni KUITESA NAFSI. Inahitaji kujituma na kujitoa, pamoja na kujikana nafsi. Ninapendekeza, kwa kusudi hili, ugwanyane muda wako katika mafungu matatu: kiasi cha theruthi moja katika kulisoma somo la kufunga katika Biblia, pamoja na masomo mengine ya Biblia. Tumia Itifaki nzuri, pamoja na maelezo yako ya pembeni mwa Biblia ikiwa yapo. Ikiwa Biblia yako haina hakikisha unatafuta iliyo nayo. Yatazame yote uwezayo kupata juu ya kufunga. Kisha tumia kama theruthi moja ingine kwa kutafakari — kuyawazia katika fikra zako, KWANINI umekuwa mbali na Mungu hivyo, kuwaza juu ya ni jinsi gani umeruhusu mambo ya kidunia yajipenyeze, utafakari juu ya uliyoyasoma katika Biblia, jinsi gani utayatumia katika maisha yako ya kila siku na katika maswala yako ya kiroho. Kisha, tumia theruthi nzima ya muda wako katika MAOMBI ya ndani na kina.

Je, umewahi kutumia SAA MOJA nzima katika kusali, ukiwa peke yako na Mungu mahala fulani patulivu na penye faragha, ukiwa katika magoti? Ni wachache sana wamewahi kufanya hivyo. Ikiwa haujawahi, safari ya kwanza utakapojaribu kufanya hivyo utakuta inahitajika kujitoa na uamuzi thabiti ikiwemo na kujilazimisha kubaki katika mfungo huku ukipambana na hiyo hisia ya njaa inayouma. Katika dakika tano ama kumi au hata pungufu zaidi, kila aina ya sababu ya kukufanya uahirishe kufunga itakuja katika fikra zako. Hauko tayari kwa sasa — kwanini usifunge baadaye? Umekumbukia jambo fulani ambalo linatakiwa litekelezwe, na unadhani ni muhimu ukaenda mara moja kulitekeleza muda huo. Ndiyo, ninajua kile kitakachokuja katika fikra zako, kwani mimi pia nimeyafanya na ninajua kupitia uzoefu. Lakini endapo utapingana na kila jaribu, na kuendelea KUBAKI katika magoti yako, hata ikiwa unadhani maombi yako hayapenyi zaidi ya paa la nyumba, katika takribani dakika 30 au 40 hivi mwovu hatimaye atakata tamaa na kuachana na wewe, nawe utajikuta umeingia katika mawasiliano na Mungu, na utakuta unaanza KUBURUDIKA katika kuzungumza naye — unaanza kuimimina nafsi yako kwake — utajikuta ukimweleza yote YEYE. Mara kwa mara tulia kwa muda, na utaafakari, umwache Mungu naye aongee na wewe. (Armstrong HW. Importance of Fasting. July 7, 1948).

Pamoja na kujinyenyekeza kwetu ikitusaidia kujitambua ni kwa jinsi gani tunahitaji kumtegemea Mungu na kumkaribia, kufunga pia kunafahamika kuwa na faida kadhaa za kimwili. Baadhi, ijapokuwa kwa bahati mbaya bado siyo wengi, katika ulimwengu wa tiba wameanza kutambua kuwa kuna faida za kiafya katika kufunga:

Uwezo Utokanao na Kufunga Mara kwa mara

Wanasayansi wanazidi kuvumbua ushahidi kwamba ufungaji wa vipindi vifupivifupi, ikiwa utatekelezwa vema, unaweza kuleta faida kadhaa za kiafya, ikiwemo uwezo wa kusaidia kupunguza uzito kwa watu wanene, kama Michael Mosley alivyovumbua...

Kupunguza ulaji wa vyakula vyenye wanga mwingi, kula vizuri lakini si kwa kushiba sana, ni moja ya mambo machache ambayo yameonyeshwa kuongeza urefu wa uhai, angalau kwa wanyama. Tumejua kuanzia miaka ya 1930s kwamba panya hula vyakula vyenye wanga kidogo, vyenye madini mengi (nutrients) na huishi muda mrefu zaidi kutokana na hilo. Upo ushahidi unaozidi kuongezeka kwamba hili pia liko kwa tumbili ...

Kiwango cha IGF-1 kinaweza kushushwa kwa kufunga. Sababu yaonekana kuwa ni kwamba pale miili yetu inapokuwa haipati vyakula hugeuka kutoka kwenye "Msukumo wa Ukuaji" (Growth Mode) na kwenda kwenye "Msukumo wa Ukarabati wa Mwili" (Repair Mode).

Kadri kiwango cha hormone za IGF-1 zinaposhuka, vichochezi vingi (repair genes) vya ukarabati wa mwili huonekana kuamshwa, kulingana na utafiti unaoendelea wa Professor Valter Longo wa Chuokikuu cha Southern California...

Mtazamo wa kisasa wa kidaktari ni kwamba faida za kufunga bado hazijathibitishwa na hadi kutakapokuwepo na utafiti zaidi kwa wanadamu inafaa angalau kula si chini ya calories 2000 kwa siku. Ikiwa unataka kweli kufunga basi unapaswa ulifanye hilo vema na kwa usimamizi wa madaktari ama kliniki, sababu wapo watu wengi, kama vile wenye mimba ama wenye kisukari walio katika matumizi ya dawa, ambao kwao yaweza kuwa ni hatari. <http://www.bbc.co.uk/news/health-19112549>

Kufunga Hupunguza Athali za Ugonjwa wa Moyo na Kisukari

Utafiti ulifanyika kwa watu zaidi ya 4,500 wa imani ya Ki-Mormon kule Utah Marekani. Watafiti walifuatilia tabia zitokanazo na athari za eneo la chini la ugonjwa wa moyo (coronary artery disease—heart disease). Baada ya kuangalia sababu zingine pia (uvutaji sigara, utumiaji pombe, unywaji kahawa, na chai), watafiti waligundua kwamba wale waliokuwa wakifunga mara kwa mara (bila kula wala kunywa maji) walikuwa katika uwezekano kidogo wa kukumbwa na ugonjwa wa moyo kuliko wale wasiofunga. Ufungaji pia ulihusika na kuwa na uwezekano kidogo wa ugonjwa wa kisukari (The American Journal of Cardiology, October 1, 2008).

Kufunga Angalau Mara Mbili kwa Mwaka Huuimarisha Mfumo wa Kinga

Utafiti Mpya Umpendekeza kwamba Kufunga Kunaweza Kusaidia Mwili Uweze Kupambana na Magonjwa kwa Kuuamusha Mfumo wa Kinga za Mwili. Utafiti Uliiongeza kwamba Kufunga Angalau Kwa Siku Mbili Kunaweza

Kuuamusha Mfumo wa Kinga za Mwili.

Kutokana na utafiti, matokeo ya kufunga kwa vipindi vya siku mbili hadi nne kila miezi sita kwa panya na pia kwa wanadamu kulifanyiwa uchunguzi na watafiti. Katika sehemu zote, iligundulika kwamba muda mrefu wa kuacha kula ulishusha idadi ya chembechembe nyekundu kwa kiwango kikubwa.

Na kwa panya, kila hatua ya kufunga kula ilisababisha hali ya mwili kujikarabati kwa kuzalisha chembechembe nyeupe mpya, ambazo nazo ziliongeza nguvu ya mfumo wa kinga ya mwili.

Valter Longo, Professor wa elimu ya Kinga ya Mwili pamoja na Sayansi ya Bayolojia (Gerontology and the Biological Sciences) katika Chuokikuu cha Southern California, alisema: "Huziruhusu chembechembe kuu (stem cells) kuanza kuujenga upya mfumo mzima wa kinga. Na habari njema ni kwamba wakati wa kufunga, mwili hupata fursa ya kuachana na sehemu ya mfumo wa kinga ambao ama umechoka au umeharibika, eneo ambalo halitendi kazi kwa usahihi".

Aliiongeza kwa kusema kwamba mfumo ambao umeharibika kwa kiasi kikubwa kutokana na kemikali za mwilini ama na kuzeeka, kufunga mara kadhaa kunaweza kuzalisha, kiujumla, mfumo mpya wa kinga.

Uchunguzi pia ulibainisha kwamba kiwango cha enzyme PKA, hushuka kutokana na kufunga. Hili huongeza urefu wa uhai kwa viumbe, ikiwemo pia kiwango cha hormone IGF-1, ambayo imehusishwa na uzeekaji, mwili kuchakaa na athari za kansa. <http://www.delhidailynews.com/news/Fasting-regenerates-immune-system-1402181003/>

Ufungaji ni kichocheo cha afya kwa wengi na pia inaonekana kuongeza urefu wa uhai. Ni dhahiri, kwa walio na matatizo ya kiafya ama walio katika kukabiliwa na kifo hawapaswi kufunga. Lakini kwa wengineo, inaweza kuwa ni kicheocheo cha afya zao, swala muhimu la kufanya kwa ajili ya maswala ya kimwili na ya kiroho pia.

Baadhi ya watu, hususani wale ambao hutumia kahawa mara kwa mara, huona kufunga ni taabu. Wale ambao huanza kwa kupunguza kwanza kiasi cha kahawa wanayotumia hukuta ufungaji unakuwa rahisi kuliko kama wangeanza kufunga moja kwa moja.

Hapa tunakuletea maoni ya Kiyahudi ya jinsi ya kujiandaa kufunga:

Dondoo za Mfungo wenye Tija

Vidokezo kwa kujiandaa kufunga ni pamoja na: Unywaji wa maji angalau lita mbili kwa siku (vikombe 10) kwenye siku zinazotangulia siku ya kufunga, na ulaji wa vyakula vya wanga pamoja na mbogamboga kwenye siku inayotangulia, wakati ukiepuka vyakula vyenye sukari, vyenye mafuta mengi, vilivyokaangwa na vyenye chumvi nyingi; kwani husababisha kiu.

Wale ambao hutumia kiasi kikubwa cha vinywaji vyenye

caffeine kila siku (kahawa, chai isiyo herb tea, soda) wanashauriwa waanze kupunguza unywaji huo taratibu, wakianza siku kadhaa kabla ya siku ya kufunga ili kupunguza kiwango cha caffeine mwilini kisisababishie matokeo kama vile kuumwa kichwa, kichefuchefu na kichwa kuwa kizito.

Mlo wa mwisho kabla ya kuanza kufunga ambao huitwa: “seudah hamafseket”, hautakiwi kuhusisha vyakula usivyovizoea, vyenye viungo vingi, ama vilivyo kaangwa; na havitakiwi kuwa na aina za mbogamboga kama cauliflower, cabbage ama broccoli.

Baada ya siku ya kufunga, wale ambao walijizua kula na kunywa wanashauriwa kuanza kurejesha maji taratibu (rehydrate slowly), kwa kutumia kinywaji kitamu kama juisi, na kuanza kula kitafunwa kwanza, kisha kula mlo mwepesi baada ya saa moja hivi kupita. <http://www.Israelnationalnews.com/News/News.aspx/148579>

Kwa upande wangu, mimi hupendelea kunywa maji mengi kwenye siku ya kabla ya kufunga, na huwa naepuka vyakula vyenye chumvi nyingi.

Vilevile, wale ambao hufunga mara kwa mara katika mwaka huwa hawapati shida yoyote kutokana na kufunga ukilinganisha na wasio na mazoea ya kufunga.

Sikukuu ya Kikristo ya Siku ya Upatanisho, huja baada ya Sikukuu ya Kuzipiga Baragumu (Feast of Trumpets) ambayo pia inajulikana kama Rosh Hoshana (Rosh Hashanah) na ni sehemu ya mpango wa Mungu wa wokovu unaoonyeshwa katika siku takatifu za kibiblia (ijapokuwa watu mara nyingi huziita za ‘Ki-yahudi’).

Vipengele vya Imani (Statement of Beliefs) vya kanisa la Continuing Church of God vinasema:

Siku ya Upatanisho, inayoitwa “Mfungo” katika Agano Jipya (Matendo 27:9), inasaidia kuonyesha udhaifu wetu na uhitaji wetu wa kuwa karibu na Mungu (Isaya 58:5,11). Inasaidia pia kuonyesha kwamba Shetani anahusika na dhambi za wanadamu na kwamba atakamatwa na kufungwa kwa miaka elfu moja (Ufunuo 20:1-3; Walawi 16:20-26; Isaya 14:12-16).

Hivyo, kutokana na kuwepo kwa taarifa zake katika Agano Jipya, Sikukuu ya Upatanisho inapaswa iwe ni kitu chenye umuhimu mkubwa kwa Wakristo.

Walio wa kanisa la Continuing Church of God huwa tunafunga kila mwaka kwenye Siku ya Upatanisho na vilevile wakati mwingine wowote katika mwaka, kila ambapo mtu binafsi anapohitaji kulingana na hali yake ya kiroho (ona: Marko 2:19-20).

Siku ya Upatanisho katika 2014 itanzia kwenye machweo ya tarehe 3 Octoba na kuendelea hadi machweo ya tarehe 4 Octoba. Katika mwaka 2015, Siku ya Upatanisho itanzia kwenye machweo ya tarehe 22 Septemba na kumalizikia kwenye machweo ya tarehe 23 Septemba.

## IRAQ KATIKA UNABII



Na Bob Thiel

Iraq imetajwa sana katika vyombo vya habari kwa miongo mingi kwa sababu ya vita vya Iran-Iraq, vita vya Kuwait, vita vyake na Marekani, pamoja na kugoma kwa waasi wa Kisuni huko.

Je, Biblia inafundisha nini kitatokea kwa Iraq? Je, nabii hizi zitatimia?

Ni malengo makuu ya Al-Qaeda pamoja na kikundi cha Islamic State in Iraq and Syria (ISIS) kuanzisha utawala wa Kiislamu (Islamic caliphate), katika Iraq na Syria. ISIS imedai tayari imetekeleza hilo kwa kulitangaza eneo ambalo wameliteka kuwa ni Taifa la Kiislamu – Islamic State.

Pamoja na kwamba ili hii Islamic State itimize nabii za Kibiblia italazimika kubadirika, kuna maswala ya uwepo wa milki kuu ya kiislamu yanayopatana na nabii za Biblia hususani kuhusu kuja kwa Mfalme wa Kusini katika Danieli 11:40-43.

### Biblia Inafundisha Nini Juu ya Hili?

Ni lipi lililo la Kibiblia litakalotokea kwa Iraq? Kwanza ni muhimu ielezwe kwamba watu walio wengi kule Iraq wametokana na wazao wa Kiarabu, kama vile Ishmaeli na mama yake Hajiri (Hagari).

Biblia inaonyesha kwamba karibia na mwisho, kutatokea muunganiko wa nchi za Kiarabu na watu wa asili ya Kituruki, pengine yaweza kuwa hata na Wakurdi pia.

Jionee yafuatayo:

“3Kwa hila wanafanya shauri dhidi ya watu wako, wanafanya shauri baya dhidi ya wale unaowapenda. 4Wanasema, “Njoni, tuwaangamize kama taifa, ili jina la Israeli lisikumbukwe tena.” 5Kwa nia moja wanapanga pamoja mashauri mabaya, wanafanya muungano dhidi yako, 6mahema ya Edomu na Waishmaeli, ya Wamoabu na Wahagari, 7Gebalia, Amoni na Ameleki, Ufilisti, pamoja na watu wa Tiro. 8Pia Ashuru wameungana nao kuwapa nguvu wazao wa Loti” (Zaburi 83:3-8).

Ni mtazamo wangu kwamba mengi ya mataifa yaliyotajwa

katika Zaburi 83 wataazimia kutumia mbinu ya ugaidi. Zaburi 83 inazungumzia juu ya kuwepo kwa muunganiko wa watu wa mataifa ya Kiarabu, Kituruki (Edomu), na ya Ulaya (Ashuru). Hii inaihusisha Iraq pia.

Biblia inaonyesha kwamba ugaidi umetabiriwa kuwepo:

14“Lakini kama hamtanisikiliza na kutimiza maagizo haya yote, 15nanyi kama mtazikataa amri zangu na kuzichukia sheria zangu, tena mkishindwa kutimiza amri zangu na hivyo mkavunja agano langu, 16ndipo nitakapowafanyia hili: ‘Nitawaletea juu yenu hofu ya ghafula, magonjwa ya kufisha na homa itakayopofusha macho yenu na kuwaondolea uhai wenu. Mtapanda mbegu bila ya mafanikio, kwa sababu adui zenu wataila. 17Nitauielekeza uso wangu dhidi yenu ili kwamba mshindwe na adui zenu, wale wanaowachukia watawatawala, nanyi mtakimbia ingawa hakuna mtu anayewafukuza (Walawi 26:14-17).

25Barabarani upanga utawakosesha watoto, nyumbani mwao hofu itatawala... (Torati 32:25).

12Piga kelele na uomboteze, Ee mwanadamu, kwa kuwa upanga u dhidi ya watu wangu, u dhidi ya wakuu wote wa Israeli. Wametolewa wauawe kwa upanga pamoja na watu wangu. Kwa hiyo pigapiga kifua chako (Ezekieli 21:12).

12Hivi ndivyo walivyo waovu, sikuzote hawajali, wanaongezeka katika utajiri 19Tazama ni jinsi gani wanavyoangamizwa ghafula, wanatoweshwa kabisa na vitisho (Zaburi 73:12,19).

25kwa kuwa mliyapuza mashauri yangu yote na hamkukubali karipio langu, 26mimi nami nitawacheka katika maafa yenu, nitawadhihaki wakati janga litakapowapata, 27wakati janga litakapowapata kama tufani, wakati maafa yatakapowazoa kama upepo wa kisulisuli, wakati dhiki na taabu zitakapowalemea (Methali 1:25-27).

Kuongezeka kwa Wanajihadi katika maeneo mengi mbalimbali ya ulimwengu ni utangulizi wa kupelekea kuwepo na ugaidi zaidi. Muungano dhidi ya Marekani, dhidi ya washirika wake wa asili ya Kiango-Saxon (Mataifa yaliyotokana na Uingereza kama Kanada, Australia n.k.), pamoja na dhidi ya Israeli utakaoshirikisha majeshi ya Kiarabu na ya Ulaya unakuja. Na kwa muda mrefu nimeamini kwamba ugaidi utakuwa ni mojawapo ya mbinu zitakazotumika.

Biblia inaonyesha kwamba Iraq itaishia katika hali fulani ya kuungana na umoja wa mataifa ya Kiarabu na ya Waturuki (Kibiblia Edomu) wa siku za mwisho:

40“Katika wakati wa mwisho mfalme wa Kusini atapigana naye vita, naye mfalme wa Kaskazini atamshambulia kwa magari ya vita na askari wapanda farasi na idadi kubwa ya meli. Atavamia nchi nyingi na kukumba nchi hizo kama mafuriko. 41Pia atavamia Nchi yakupendeza. Nchi nyingi zitapinduliwa, bali Edomu, Moabu na viongozi wa Amoni wataokolewa kutoka katika mkono wake. 42Atapanua mamlaka yake juu ya nchi nyingi, Misri haitaepuka” (Danieli 11:40-42).

“Neno la BWANA likanijia kusema: 2“Mwanadamu, toa unabii na useme: ‘Hili ndilo BWANA Mwenyezi asemalo: “ ‘Ombotezeni ninyi na msemi, ‘Ole wa siku ile!’ 3Kwa kuwa siku ile imekaribia, siku ya BWANA imekaribia, siku ya mawingu, siku ya maangamizi kwa mataifa. 4Upanga utakuja dhidi ya Misri, nayo maumivu makuu yataijia Ethiopia. Mauaji yatakapoangukia Misri, utajiri wake utachukuliwa na misingi yake itabomolewa. 5Ethiopia na Putu, Ludi na Arabia yote, Libya na watu wa nchi ya agano watauawa kwa upanga pamoja na Misri” (Ezekieli 30:1-5).

Hivyo umoja utanzishwa, Iraq itakuwa sehemu ya ushirika huo, na mengi ya mataifa hayo ambayo yataingia kwenye ushirikiano na Misri yataathirika vibaya. Iraq itashirikiana na huyu ambaye Biblia inamtaja kuwa atakuwa ni Mfalme wa Kusini.

Ebu jionee kile ambacho mwandishi mmoja wa Kanisa la Mungu (COG) aliwahi kufundisha:

Danieli 11 pia inataja juu ya baadhi ya watu wa Mashariki ya Kati ambao watahusika katika mapambano hayo ya mataifa katika hitimisho la zama zetu. Wahusika wakuu watakuwa ni pamoja na “Mfalme wa Kaskazini”, ambaye atakuwa ni kiongozi wa Muungano wa Ulaya (ama hatua yake ya mwisho, akiitwa “Mnyama”). “Mfalme wa Kusini” (ambaye atakuwa akiongoza mataifa ya Kiislamu—yaonekana anaweza kutokea Misri {au} hata taifa jingine la Kiislamu) naye pia ametajwa. Nchi ama mataifa yafuatayo yametajwa moja kwa moja: Misri, Nchi Takatifu (Israeli/Palestina), Ethiopia (Wakushi wa leo, wako kusini mwa Misri), Libya, Edomu, Moabu na Amoni. Wengi wa wazawa wa kale wa watu waliojulikana kama Waedomu ama Waidumea kwa sasa wanaishi katika eneo la Ukingo wa Magharibi (Palestina), Jordan, Iraq, Turkey, Syria, Arabia, Yemen, pamoja na baadhi ya mataifa ya Guba ya Uajemi (the Persian Gulf states), etc. (McNair R. Solving the Arab-Israelii Impasse! Copyright Raymond F. McNair 2005).

Lakini sasa huyu “Mfalme wa Kusini” ni nani?...katika aya ya 40 tunapelekwa hadi “nyakati za mwisho”...aya hii yamkini ilitimizwa kwa sehemu wakati wa mapambano ya mwaka 1896...Lakini Mussolini hakuukamilisha unabii...Sawa na ambavyo kutakuwa na “mfalme wa kaskazini” wa mwisho... kwa jinsi ileile, kutaibuka “mfalme wa kusini” wa mwisho—kiongozi wa kiujumla wa ushirika wa mataifa ya kiarabu ya kiislamu, pengine hata akibeba cheo cha kuitwa Mahdi... Zaburi ya kiunabii (Zaburi 83) inatupatia taarifa za ziada juu ya hali halisi ya Mashariki ya Kati. Ujerumani (Ashuru katika unabii wa Biblia) pengine hata na baadhi ya Ulaya kwa ujumla wataingia katika ushirikiano na mwungano wan chi za Kiarabu...

“4Wanasema, “Njoni, tuwaangamize kama taifa, ili jina la Israeli lisikumbukwe tena.” 5Kwa nia moja wanapanga pamoja mashauri mabaya, wanafanya muungano dhidi yako, 6mahema ya Edomu (Esau yaani Uturuki ya sasa taifa lisilol la Kiarabu ila la Kiislamu) na Waishmaeli (Saudi Arabia), ya Wamoabu (sehemu ya Yordani) na Wahagari (hapo kale watu hawa waliishi katika eneo liljulikanalo leo kama Syria), 7Gebalia (Lebanoni), Amoni (Yordani ya leo) na Ameleki

(Sehemu ya Uturuki), Ufilisti (Upalestina ya leo), pamoja na watu wa Tiro (Lebanoni). 8Pia Ashuru (Ambao wazao wao ndio walihamia Ujerumani kale) wameungana nao kuwapa nguvu wazao wa Loti (Yordani na Iraq ya Magharibi)” (Zaburi 83:4-8)...

Lakini wakati wa mwisho, huu ushirika wa Ulaya na Waarabu utakuwa ni wa muda mfupi: “... naye mfalme wa Kaskazini atamshambulia (Mfalme wa Kusini) ...” Danieli 11:40-41... Mwingano wa mataifa ya Kiarabu-Kiislamu kwa ujumla, yatatupwa katika kuchanganyikiwa na vurugu kubwa kupitia uvamizi huo. (Stump K. The Arab World in Prophecy. Plain Truth, December 1979, pp. 11-12).

Baadhi hudhani kwamba Wahagari ndio ambao uzao wao uko Iraq—lakini kwa kuwa mama yake na Ishmaeli aliitwa Hagari (Hajiri)—Mwanzo 16:15—basi wote ni ndugu na wanahusiana. Iwe wanajulikana vema zaidi kama Wahagari ama Waishmaeli, Iraq pamoja na watu wengine wa asili ya Kiarabu wametabiriwa (wakiwa na jamii zingine) kuwa sehemu ya mwungano utakaozimia kuiangamiza Israeli.

## Babeli: Iliyopita na Ijaye

Babeli ya Kale ilikuwa inapatikana kwenye eneo lililoitwa Mesopotamia, ambayo kwa sasa ni sehemu ya nchi ya Iraq.

Baadhi ya wahubirio juu ya kunyakuliwa kwa kanisa kabla ya kuanza kwa Dhiki Kuu wao pia wanaamini kwamba mji wa Babeli ya kale ndio utakaokuja kutimiza unabii wa Babeli Mkuu wa kitabu cha Ufunuo (LaHaye T, Jenkins J. Are We Living in the End Times? Tyndale House, Wheaton (IL), 1999, pp. 133-135 ; Walvoord J. The Prophecy Handbook. Victor Books, Wheaton (IL), 1990, pp. 608-611). Hili halingewezekana. Mji wa kale wa Babeli ulikoma kuwa na umuhimu wowote wa kidini kwa maelfu kadhaa ya miaka sasa.

Jiografia nayo moja kwa moja inaiondolea mbali Babeli ya kale. Jiji la Babeli ya kale lilikuwa limejengwa kwenye tambarare. Wakati, “Babeli Mkuu” ya Ufunuo inahusiana na jiji lililo kwenye vilima saba (Ufunuo 17:9). Unahusishwa pia kuwa na historia ya kuwatesa Wakristo wa kweli, jambo ambalo halikuwahi kutokea (kwa namna yoyote muhimu) wakati wa Babeli ya kale.

Wote wanatakiwa kuelewa kwamba kitabu cha Ufunuo kiujumla hutumia miji ikiwa na majina tofauti na uhalisia wake (mfano Ufunuo 11:8); na kwamba mara nyingi huongezea neno la ufafanuzi kama vile (Mkuu) baada ya neno Babeli (mfano Ufunuo 17:5), hivyo hatupaswi kung’ang’ania kwamba mji wa Babeli ya kale ndio unaohusishwa. Zaidi sana, Agano la Kale linataja utawala wa mfalme wa Kaskazini kama “Binti wa Babeli” (Ona: Yeria 50:41-43; Zekaria 2:6-7) kitu ambacho kinafanana na Babeli ya Ufunuo—hivyo ni aina nyingine ya Babeli ndiyo inayotolewa unabii wa nyakati za mwisho.

Inatakiwa ieleweka kwamba kwa vile watu wa Mungu wameonywa moja kwa moja wakimbie kutoka kwa “Binti wa Babeli” aliye Kaskazini (Zekaria 2:6-7) sawa na isemavyo juu ya Babeli wa Ufunuo (18:2-4); inafanya mtu atambue siyo lazima kwa Babeli katika Ufunuo kuwa ndiyo Babeli ya kale (Babeli ya kale hata hivyo iko eneo la mashariki, na ni kwa sehemu ndogo

sana iko kaskazini mwa Yerusalemu). Hivyo, muumini yeyote wa Kiprotestanti anayefundisha kuwa Babeli ya kale ndiyo Babeli ya Mnyama wa Ufunuo ni dhahiri yuko katika makosa. ‘Binti wa Babeli’ wa nyakati za mwisho anaitwa “Babeli Mkuu, Mama...”

“4Huyo mwanamke alikuwa amevaa mavazi ya rangi ya zambarau na nyekundu, yakimetameta kwa dhahabu, vito vya thamani na lulu. Mkononi mwake alikuwa ameshika kikombe cha dhahabu kilichojaa mambo ya machukizo na uchafu wa uzinzi wake. 5Kwenye kipaji chake cha uso palikuwa pameandikwa jina:

“SIRI, BABELI MKUU, MAMA WA MAKAHABA NA MACHUKIZO YA DUNIA.”

6Nikaona kuwa huyo mwanamke alikuwa amelewa kwa damu ya watakatifu, yaani, damu ya wale watu waliouawa kwa ushuhuda wa Yesu. Nilipomwona huyo mwanamke, nilistaajabu sana. 7Ndipo yule malaika akaniambia, “Kwa nini unastaajabu? Nitakufafanulia siri ya huyo mwanamke na huyo mnyama aliyempanda, mwenye vichwa saba na pembe kumi. 8Huyo mnyama, ambaye ulimwona, wakati fulani alikuwepo, lakini sasa hayupo, naye atapanda kutoka katika lile shimo lisilo na mwisho na kwenda kwenye maangamizo. Watu waishio duniani ambao majina yao hayakuandikwa kwenye kitabu cha uzima tangu kuumbwa kwa ulimwengu watastaajabu kumwona huyo mnyama, kwa maana alikuwepo, wakati fulani na sasa hayupo, lakini atakuja. 9“Hapa ndipo penye akili pamoja na hekima. Vile vichwa saba ni vilima saba ambavyo huyo mwanamke amevikalia” (Ufunuo 17:4-10).

“18Yule mwanamke uliyemwona ni ule mji mkubwa unaotawala juu ya wafalme wa dunia” (Ufunuo 17:18).

“1Baada ya haya nikaona malaika mwingine akishuka kutoka mbinguni, akiwa na mamlaka makuu na dunia ikamulikiwa na mng’ao wake. 2Naye akalia kwa nguvu kwa sauti kubwa, akisema: “Umeanguka! Umeanguka Babeli ulio mkuu! Umekuwa makao ya mashetani na makazi ya kila pepo mchafu, makazi ya kila ndege na kila mnyama achukizaye. 3Kwa maana mataifa yote yamekunywa mvinyo wa uasherati wake, nao wafalme wa dunia wamefanya uzinzi naye, nao wafanyi biashara wa dunia wametajirika kutokana na wingi wa utajiri wake.” 4Kisha nikasikia sauti nyingine kutoka mbinguni ikisema: “Tokeni katikati yake, enyi watu wangu, ili msije mkashiriki dhambi zake, ili usije ukapatwa na pigo lake lo lote, 5kwa kuwa dhambi zake zimelundikana hadi mbinguni, naye Mungu ameukumbuka uhalifu wake. 6Mtendee kama yeye alivyotenda, umlipe mara mbili kwa ajili ya yale aliyotenda. Katika kikombe chake mchanganyie mara mbili ya kile alichochanganya. 7Mpatie mateso na huzuni nyingi sawa na utukufu na anasa alizojipatia. Kwa kuwa moyoni mwake hujivuna akisema, ‘Mimi ninatawala kama malkia, mimi si mjane wala sitaona huzuni kamwe.’ 8Kwa hiyo mapigo yatampata kwa siku moja: mauti, maombolezo na njaa. Naye atateketewa kwa moto, kwa maana amhukumuye ni Bwana Mungu Mwenyezi” (Ufunuo 18:1-8).

Hii ni sehemu ambayo Wakristo wanapaswa kuiepuka na itakuwa inapatikana Ulaya, siyo Iraq. Roma ndio mji mashuhuri zaidi wenye vilima saba, na kwa kuwa Babeli ya Iraq iko kwenye tambarare, haiwezi kuwa ndiyo inayozungumziwa katika Maandiko. Lakini sawa na jinsi wengi hawatauelewa ukweli kuhusu Babeli ya nyakati za mwisho, elewa ndiyo maana imeitwa SIRI Babeli Mkuu katika Ufunuo 17.

Wale waaminio na wadhaniao kwamba Babeli ya kale inatakiwa kufufuliwa na kujengwa upya ndipo utimilifu wa nabii za kibiblia zitimie watakuwa wakitarijia jambo ambalo kibiblia halitarajiwi kutokea.

Jionee unabii ufuatao ambao unaweza kuhusiana na mashambulizi ya Mfalme wa Kaskazini dhidi ya Mfalme wa Kusini:

“11Kwa kuwa hili ndilo BWANA Mwenyezi asemalo: ‘Upanga wa mfalme wa Babeli utakuja dhidi yako. 12Nitafanya makundi ya watu wako wenye jeuri kuanguka kwa panga za watu mashujaa, taifa katili kuliko mataifa yote. Watakiwunjavunja kiburi cha Misri, nayo makundi yake yote ya watu wenye jeuri yatashindwa” (Ezekieli 32:11-12).

Huu SIYO unabii kuhusu Iraq kuishambulia Misri. Huu ni unabii juu ya nyakati za mwisho ambapo Babeli ya nyakati za mwisho, Mfalme wa Kaskazini wa Ulaya, atayashinda majeshi yaliyokwenye ushirika na Misri.

Jionee aya zifuatazo pia:

“13Nitaangamiza mifugo yake yote wanaojilisha kando ya maji mengi, hayatavurugwa tena kwa mguu wa mwanadamu wala kwato za mnyama hazitayachafua tena. 14Kisha nitafanya maji yake yatulie na kufanya vijito vyake vitiririke kama mafuta, asema BWANA Mwenyezi. 15Nitakapoifanya Misri kuwa ukiwa na kuiondolea nchi kila kitu kilichomo ndani yake, nitakapowapiga wote waishio humo, ndipo watakapojua kuwa Mimi ndimi BWANA” (Ezekieli 32:13-15).

Tambua pia kwamba yaweza kuwa aya hii inahusika na mwanzo wa siku ya mwisho ya Siku ya Bwana na kwahiyo aya hii haijatimizwa na hivyo maelezo haya katika kitabu cha Ezekieli yanaweza kuwa yanahusika na Misri pamoja na washirika wake watakaokuja wa kipindi cha karne ya 21.

## Harmagedoni

Pamoja na wengi kuwa wameshasikia juu ya “Harmagedoni”, jina hili limetumika katika Biblia mara moja pekee:

“12Malaika wa sita akamimina bakuli lake kwenye mto mkubwa Eufirati, maji yake yakakauka ili kutayarisha njia kwa ajili ya wafalme watokao mashariki. 13Kisha nikaona roho wachafu watatu waliofanana na vyura wakitoka katika kinywa cha lile joka na katika kinywa cha yule mnyama na katika kinywa cha yule nabii wa uongo. 14Hizo ndizo roho za pepo wachafu zitendazo miujiza. Nazo huwaendea wafalme wa ulimwengu wote na kuwakusanya tayari kwa ajili ya vita katika siku ile kuu ya Mungu Mwenyezi. 15“Tazama, naja kama mwivi! Amebarikiwa yeye akeshaye na kuziweka

tayari nguo zake ili asiende uchi na kuonekana aibu yake”. 16Ndipo wakawakusanya wafalme pamoja mahali paitwapo “Harmagedoni” kwa Kiebrania” (Ufunuo 16:12-16).

Je, hili linahusiano gani na nchi ya Iraq?

Ukweli ni kwamba, mto Eufirati unatiririka kupitia huko. Majeshi yajayo kutokea mashariki ambayo yataishia kukusanyika Harmagedoni yatapitia Iraq.

Ni majeshi ya askari wangapi? Jeshi kubwa mno, la askari milioni 200 (Ufunuo 9:13-19).

Eneo la nchi ya Iraq linahusika na unabii wa Biblia wa nyakati za mwisho, lakini si kwa namna wengi waonekanavyo kuelewa. Iraq siyo Babeli ya kale, lakini itaasirika pale mto Eufirati utakapokauka na kuruhusu majeshi yatokayo mashariki yavuke kupitia katika nchi hiyo kwenye nchi kavu.

Majeshi ya askari wengi sana yatakusanyika kule Megiddo. Lakini yataangamia kwa kuteketezwa.

Lakini Ziko Habari Njema kwa Iraq

Pamoja na unabii juu ya kushindwa kwake vitani na kujihusisha kwake na Mfalme wa Kusini wa mwisho na pia Harmagedoni, napenda kueleza kwamba Iraq haitapoteza kila kitu. Wao pia hatimaye nao watapewa wokovu, na Biblia inaonyesha kwamba wataupokea.

Kushindwa vitani siyo hatima kwa Wairaq walio wengi. Badala yake, ni kufanywa watakatifu (Deification) ndiyo hatima yao.

## Lakini kwa namna gani?

Mtazamo sahihi wa “Kikristo” unafundisha kwamba hakuna wokovu kupitia njia nyingine yoyote bali ni kupitia kwa Yesu Kristo pekee (Matendo 4:10-12), kwa kuwa: “ 12 ... kwa maana hakuna Jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo” (Aya12).

Lakini ni nini kitakachotokea kwa idadi kubwa ya watu wa Iraq na kwingine kwingineko ambao hata hawakuwahi kulisikia jina la kweli la Kristo? Vipi kuhusu wale ambao hawatajali wala kuitikia sawa na Torati 4:29-31 ielezavyo? Na ni kipi kitatokea kwa wale ambao walizaliwa kabla ya huduma ya Kristo hapa duniani? Kumbuka Biblia inafundisha kwamba baada ya Adamu kutenda dhambi, wanadamu wote walizuiwa wasiendee mti wa uzima, kwa Mungu kuweka malaika aulinde mwanadamu asiufikie kwa mbinu zake mwenyewe (Mwanzo 3:22-24).

Hata imani ya kiujumla ya madhehebu ya Kiprotestanti inafundisha, sharti mtu amkiri Yesu kabla hajafa mauti ya kwanza, vinginevyo hataweza kuupata wokovu. Pengine ni kutokana na tofauti ya mitazamo kama hii baina yao na kanisa la Continuing Church of God, kwamba Waprotestanti huliita kanisa letu kuwa ni “dini/dhehebu”.

Mabaki ya Wanafiladefia ya Kanisa la Mungu (Filadelfia remnant of the Church of God), ambayo yanawakilishwa na kanisa la

Continuing Church of God, hufundisha kwamba Mungu kwa sasa anawaita kundi dogo tu, watu katika zama hizi ikiwakilishwa na Sikukuu ya Pentekoste (Day of Pentecost) (ambayo pia huitwa Siku ya Malimbuko, Hesabu 28:26) ikilifafanua hili: “18Kwa mapenzi Yake mwenyewe alituzaa kwa Neno la kweli, kusudi tuwe kama mazao ya kwanza katika viumbe Vyake vyote” (Yakobo 1:18).

Yesu pamoja nasi tulio wa kanisa la Continuing Church of God tunafundisha: “44Hakuna mtu awezaye kuja kwangu kama asipovutwa na Baba aliyenituma...” (Yohana 6:44).

Na hawa ni wachache tu kwa kipindi hiki:

“14Kwa maana walioitwa ni wengi, lakini walioteuliwa ni wachache” (Mathayo 22:14).

“14Lakini mlango ni mwembamba na njia ni finyo ielekeayo kwenye uzima, nao ni wachache tu...” (Mathayo 7:14).

Wa imani za Kiprotestanti na Wakatoliki wanaelewa kwa usahihi kwamba Mungu huwatumia watumishi wake (Wachungaji) kuhubiri (Warumi 10:14). Lakini, bahati mbaya, ujumbe wanaohubiri wachungaji wao hauko sahihi na ni kinyume cha Biblia.

Katika Isaya 6:9-11 Mungu anafundisha:

“9Akasema, “Nenda ukawaambie watu hawa: “Mtaendelea daima kusikia, lakini kamwe hamtafahamu, mtaendelea daima kuona, lakini kamwe hamtatambua.’ 10Fanya mioyo ya watu hawa kuwa migumu, fanya masikio yao yasisikie na upofushe macho yao. Ama sivyo wanaweza kuona kwa macho yao, wakasikia kwa masikio yao, wakatambua kwa mioyo yao, nao wakageuka na kuponywa.” 11Ndipo nikasema, “Hadi lini, Ee Bwana?” Naye akanijibu: “Hadi miji iwe imeachwa magofu na bila wakazi, hadi nyumba zitakapobaki bila watu, na mashamba yatakapoharibiwa na kuangamizwa”.

Kwa maneno mengine, wengi wa wanadamu hawawezi kwa sasa kuuelewa ujumbe wa Mungu hadi wakati wa zama za watu wote kuitwa ziwadie.

Labda pale tu mtu wa Iraq awe ametenda dhambi isiyosameheka (nao ni wachache mno wawezao kuwa wameitenda) vinginevyo atahukumiwa kuwa ni miongoni mwa ambao walikuwa bado hawajaitwa.

Biblia inafundisha wazi kabisa kwamba wokovu hatimaye utatolewa kwa wote. Na hii inawahusu hata Wairaq pia. Ebu jionee maandiko yafuatayo:

“6...na watu wote watauona Wokovu wa Mungu” (Luka 3:6).

Wale ambao hawakuwa wameitwa wakati wa kipindi hiki cha zama zetu (ikiwemo watu waliowengi wa taifa la Iraq, ikiwemo hata na wengi ambao walikufa zamani) watapewa fursa yao ya wokovu.

Na karibia wote miongoni mwao wataupokea. Kanisa la Continuing Church of God linafundisha kwamba Mungu atampatia kila mwanadamu fursa ya kuupata wokovu –na kwamba karibia

kila mtu ataipokea fursa hiyo. Wengi wa wanadamu hatimaye wataingia katika familia ya Mungu.


Hii inamaana kwamba karibia kila Muiraq atafanyika sehemu ya kudumu ya Ufalme wa Mungu. Ebu jionee baadhi yafafanuzi kutoka katika Kitabu cha Ufunuo:

“2Nikaona Mji Mtakatifu, Yerusalemu mpya, ukishuka kutoka mbinguni kwa Mungu, ukiwa umeandaliwa kama bibi arusi aliyepambwa kwa ajili ya mumewe. 3Nami nikasikia sauti kubwa kutoka katika kile kiti cha enzi ikisema, “Tazama, makao ya Mungu ni pamoja na wanadamu, naye atakaa pamoja nao. Yeye atakuwa Mungu wao nao watakuwa watu wake, naye Mungu mwenyewe atakuwa pamoja nao. 4Atafuta kila chozi, kutoka katika macho yao. Mauti haitakuwepo tena, wala maombolezo, wala kilio, wala maumivu, kwa maana mambo ya kwanza yamekwisha kupita” (Ufunuo 21:2-4).

Hivyo, pamoja na taarifa mbaya, hatimaye kutakuja taarifa njema za kupendeza kwa Wairaq, na kwa wanadamu wengine wote pia, zinazowahusisha kuwemo katika Ufalme wa Mungu ujao. Wote wanapaswa wayatii maneno ya Yesu Kristo na kusali: “Ufalme wako UJE” (Mathayo 6:10).



# ENCYCLOPEDIA YA KIKATOLIKI JUU YA KRISIMASI



Na Bob Thiel

Wengi wa wakirio kuwa ni Wakristo, na pia hata wengine ambao siyo, siku hizi husherehekea sikukuu iitwayo Krisimasi. Ni sherehe iliyobuniwa na inayosimamiwa na Kanisa la Rumi. Kwa kuwa haizungumzwi popote katika Biblia, je wasomi wa dhehebu la Roman Catholic wanatambua ni wapi sikukuu hii na nyingi ya vielelezo vyake vilitokea?

Ndiyo, wanajua.

Kitabu kitiwacho: Catholic Encyclopedia (Encyclopedia ni kitabu kielezacho taarifa za matukio ya kale) kinafundisha kwamba:

Krisimasi haikuwa miongoni mwa sikukuu za awali za Kanisa (Martindale C. Transcribed by Susanti A. Suastika. Krisimasi. The Catholic Encyclopedia, Volume III. Copyright © 1908 by Robert Appleton Company. Online Edition Copyright © 2003 by K. Knight. Nihil Obstat, November 1, 1908. Remy Lafort, S.T.D., Censor. Imprimatur. +Yohana Cardinal Farley, Archbishop of New York).

Maelezo haya juu ni yaki kweli. Wakristo wa awali hawakusherehekea Krisimasi, na hadi leo walio waumini wa makanisa yaitwayo Church of God, ikiwemo kanisa la Continuing Church of God bado hawasherehekei.

Disemba 25 Ilikuwa Kutoka Wapi?

Kwakuwa tarehe 25 Disemba haielezwi popote katika Biblia, sasa ilitokea wapi?

Disemba 25 hapo kale ilisherehekewa kama sikukuu ya kuzaliwa jua ikiwa ni sehemu ya tafrija za Kirumi iliyoitwa "Saturnalia". Inasemekana kuwa pia ndiyo tarehe ya siku ya kuzaliwa (birthday) ya muungu—jua wa kipagani, Mithras (ambaye pia maeneo mengine alitamkwa Mithra).

Jionee kile ambacho kitabu cha Wakatoliki cha The Catholic Encyclopedia kinachosema:

Constantine Mkuu: ... Constantine anapaswa kwa halali

kabisa kupewa heshima ya kuitwa "Mkuu", kwani ndiye aliyeibadiri historia ya ulimwengu kuielekeza kwenye mwelekeo mpya na akaufanya Ukristo...uwe dini ya Serkali yake... ni rahisi kutambua kwamba wafalme wengi wa milki ya Kirumi (emperors) walikubaliana na ushawishi kwamba wataweza kuwaunganisha raia wote wa milki yao waliabudu jua ambalo ndilo lilikuwa muungu wao ambalo walilichukulia kuwa ndiye Mungu- Baba wa Wakristo kwamba ndiye Mithras ambaye walikuwa wanamwabudu kwa heshima kubwa; hivyo walionelea milki yao itaweza kusimikwa upya chini ya umoja uletwao na dini moja. Hata Constantine... aliiheshimu sana hii imani potofu ... je, haiwezekani "Sol Deus Invictus", ambaye hata Constantine alizitengeneza sarafu za fedha ya milki yake zikiwa na sura yake, ama "Sol Mithras Deus Invictus", aliyeabudiwa na wafalme Diocletian pamoja na Galerius, wakawa miungu yenye nguvu ya milki? Constantine yaonekana alitafakari hivyo. Wala hakuachana na wazo hilo hata pale alipotokewa na ono la kimwujiza ambalo lilimshawishi kwa nguvu aelekee kukubaliana na Mungu wa Wakristo... Ni kweli kwamba waumini wa muungu Mithras walimwabudu kwenye siku ya Jumapili na pia walimwabudu kwenye Sikukuu ya tarehe za Krisimasi. Kutokana na hayo, Constantine haizungumzii siku ya Bwana, bali siku ya jua la milele. (Herbermann C., Georg Gp. Constantine the Great. The Catholic Encyclopedia. Vol. 4. Nihil Obstat. Remy Lafort, Censor. Imprimatur. +Yohana M. Farley, Archbishop of New York. New York: Robert Appleton Company, 1908).

Umithra: Hii ilikuwa ni dini ya kipagani iliyohusu kumwamini na kumwabudu muungu jua wa jamii ya kale ya Wahindi na Wairan, aliyetwa Mithra. Imani hii iliingia Ulaya kutoka Asia Ndogo baada ya Alexander Mkuu kuyateka maeneo hayo, ikasambaa kwa kasi sana hadi kuenea kote ambako Milki ya Rumi ilikfika, katika enzi za zama hizi; na ilifikia kilele chake katika nyakati za karne ya tatu, kisha ikaanza kutoweka kutokana na sheria kali za Mfalme Theodosius wakati wa mwishoni mwa karne ya nne... Helios Mithras ni muungu mmoja... Jumapili (Sunday) ilikuwa ndiyo siku yake, takatifu kwa ajili ya jua—Mithra, na kila siku ya kumi na sita ya kila mwezi ilikuwa ni teule kwake kama siku yake ya kupatanisha. Tarehe 25 ya kila mwezi Disemba ilisherehekewa kuwa ndiyo tarehe yake ya kuzaliwa (birthday), ikiitwa "natais invicti", kuzaliwa upya kwa jua la majira ya baridi (winter-sun), lisiloshindwa na mzunguko wa majira (Arendzen J. Mithraism. The Catholic Encyclopedia, Volume X. Nihil Obstat, October 1, 1911. Remy Lafort, S.T.D., Censor. Imprimatur. +Yohana Cardinal Farley, Archbishop of New York. New York: Robert Appleton Company, 1911).

Sikukuu ya kuzaliwa kwa muungu jua Mithras ndiyo ambayo Mfalme Constantine alikuwa akisherehekea na alikusudia raia wa milki yake wote nao waisherehekee pia. Naye akahakikisha inakubaliwa na maaskofu wa eneo la Ugiriki na Rumi wakati wa utawala wake.

Zaidi sana, hapa kuna taarifa zaidi kutoka kwenye kitabu hicho The Catholic Encyclopedia kama kinavyofundisha juu ya Krisimasi:

Krisimasi: ...Irenaeus pamoja na Tertullian (Waandishi wakuu

wa taarifa za awali wa Kirumi) hawakuitaja kwenye orodha yao ya Sikukuu; Origen, pengine baada ya kujionea sherehe ya kidhambi ya kuzaliwa kwa Mfalme (Imperial Natalitia), anaeleza (katika Lev. Hom. viii in Migne, P.G., XII, 495) kwamba katika Maandiko matakatifu ni wenye dhambi pekee yao, siyo watakatifu, ndio husherehekea siku ya kuzaliwa kwao (birthday); Arnobius (VII, 32 katika makala yake P.L., V, 1264) bado alikuwa akizidhihaki sikukuu za kuzaliwa kwa miungu ("birthdays of the gods").

Alexandria: Ushahidi wa awali kabisa juu ya sikukuu hii ulipatikana kule Misri. Kadri ya mwaka 200 B.K., Clement wa mji wa Alexandria (Strom., I, xxi in P.G., VIII, 888) alieleza kwamba wanatheolojia fulani wa Kimisri "wakishangaza sana" walitaja, siyo mwaka peke yake, bali hata na tarehe ya kuzaliwa kwa Kristo, wakisema ni tarehe 25 ya mwezi Pachon (20 Mei) katika mwaka wa 28 wa kutawala kwake Mfalme Augustus...

Cyprus, Mesopotamia, Armenia, Asia Minor. Huko Cyprus, mwishoni mwa karne ya 4, Epiphanius naye alitoa madai (Hær., li, 16, 24 in P. G., XLI, 919, 931) kwamba Kristo alizaliwa tarehe 6 Januari...

Roma: Huko Roma ushahidi wa awali kabisa unapatikana katika kalenda ya Philocalian (P. L., XIII, 675; inaweza kuangaliwa kwenye makala ya J. Strzygowski, Kalenderbilder des Chron. von Jahre 354, Berlin, 1888), iliyotengenezwa mwaka 354 B.K., ambayo ina vipengele vitatu muhimu. Katika kalenda ya serkali tarehe 25 Disemba imetajwa kuwa ni "Natalis Invicti" (Kuzaliwa kwa muungu -jua)...

Kufikia nyakati za Jerome na Augustine, tayari sherehe ya mwezi Disemba ikawa imeshazoeleka, ijapo kalenda iliyofuata (Epp., II, liv, 12, in P.L., XXXIII, 200) haiionyeshi kwenye orodha ya sikukuu muhimu. Kuanzia karne ya nne, kila kalenda ya nchi zote za Ulaya inaionyesha tarehe 25 Disemba...

Injili: Kuhusu tarehe ya kuzaliwa kwa Kristo vitabu vya Injili havitoi msaada wowote; juu ya taarifa zake kuna ubishi mwingi. Kufanyika kwa sense ("census") ya watu isingewezekana iwe nyakati za majira ya baridi: idadi yote ya raia wasingeweza kuhudhuria sensa hiyo wakati huo wa majira ya baridia...

Natalis Invicti: Sikukuu inayojulikana sana ya jua, iitwayo "Natalis Invicti", ilisherehekewa tarehe 25 Disemba, na inahusika kwa kiwango kikubwa na tarehe ya sasa ya sikukuu yetu ya mwezi Disemba. Kutokana na historia ya imani ya kuliabudu jua, tarehe hiyo ndipo jua lilikuwa kwenye mhimili wake katika Milki ya Rumi, na hii iliendana na imani ya Ki-Mithra, yasome haya katika Cumont's epoch-making "Textes et Monuments" etc., I, ii, 4, 6, p. 355...Taarifa za awali kabisa juu ya tarehe ya kuzaliwa kwa Kristo pamoja na jua ziko katika makala ya: Cypr., "De pasch. Comp.", xix, "O quam præclare providentia ut illo die quo natus est Sol . . . nasceretur Christous." - "O, ni Baraka ya kiwango gani tuliyopewa, kwamba kwenye siku ile ambayo Jua lilizaliwa. . . Kristo ndipo naye amezaliwa"... (Kutoka makala ya Krisimasi,

ilivyoandikwa katika kitabu: The Catholic Encyclopedia).

Hivyo, kitabu cha The Catholic Encyclopedia kinafundisha kwamba viongozi wa kanisa wa awali hawakuisherehekea Krisimasi, kwamba isingewezekana kwamba sensa aliyozungumzia Luka iwe ilifanyika majira ya baridi (hivyo haiwezekani Yesu Kristo awe alizaliwa Disemba 25 ambapo ni kipindi cha majira ya baridi), na tarehe hiyo tena inahusiano na upagani wa ibada ya muungu-jua ambako ndiko siku hiyo ilikoazimwa na kupandikizwa kwenye ukristo wa bandia wa Disemba 25 kuwa ni siku ya Kristo.

### Vipi Juu ya Vielelezo Viambatanavyo na Krisimasi?

Wakati ni dhahiri kabisa kwamba Disemba 25 imetolewa kwenye upagani na siyo kutoka katika Biblia, vipi sasa kuhusu vielelezo vinavyofanyika siku ya Krisimasi?

Kitabu cha The Catholic Encyclopedia kinafundisha:

Card na zawadi: Ilikuwa ni jadi ya kipagani ihusianayo na sherehe ya mwezi wa kwanza wa mwaka - Januari wenye kalenda, ambayo iliazimwa na kuigwa katika kusherehekea Krisimasi...

Gogo la Mti wa Yule: Moto uliokuwa ukiwashwa kutumia gogo la mti huu wakati wa majira ya Krisimasi ulileta mtafaruku mkubwa hata kwa Roma yenyewe, na St. Boniface alimwomba Papa Zachary waachane na desturi hiyo (Martindale C. Krisimasi, 1908).

Hivyo ni dhahiri kabisa kwamba waandishi wa historia wa awali wa Kirumi kama vile Irenaeus, Tertullian, na Origen hawakuifahamu Krisimasi, wala hata Augustine naye hakuiorodhesha kuwa ni miongoni mwa sikukuu muhimu za dini. Na ni kwamba hata maandiko ya baadaye ya Kikatholiki yanabainisha ukweli kwamba haiwezekani sensa (inayozungumzwa katika Luka 2:1) iwe ilifanyika wakati wa majira ya baridi -hivyo hili linaifanya tarehe 25 Disemba isiweze kuwa ndipo Kristo alipozaliwa (muda huo pia ingekuwa ni baridi kali mno kwa wachunga kondoo kuwoko makondeni wakichunga mifugo yao usiku mahala pa wazi katika kipindi cha baridi kama hicho, hivyo aliyoyaandika Luka 2:8, hayawezi kuwa yalifanyika kipindi cha majira ya baridi, jambo linaloishanya Disemba 25 isiweze kabisa kuwa ndio muda na majira aliyozaliwa Kristo).

Inatakiwa pia ieleweke kwamba mashada ya maua, kulingana na Tertullian ambaye awali alikuwa kipenzi wa imani ya Roman Catholic, yalikuwa ni sehemu ya sherehe za kipagani zilizogfanyika mwanzoni mwa majira ya baridi (winter). Alionya waachane na matumizi yake, lakini nayo yaliigwa na walioishika Krisimasi.

Jionee pia kile ambacho Cesare Baronius, Mkatholiki aliyeheshimika wa karne ya 16, alichandika:

Ikiwa mishumaa ambayo ilitumiwa kwa ajili ya sherehe ya jua "Saturnalia" sasa inatumika kwenye sherehe yetu ya Kutukuzwa kwa Bikra mama yetu! Kile ni ulizacho, je, inastaajabisha kwamba maaskofu wameruhusu jadi zingine ambazo zilijulikana wazi kuwa ni za watu wapagani, ambazo

kwamba hata baada ya wapagani hao kuongoka na kuwa Wakristo bado hawakuweza kuongozwa kuachana nazo, imeshindikana kuwabadiri ili wamwabudu Mungu wa kweli?" (Baronius, "Annales", ad ann. 58, n. 77). (as cited in Thurston, Herbert. "Lights." The Catholic Encyclopedia. Vol. 9. Nihil Obstat. October 1, 1910. Remy Lafort, Censor. Imprimatur. +Yohana M. Farley, Archbishop of New York. New York: Robert Appleton Company, 1910. 21 Dec. 2009 <<http://www.newadvent.org/cathen/09244b.htm>>).

Hivyo, kimsingi Baronius alibainisha wazi kwamba mishumaa na sherehe za Saturnalia ni miongoni mwa desturi za kipagani, lakini bado kuzitumia ilikuwa inakubalika! Krisimasi kimsingi ni sherehe iliyokarabatiwa ya kipagani iliyoitwa hapo awali Saturnalia. Iliigwa kwa sababu ya kuvutwa kukubaliana na desturi za kipagani.

Pamoja na hayo, hata nakala ya Biblia ya Rheims' ya Agano Jipya (tafsiri ya Kikatholiki wanayoikubali) inaeleza kifuatacho:

15. Na kuna makubaliano gani kati ya Kristo na Beliali? Ama watakatifu wana sehemu gani kati yao na makafiri?
16. Na kuna makubaliano gani kati ya hekalu la Mungu na Sanamu? Maana nyie ni hekalu la Mungu aliye hai. Kama Mungu asemavyo, ndipo nitaishi, na kuenenda kati yao, nami nitakuwa Mungu wao: nao watakuwa watu wangu.
17. Na kwa sababu hiyo, Tokeni kati yao, mkajitenge nao. Asema Bwana wetu, nanyi msiguse kitu kilicho najisi: nami nitawakaribisha kwangu (2 Wakorintho 6:15-17, The Original And True Rheims New Testament Of Anno Domini 1582. Prepared and Edited by Dr. William von Peters, Ph.D. Copyright © 1998, Dr. William G. von Peters. Ph.D. 2004, copyright assigned to VSC Corp.).

Tambua kwamba desturi chafu (najisi) zihusianazo na ibada za sanamu (Upagani) zimekatanzwa na Mungu. Je, hilo haliihusishi pia sherehe za kipagani ambazo zimeazimwa na kuletwa kwenye ukristo wa leo?

Saturnalia ya Ki-Roma pamoja na Mithraism ya Ki-Persia vyote viliigwa toka dini za upagani wa kale—kutoka kwenye dini za kipagani ya Siri ya Kibabeli. Wa-Babeli ya kale walisherehekea kuzaliwa kwa Nimrod mfalme wao (reborn Nimrod) akiwa kama muungu wao Tammuz (newborn Tammuz) kwa kuuabudu mti wa majani ya kijani yasiyonyauka. Wa babeli ya kale pia waliifanya sherehe hiyo ya kuzaliwa wakati wa majira ya baridi kwenye tarehe za kuchipuka kwa jua (winter solstice). Yeremia aliwakemea Waisraeli wa kale wasiige upagani huo, na akakemea matumizi ya kipagani ya mti wa kijani, soma Yeremia 10:2-4 na mti usionyauka wa kijani katika Yeremia 3:13.

Kulipeleka swala hili mbele zaidi, jionee kwamba kutumia miti ya kijani kama sehemu ya ibada ilikemewa na Mungu tangu zamani kwa miaka maelfu kabla:

"2Haribuni kabisa kila mahali pao pa kuabudia kwenye milima mirefu, vilima na chini ya kila mti mkubwa ambamo mataifa haya mnayokwenda kuchukua ardhi yao huabudia miungu yao. 3Bomoeni madhabau zao, vunjeni yale mawe wanayoabudu, chomeni moto nguzo zao za Ashera, katilieni mbali sanamu za miungu yao na mfute majina yao mahali

hapo" (Torati 12:2-3).

"2Haribuni kabisa kila mahali pao pa kuabudia kwenye milima mirefu, vilima na chini ya kila mti mkubwa ambamo mataifa haya mnayokwenda kuchukua ardhi yao huabudia miungu yao. 3Bomoeni madhabau zao, vunjeni yale mawe wanayoabudu, chomeni moto nguzo zao za Ashera, katilieni mbali sanamu za miungu yao na mfute majina yao mahali hapo. 4Kamwe msimwabudu BWANA Mungu wenu kama wanavyoabudu wao" (Torati 12:2-4).

"16Jihadharini, la sivyo mtashawishika kugeuka na kuabudu miungu mingine na kuisujudia" (Torati 11:16).

"9Wakati mtakapoingia katika nchi ambayo BWANA Mungu wenu anawapa, msijifunze kuiga njia za machukizo za mataifa ya huko. 12Mtu ye yote afanyaye mambo haya ni chukizo kwa BWANA, tena ni kwa sababu ya matendo haya ya kuchukiza wayafanyayo ndiyo maana BWANA Mungu wenu atayafukuza mataifa hayo mbele yenu" (Torati 18:9,12).

"24Mungu ni Roho na wote wanaomwabudu imewapasa kumwabudu katika roho na kweli" (Yohana 4:24).

Tafsiri za Kikatholiki za Biblia zinaonyesha wazi kwamba kusimika miti ya kijani yenye kivuli, haikutakiwa iwe sehemu ya kumwabudu Mungu wa kweli—na kwamba watu hawatakiwi kuhadaika na kutumia desturi zingine za kigeni. Ukweli ni kwamba Krisimasi inatukumbusha kwamba watu mara nyingi hawako tayari kumwabudu Mungu kwa mfumo anaoutaka Yeye, bali badala yake hupendelea kuiga desturi za kipagani ambazo wao huziona zinafaa ilimradi tu ziiitwe kwa majina ya kibiblia ama waziite zinamhusu Yesu.

Wasomi wa Kikatholiki Wanajua

Nakala ya Biblia ya Rheims inafundisha:

"22Basi iweni watendaji wa Neno wala msiwe wasikiaji tu, huku mkijidanganya nafsi zenu" (Yakobo 1:22).

Wasomi wa Kikatholiki wanaelewa wazi kabisa kwamba Krisimasi haikutoka katika Biblia, kwamba Disemba 25 ilikuwa ni sikukuu ya kuzaliwa kwa muungu wa kipagani, na kwamba mengi ya mambo yafanyikayo wakati wa Krisimasi yametokana na mila za ibada za kipagani.

Lakini wao pamoja na kanisa lao bado wanaruhusu sherehe na ibada hizi pasipo kujali. Wanajidanganya wenyewe huku wakifahamu wazi.

Wale wanao yaamini maneno ya Kristo kiukweli, "Wanadamu hawataishi kwa mkate pekee bali kutokana na kila neno litokalo kwenye pumzi ya kinywa cha Mungu" (Mathayo 4:4); hawataendelea kuisherehekea sikukuu ya kipagani kama Krisimasi kwa sababu inadesturi na matendo yaliyoonywa na kukataliwa na Biblia na haikuwahi kushikwa na waumini wa kweli wa mwanzo.

Sisi tulio wa kanisa la Continuing Church of God kamwe hatusherehekei Krisimasi.

Kuitekeleza  
Mathayo 24:14  
Pamoja na  
Mathayo 28:19-20



*Website ya Kanisa la Continuing Church of God: [www.ccog.org](http://www.ccog.org)  
Website ya Taarifa za Unabii wa Biblia za Kilasiku: [www.cogwriter.com](http://www.cogwriter.com)*

**CCOG.ASIA:** Hii ni Website ilengayo wasomaji kutoka Asia. Inazo makala katika lugha ya Kichina cha Mandarin pia na katika Kiingereza pamoja na lugha zingine za Kiasia.

**CCOG.IN:** Hii ni Website inayolenga wale walio wa asili ya kihindi.

**CCOG.EU:** Hii ni Website kwa wale wa Ulaya. Inazo makala katika lugha nyingi za Ulaya.

**CDLIDD.ES:** Hii ni website ya Continuing Church of God katika lugha ya Kihispania.

**PNIND.PH:** Hii ni Website kwa ajili ya wale wa Ufilipino ama wenye asili yao.

---



***Chaneli ya Habari za Unabii wa Biblia***  
*[www.youtube.com/BibleNewsProphecy](http://www.youtube.com/BibleNewsProphecy)*

***Chaneli ya kanisa la ContinuingCOG***  
*[www.youtube.com/continuingcog](http://www.youtube.com/continuingcog)*

---

Mchungaji Mwandamizi wa Continuing Church of God ni mgeni mwalikwa mara kwa mara kwenye radio, akitumia radio kuwafikia wasikilizaji wa maeneo mengi.

Kanisa la Continuing Church of God pia hutumia majarida pamoja na magazeti ya kielectronic, vitabu na barua za kila juma kwa waumini wake katika nkutekeleza Mathayo 24:14 pamoja na Mathayo 28:19—20

